*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

### Kikao cha Tisa – Tarehe 13 Desemba, 2013

*(Mkutano ulianza saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

Mwenyekiti (Mhe. Mussa Zungu Azzan) Alisoma

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. JUMA SURURU JUMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII):**

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka 2013.

**MHE. SAID MTANDA (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE NA MAENDELEO YA JAMII):**

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka 2013.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 92

**Hitaji la Gari la Wagonjwa Jimbo la Mwibara.**

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA** aliuliza:-

Je, ni lini Jimbo la Mwibara litapatiwa gari la kubebea wagonjwa hususan katika Kituo cha Afya cha Kasahunga?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu**:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kangi Lugola, Mbunge wa Jimbo la Mwibara, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna tatizo la kukosekana kwa gari la wagonjwa katika kituo cha Afya cha Kasahunga kilichoko katika Jimbo la Mwibara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ina jumla ya vituo 48 vya kutolea huduma za afya ambavyo ni Hospitali 2 vituo vya Afya 6 na Zahanati 40. Hospitali zilizopo ni pamoja na Hospitali ya Bunda *DDH* na Hospitali ya *Mission* ya Kibara. Vituo vya Afya ni Ikizu, Kasahunga, Kasuguti, Manyamanyama, Kisolya na Mugeta.

Wilaya ina Zahanati 34 za Kiserikali, Zahanati za watu binafsi ziko 3 na Zahanati za Mashirikia ya Dini ziko 3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ina gari moja tu la kubebea wagonjwa yaani *"ambulance"* linalotoa huduma katika vituo vyote 48 na kuna pikipiki 4 za kubebea akina mama wajawazito katika vituo vya Afya vya Kasahunga na Kisolya kwa upande wa Jimbo la Mwibara, Ikizu na Mgeta kwa upande wa Jimbo la Bunda.

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (TAMISEMI)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na tatizo hili Halmashauri ya Wilaya ya Bunda imeweka kipaumbele kwenye mpango wa Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2014/2015 kwa ajili ya kununua gari la wagonjwa litakalotumika kutoa huduma katika vituo vyote vya Afya vilivyopo katika Wilaya ya Bunda ikiwemo kituo cha Kasahunga.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Alphaxard Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo la kutokuwa na magari ya wagonjwa kwenye Vituo vya Afya vilivyopo hapa Nchini sababu mojawapo ni kutogawana rasilimali kwa usawa. Na kwa kuwa upo ushahidi kwamba Wilaya zingine zina magari ya kubebea wagonjwa zaidi ya 5.

Kwa mfano Wilaya ya Mheshimiwa Naibu Waziri anayetoa majibu hapa ana ambulance zaidi ya 5 wakati Wilaya yake ukubwa ni mdogo kuliko Bunda, Idadi ya watu ni wachache kuliko Bunda. Nataka aniambie kama kuna upungufu wa chakula eneo moja, tunachukua chakula sehemu yenye ziada tunapeleka sehemu nyingine.

Je, yuko tayari kwa njaa ya *ambulance* tulizonazo Wilaya ya Bunda afanye *reallocation* atoe angalau *ambulance* moja kutoka kwenye Wilaya yake?

Kwa kuwa hizi pikipiki anazozungumzia ni pikipiki zilizonunuliwa kwa kulidanganya Bunge hili kwamba zitabeba wagonjwa ni bodaboda.

Je, atakubaliana na mimi kwamba pikipiki hizi ni za kisanii, hazisaidii Wananchi wa Wilaya ya Bunda na Mwibara na yuko tayari Bunge lijalo la Bajeti nitatumia pesa zangu kukodi Fuso na kuisafirisha pikipiki anayoisema ili niilete kwenye viwanja vya Bunge na nikiruhusiwa niiingize humu ndani ili aniambie kama kweli hiyo pikipiki inabeba wagonjwa kwenye Kata ya Kasahunga, yuko tayari niibebe niilete?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba nijibu maswali mawili ya Ndugu yangu Mheshimiwa Lugola, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Kwanza nashukuru sana, mimi napenda hizi *vibration* za namna hii. Mao wa China alisema hivi: *No research no right to speak.* Nataka niliweke vizuri. Kwanza hili linalohusu Wilaya ya Siha mimi ndiye Mbunge wa Siha nataka *declare interest* kwako. Bahati nzuri na tena namshukuru Mungu aliyeko juu Mbinguni kwamba jambo hili linakuja hapa kwa namna hii ili nieleze. Gari moja la kisasa lililoko katika Wilaya ya Siha, la kisasa zuri lina na *Oxygen* ndani yake limetoka Australia limetolewa na Dkt. Masika, ambalo alimkabidhi Mheshimiwa Rais moja kwa moja kwa maana ya Wilaya ya Siha.

Gari lingine lililoko pale limetolewa na *UNICEF* liko pale, gari lililokuja ambalo limetoka hapa linalotoka TAMISEMI ni moja ndilo ninalolifahamu. Tutume watu wa hapa tusitake kuleta *impression* za ajabu hapa, watu wakatuona kwamba ni watu wa ajabu. Mheshimiwa Lugola kama una tatizo la gari zungumza yako maeneo mengine ambayo yana matatizo kama haya.

Ukienda mahali ambapo palikuwa na mradi, kwa mfano ukienda Karagwe ambapo palikuwa na mradi au ukienda Magu ambapo kuna *UNDP* wamefanya pale utakuta magari pale yanaonekana ni mengi kwa sababu ya mradi ulioko pale au uliopita pale. Magari ambayo yanazungumzwa hapa Mheshimiwa Mwenyekiti nataka niliweke wazi na namshukuru Mungu kwamba jambo hili linakuja. Ninajua kwamba ni nini kinachozungumzwa hapa.

Magari yaliyokuja nyuma pale TAMISEMI yalikuwa magari 63 kama ninakumbuka vizuri kwa sababu *figure* hizi nazikumbuka kumbuka hivi. Ninaweza nikawa nimekosea

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



*figures.* Magari haya yalitolewa wakati wa Wajerumani, Denmark walisaidia pamoja na Japan. Hii ilikuwa kwenye mwaka wa 2007 na mwaka wa 2010 ndiyo magari haya yalitolewa. Mradi ule akaletwa hapa Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Waziri Mkuu wakasema tulete orodha:-

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri jibu tu mengine utamalizia baadaye.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Ni msisitizo tu kwamba maana yake hili linalosemwa ni jambo zito hapa. Tukaambiwa kwamba tulete orodha hapa, orodha ikaletwa hapa tukaangalia.

Kutoka wakati ule yalipogawanywa magari yale mzee wangu, hayajagawanywa tena mpaka leo tunapozungumza hapa. Kwa hiyo, mradi ule ukawa haupo.

Mheshimwa Mwenyekiti, kuhusu pikipiki hayo mengine tutaelezana na Ndugu Lugola tutazungumza vizuri tutaelewana. Atajua tu tunachozungumza hapa, pikipiki hizi Mheshimiwa Mwenyekiti sisi ni Watanzania, akina mama wamewahi kubebwa kwa chekecheke hapa, akina mama kule vijijini wanapata matatizo ndugu zangu tunazungumza hapa. Sisi tunafahamu kwamba akina mama walikuwa wanachukuliwa kwa shida sana, anapelekwa, anabebwa. Tumekwenda mahali tukazipata hizi pikipiki sasa pikipiki hizi zimegeuka tena na sisi wenyewe tuliambiwa hapa kwamba pikipiki walau zisaidie kuondoa hili tatizo lililokuweko kule sasa Mheshimiwa Lugola unataka kupakia pikipiki kwenye Fuso kuiletea hapa. Mimi nisingeangalia zaidi pikipiki ningeangalia jitihada za Serikali za kuangalia tatizo hilo ili tuondokane na matatizo tuliyonayo.

Nakubali kwamba hizi katika hali ya Tanzania tuliyonayo Mheshimiwa Mwenyekiti ni kweli kuna maeneo mengine ya Tanzania ambayo pikipiki haziwezi kusaidia lakini wakati mwingine tumechomoa kile kitanda tukatumia pikipiki yenyewe katika kutoa hizo huduma.

Naomba Mheshimiwa Lugola asitupelekee pikipiki hapa abaki nazo kule ziendelee kusaidia wananchi wakati tunafikiria namna ya kumsaidia kupata tumetenga million 150 zinaingizwa katika bajeti hii kwa ajili ya kumsaidia kwenda kununua gari.

Aje tuzungumze tusaidiane gari liweze kupatikana kwa ajili ya kusaidia kituo cha Kasahunga. Lakini gari litakapopatikana Mheshimiwa Mwenyekiti litapelekwa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda halitapelekwa Mwibara. Jimbo halitengewi gari, gari likihabirika wanaotengeneza gari lile ni Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Mwanri ambaye alifanya jitihada kubwa sana kuhakikisha kwamba Hospitali yetu ya Wilaya ya Iringa inafunguliwa kwa haraka sana. Lakini tatizo kubwa lilikoko katika Hospitali ile ni gari la wagonjwa.

Je, Serikali inaweka vigezo gani katika kugawanya haya magari kwa sababu kila Mbunge anayesimama analalamikia haya magari ya wagonjwa?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, kwa kifupi Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba Mheshimiwa Kabati arudie hiyo sehemu ya mwisho sikumpata vizuri.

**MHE. RITTA E. KABARI:** Ni vigezo gani vinatumika katika kugawanya haya magari katika Hospitali zetu na vituo vyetu vya Afya kwa sababu imekuwa malalamiko ya kila Mbunge anayesimama hapa Bungeni.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kabati Mbunge wa Viti maalum, kama ifuatavyo:-

Kwanza kumshukuru kumwambia asante dada yangu, nimekwenda kule tumesaidiana naye ni kweli kwamba pale palikuwa na matatizo lakini tumeona jitihada ambazo anazifanya Mheshimiwa Mbunge wa Viti maalum katika lile eneo na tunampongeza sana kwa kazi nzuri anayofanya pale.

Swali linaloulizwa Mheshimiwa Mwenyekiti nimeulizwa na Mheshimiwa Kabati sasa naona kuna maswali mengine ya nyongeza kama unaniruhusu nijibu na hayo mengine ambayo yanaulizwa:-

**MWENYEKITI**: zungumza na meza endelea na hilo la Mheshimiwa Kabati.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Niendelee na hili la Mheshimiwa Kabati tu ee!

**MWENYEKITI:** *YES!*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tunafanyafanyaje, kwa kule nyuma kama nilivyoeleza hapa, magari yaliwahi kuja ya misaada hayo niliyoyasema yaliletwa kwetu sisi TAMISEMI yaliletwa na hao walioleta misaada yakagawanywa katika Halmashauri na Halmashauri zilizopewa magari haya ni Halmashauri zile mpya.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Halmashauri zilizopewa ni zile mpya walio wengi waliopewa haya magari ni wale waliotoka katika zile Halmashauri mpya, lakini kama nilivyokueleza kama wale wanaotoa msaada huu wangeendelea kutoa msaada mana yake tungeendelea hivyo hivyo kwa utaratibu huo huo na hao wengine ambao wanazungumza hapa wangepata.

Kwa sasa tunachofanya hapa Halmashauri inachofanya inaomba yenyewe Halmashauri inaiingiza katika mpango huu na inaingiza katika Bajeti yake.

Lakini kwa maneno mengine hawezi akatoka Mbunge akasema hivi nataka mimi TAMISEMI mniletee hapa *Ambulance,* na ndio maana nilipokuwa najibu hili swali la Mwibara, Mheshimiwa Mwenyekiti nilikuwa nasema hapa kwamba watatakiwa wawe wameonyesha katika Bajeti yao sasa katika Bajeti yao hawa nitakwenda kuangalia kama wame *capture* na sasa hivi tunapozungumza hapa ndio Bajeti zinaendelea.

Kwa hiyo, rai yangu kwa Wabunge wote ni kwamba sasa hivi kama kuna mtu anafikiria kwamba zitakuja nyingine ule mradi wa Denmark pamoja na ule wa Japan, mimi sikumbuki mara ya mwisho ilikuwa ni mwaka 2010/2011.

Sijawahi kusikia tena zimegawanywa pale. Zingegawanywa na mimi niko pale ningejua kabisa kwamba tutafanya kazi hiyo. Kwa hiyo, ninataka niseme hilo kwamba kumekuwa kuna hilo. Kwa hiyo Mheshimiwa Kabati ni hilo.

Hili analolizungumza hapa la vitanda Mheshimiwa Mbunge amepeleka vitanda pale.....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, inatosha. Sasa Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru niulize swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Mwenyekiti tatizo la hizi Bajaji za miguu mitatu kwa ajili ya akinamama wajawazito ni tatizo kubwa kwa nchi nzima. Mabajaji hayo yamekosa madereva.

Mimi naomba nipate kauli ya Serikali juu ya Wakurugenzi ambao wameshindwa kupata madereva wa kuendesha hizo Bajaji kitu ambacho kimesababisha wananchi kutafuta wao madereva na huduma hiyo imekuwa haipatikani kwa urahisi.

Ni kauli gani ya Serikali kwa hao Wakurugenzi ambao wameshindwa kuendesha vyombo hivyo?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pauline Gekul, kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Mwenyekiti, anachosema ni sahihi naelewa kwamba ambacho kingetakiwa kifanyike hapa ni kila unapokuwa na hiyo Bajaji hiyo *ambulance* ya kibajaji bajaji unatakiwa uwe na dereva wake anayeendesha pale na wakati mwingine tumekuwa na matatizo hayo.

Lakini hasa hasa niseme kwamba desturi imekuwa ni nini ili wengine waweze kuelewa, tumetaka zaidi kwa sababu zinapelekwa katika vituo vya Afya na katika Zahanati wale wanaoendesha kituo pale wao wenyewe kwanza tunataka wajue jinsi ya kuiendesha. Wale wanaoendesha kile kituo wajue jinsi ya kuiendesha ile Bajaji pale kwa sababu wakati mwingine ni watu wa kawaida pale wanaweza wakamchukua Mhudumu pale, Mhudumu akawa anafanya kazi zake za uhudumu lakini wakati huo huo akawa anajua jinsi ya kuiendesha ile bajaji pale inayoendeshwa pale.

Lakini kama unavyosema, ukisema pale kwa resources tulizonazo na kwa hali halisi ya Halmashauri kwamba kila bajaji pale umpatie dereva wake pale na nini na nini wakati mwingine mnaweza mkafika mahali mkapata matatizo sana katika suala la kuhakikisha kwamba wanapata masuala yao na marupurupu.

Lakini hata hivyo naomba nitataka kulistadi vizuri hili unalolizungumza hapa ili tuone hata kama kwa sababu kwamba sio kila wakati bajaji inaitishwa ni wakati kunapokuwa na *emergency.*

Kwa hiyo kama ziko tatu nne tano pale tunaweza tuaona kwamba tukawa na dereva mmoja pale ambaye ni *Competent* lakini sasa ujue kwamba hizi zinakaa katika vituo. Lakini sana sana tunachotaka kushauri hapa ni kuhakikisha wale wanaoendesha kituo kile wenyewe wanajua jinsi ya kuiendesha ile Bajaj.

**MWENYEKITI**: Tunaendelea Wizara ya Maji Mheshimiwa Kiwanga.

Na. 93

**Tatizo Sugu la Maji**

**MHE. PAULINE P. GEKUL (K.n.y. MHE. SUSAN L. KIWANGA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sana tangu tupate uhuru wananchi wengi wa Igunga wamekosa maji kwa matumizi yao na kwa mifugo yao.

Je, ni lini Serikali itawapatia wananchi hao maji kwa matumizi yao (maji salama) na maji kwa ajili ya mifugo yao ili kuwaondolea adha kubwa wanayopata kila siku kuhangaika kutafuta maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Kiwanga Mbunge wa Viti maalum, kama ifuavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutatua tatizo la maji lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji kupitia mradi wa vijiji 10 katika Halmashauri ya Igunga ambapo ujenzi wa miundombinu ya maji umekamilika katika vijiji 2 vya Mwandihimiji na Matinje. Katika vijiji vya Bulangamilwa, Bulembela, Mwalala na Mgongoro ujenzi wa miundombinu ya maji umeanza na upo katika hatua mbalimbali.

Vijiji vya Isenegeja, Mwabakima, Mwamashimba na Mwamala vipo katika hatua za mwisho za usanifu na uandaaji wa makabrasha ya Zabuni Aidha Serikali imeboresha huduma ya maji katika vijiji 3 vya Mbutu, Butamisuzi na Handishi baada ya kukamilisha mradi mkubwa wa maji katika mji wa Igunga.

Katika mipango ya muda mrefu ya kutatua tatizo la maji Igunga Serikali imeanza kutekeleza mradi wa kujenga bomba la kutoa maji Ziwa Victoria hadi kufikisha Tabora Mjini ikihusisha Miji ya Nzega, Igunga pamoja na vijiji vyote ambavyo vitakuwa umbali usiozidi kilomita 12 kwa sasa kila upande kutoka kwenye bomba.

Mtaalamu mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni atapatikana mwishoni mwa mwezi Desemba 2013. Pia Serikali imeingia makubaliano na Kampuni ya Serikali ya India *WAPCOS* kufanya tathmini ya mradi huo pamoja na gharama za utekelezaji. Kazi hiyo imekamilika na imewasilishwa Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Serikali inafanya utafiti katika maeneo ya Igurubi, Choma, Chankola, Itumba na Simbo kwa ajili ya kuchimba mabwawa makubwa na madogo yatakayotoa huduma kwa wananchi na mifugo.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Susan Kiwanga swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri, tatizo la maji Igunga, Serikali inalifahamu na Wabunge wengi waliokwenda kwenye kampeni wanalifahamu.

Kuna baadhi ya maeneo ambayo inabidi watumie punda kutafuta hayo maji zaidi ya kilomita 10 au 20. Mfano maeneo ya Genyawa, Chagana, Igoweko na Simbo; hali ni mbaya sana kwa Jimbo la Igunga. Na Mheshimiwa unasema mkakati uliopo ni wa kutumia mradi huu wa Ziwa Victoria na *World Bank,* miradi ambayo ni ya muda mrefu sana:-

Naomba nifahamu, kufanya hivi Serikali haioni kwamba imewatelekeza wananchi wa Igunga? Kama haijawatelekeza, mko tayari kutenga fedha za ndani kuwasaidia wale wananchi wa Igunga kwa sababu waliwapa kura za kishindo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Swali la pili. Mradi wa *World bank Phase III*, maji kutoka kwa wananchi baada ya kuchimbwa kwenye visima na maji yamepatikana, hiyo *Phase III* haijaanza.

Mfano mzuri ni wananchi wangu wa Mkoa wa Manyara, pale Babati katika Kisima cha Nakwa na Kisima cha Kiongozi, maji yako tayari miaka mitatu hayaendi kwa wananchi wakayatumia. Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini mkakati huu wa kuwapatia maji wananchi na wakaanza kutumia, ni lini mkakati huu utaanza sasa rasmi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Pauline Gekul, kama ifuatavyo:-

Kwanza nimwombe Mbunge kwamba siyo kweli kwamba Serikali imewatelekeza wananchi wa Igunga, Serikali

imefanya kazi kubwa pale. Katika jibu la msingi kama umeliona, tumejenga mradi mkubwa wa maji pale Mjini Igunga ambao tumetumia bilioni sita, na wananchi wameshaanza kupata maji pale. *(Makofi)*

Lakini vile vile Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Serikali imetoa kipaumbele kwa Igunga baada ya kupata visima 144 vya Serikali ya Japan, imeelekeza visima 12 kwa ajili ya Igunga. Kwa Mkoa mzima wa Tabora watapata visima hivyo. Lakini tatu, *World Vision* wanasaidia miradi ya maji pale. Kwa hiyo, ninataka nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inajali sana, na hii ni kazi kubwa sana inayofanywa na Mheshimiwa Dkt. Kafumu ambaye kwa kweli anafuatilia sana. Wanasema Simba mwenda kimya ndiye mla nyama. Anaonekana mkimya, lakini anafuatilia sana miradi ya maji. *(Makofi)*

Swali la pili na Mheshikiwa Gekul, naomba nitumie fursa hii kuwaeleza Watanzania kwamba hatuna *Phase III*. Tuna *Phase I* na *Phase II*. *Phase I* ndiyo tunayoitekeleza sasa hivi, ya vijiji kumi kila Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mbunge kwamba mradi wa vijiji kumi umekwishaanza kutekelezwa na matokeo yameanza kuonekana na Wabunge ni mashahidi. Kwenye Jimbo hili la Igunga, nimesema vijiji viwili vimekamilika.

Nadhani hili mngeshukuru kama ni juhudi ambazo zinafanywa na Serikali ya Awamu ya Nne. Tumesema kwamba *Phase* hii ya Kwanza ambayo ni ya vijiji kumi vya Halmashauri, tumechukua vijiji 1449 kwa Tanzania nzima, kila Halmashauri kumi kumi; na vijiji hivi vitakamilika mwezi wa sita mwaka kesho. Karibu vijiji vingine vimeshakwisha karibu nusu katika Halmashauri zingine. Kwa hiyo nataka nimhakikishie kwamba mipango ya Serikali ya Awamu ya Nne inatekelezeka. Lakini vile vile nimhakikishie kwamba Awamu ya pili sasa ndiyo inaaza mwezi wa sita mwaka kesho, na tutachukua vijiji kuanzia 20 mpaka 30 kila Halmashauri. *(Makofi)*

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi mimi mwenye Mbunge wa Jimbo lenyewe niulize swali moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali katika kutakeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 mpaka 2015, imeweza kupeleka maji safi na salama katika Mji wa Igunga na kwa kuwa katika kipindi hiki kifupi cha ubunge wangu, Serikali pia imeanza kujenga mabwawa katika Vijiji vya Itumba, Igurubi, Choma, Mngazi, Mwazizi na vijiji vingine.

Serikali inaiambia nini au inaliambia nini Bunge lako Tukufu hili katika kukamilisha mradi wa kuleta maji kutoka Ziwa Victoria mpaka Igunga, ambao ndio utakuwa jibu halisi la uhakika na la mwisho kabisa katika kuleta maji katika Jimbo la Igunga? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kafumu, kama ifuatavyo:-

Kwanza nimshukuru kwa kutambua ile miradi ambayo inatunzwa na awamu hii, ni kweli kama alivyosema. Nataka nimhakikishie kwamba kutoa maji kupeleka Igunga, Nzega na Tabora; ndio mpango ambao tumekwishaanza kuutekeleza. Sasa bahati mbaya hizi taratibu za manunuzi haziwezi kuonekana kwa wananchi, lakini lazima zipitiwe.

Tumekwishaanza kumtafuta mtaalam mshauri atakayeandaa michoro ya kiufundi, na gharama za ule mradi ili utafutiwe fedha uweze kuanza kujengwa. Kama tulipeleka maji Kahama na Shinyanga, haitashindikana kupeleka maji Igunda, Nzega na Tabora.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Na. 94

**Utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Vijiji Kumi Chunya**

**MHE. VICTOR KILASILE MWAMBALAZWA** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitekeleza mpango wa maji safi na salama kupitia mradi wa vijiji kumi kila wilaya, unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

(a) Je, changamoto gani zimejitokeza katika utekelezaji wa mradi huo Wilayani Chunya?

(b) Je, wananchi wa Chunya wamenufaika kwa kiasi gani kutokana na mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalazwa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizojitokeza wakati wa kuanza utekelezaji wa miradi ya vijiji 10 katika Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ni, ni pamoja na taratibu za manunuzi za Benki ya Dunia, zilikuwa mpya kwa Halmashauri zote nchini na Halmashauri hazikuwa na wataalam wenye ujuzi wa kutumia taratibu hizo mpya ambazo zilihusisha Halmashauri kupata vibali mbalimbali kabla ya kuanza ujenzi, yaani *'No Objection'.* Taratibu hizo zimechangia sana kuchelewesha utekelezaji wa miradi hiyo.

Kwa sasa Halmashauri zimeshajengewa uwezo wa kutosha na Serikali imeondoa taratibu za upatikanaji wa vibali vya miradi ya maji ya vijiji 10. Hivyo kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Chunya, ujenzi wa miundombinu ya maji umekamilika katika Kijiji cha Namkukwe, ambapo wananchi wapatao 4,000 wanapata huduma ya maji safi na salama.

Ujenzi wa miundombinu ya maji umeanza na upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji katika Vijiji vya Kiwanja, Mkola, Udinde, Mwambani, Chang'ombe na Mbuyuni, ambapo utakamilika Februari, 2014. Vijiji vya Lupa, Mapogoro, Lualaje, Mwinji, Matwiga, Isangawana na Mtanila vitatumia chanzo cha Bwawa la Matwiga.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji Mdogo wa Makongorosi una wakazi zaidi ya elfu kumi na sita na una kakisima kamoja kadogo sana. Huu mradi wa visima 10 wa *World Bank* walipochimba kwenye mji huo wa Makongorosi walikosa.

Je, Serikali inasemaje katika kuwasaidia wananchi hawa zaidi ya elfu kumi na sita katika Mji Mdogo wa Makongorosi?

Swali la pili. Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake mazuri amesema Kata za Lupa, Mtanila, Lualaje na Matwiga zitafaidika na mradi wa Bwawa la Matwiga. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri mwenyewe amelitembelea bwawa lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa hili toka limeanza kujengwa mwaka 2008, wanakwenda Makandarasi, mafundi wao wanaacha kutengeneza bwawa, wanaanza kulima tumbaku wanaoa wananchi, wanakaa vijijini wanaliacha bwawa. Mwaka 2010 amekwenda Kandarasi na mafundi wake, wameacha kutengeneza bwawa, wanaanza kulima tumbaku, wanaoa wanakaa vijijini. Sasa naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie ni lini Bwawa la Matwiga litajenga na kukamilika? *(Makoffi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Lakini kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mwambalaswa anafuatilia sana miradi ya maendeleo, mimi nimefika kwake na nimeona jinsi jimbo linavyokwenda vizuri.

Swali la kwanza kuhusu Mji Mdogo wa Makongorosi, mji huu naufahamu, ni kweli unakua. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba tunapeleka maji kwenye miji yote na hii miji ambayo inakua haraka tutaipa kipaumbale zaidi na kwa sababu yale maeneo yana tatizo la maji, tutaendelea kufanya utafiti ili tupate visima vya kutosha kuwapatia wananchi wa Makongorosi.

Sehemu ya pili, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, hili bwawa lilishaanza kujengwa mwaka 2009. Lakini yule mkandarasi akafika mahali akalitelekeza lile bwawa, akawa hafanyi kazi. Nimekwenda kulitembelea nimekuta limejengwa kwa kiwango cha chini. Kwa hiyo, tumefanya maamuzi ya kumbadilisha yule mkandarasi.

Jambo zuri sana kwa Mheshimiwa Mwambalaswa kwamba tumechagua mabwawa matatu – la Habia likiwemo na hili la Matwiga, ambayo sasa yatajengwa na wakala wa uchimbaji visima na mabwawa *Drilling and Dams Construction Agency (DDCA)* ambayo iko chini ya Wizara yetu ya Maji. Wana vifaa vya kutosha, na hatua za mwisho wamesaini mkataba nadhani tarehe 12.

Kwa hiyo, wataanza ujenzi wakati wowote. Wananchi wa Matwiga watapata maji na watapata bwawa ambalo ni la uhakika zaidi. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza:-

Kwa kuwa Mji wa Longido ni mji unaokua haraka sana na Naibu Waziri ni shahidi kwamba alipokuja Longido alikuta kwamba hali ni mbaya. Mradi uliokuwepo Longido umeliwa fedha, kwa hiyo siyo mradi ambao wananchi wanautegemea tena. Kwa kuwa tuna mradi wa maji kutoka Mlima Meru unaokuja Mji wa Longido.

Je, Serikali itafanya haraka mradi huo ili wananchi wa Longido wapate maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lekule Laizer, kama ifuatavyo:-

Naye nampongeza sana kwa sababu amekuwa akifuatilia masuala ya maji ndani ya Bunge na nje ya Bunge. Ni kweli pana shida kubwa sana ya maji pale Longido Mjini na katika vijiji kumi tulipata mradi mmoja ambao hata utekelezaji wake haujaenda vizuri.

Kwa hiyo, Serikali imefikia maamuzi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Longido kuona uwezekano wa kutoa maji kwenye Mlima Meru na tayari kazi ya kumpata mtaalam mshauri imeshaanza. Sasa bila mtaalam mshauri kupatikana na kuandaa michoro na gharama za mradi. Hakitawezekana chochote kufanyika kabla ya yeye kukamilisha hizo kazi.

Kwa hiyo, nataka nimwombe Mheshimiwa Mbunge tuvumilie. Maamuzi yameshafanyika, akipatikana mtaalam mshauri atafanya maandalizi ya hiyo michoro, tutajua gharama; tutaanza kutafuta fedha kwa ajili ya kuwapatia wananchi maji ambao watakuwa ni wananchi wa Longido na Arusha Vijijini.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Serikali inajitahidi kutupatia maji safi na salama ya kunywa.

Lakini ningemwomba Mheshimiwa Naibu Waziri atueleze maana ya maji safi na salama. Kwa sababu katika Jiji la Dar es Salaam, ukifungua mabomba maji ni machafu na yana udongo na hayafai kwa matumizi ya kunywa. Lakini wanatuambia maji ni salama na safi ya kunywa. Je, maji ya Dar es Salaam ni safi na salama kwa matumizi ya binadamu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Owenya, kama ifuatavyo:-

Nataka niwahakikishie Watanzania wote waishio Dar es Salaam kuwa maji ya Dar es Salaam ni safi na salama. Wabunge mmekuwa mashahidi hapa kwamba Serikali iondoe *VAT* ya ununuzi wa madawa ambayo yanatumika kutibu yale maji na Serikali kwa kweli imeondoa *VAT* kwenye ununuzi wa madawa ambayo yanatumika kutibu maji Dar es Salaam. Yale maji yanatibiwa, na hatuna taarifa za kitaalam zinazoonyesha kwamba siyo safi na salama.

**MHE. SULEIMAN MASOUD NCHAMBI SULEIMAN:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi Wilayani Kishapu juu ya miradi ya maji katika Vijiji vya Mwigumbi, Bunambiu, Mipa, Iboja, Mwamashimba, Nyenze, Mwamashele, Bubinza Mwamanota na Lagana, inatekelezwa kikamilifu.

Je, Mheshimiwa Waziri wa Maji yuko tayari kufuatana na mimi baada tu ya Bunge hapa tuingie kwenye gari lake ili aende akaone utekelezaji wa miradi ya Chama cha Mapinduzi inavyotekelezwa kwa uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kumjibu Mheshimiwa Nchambi, Mbunge wa Kishapu, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Kwanza namshukuru sana kwa kufuatilia miradi, kiasi kwamba anafahamu ni miradi kiasi gani inatekelezwa na Awamu hii ya nne. Nataka kumhakikishia kwamba mimi niko tayari kufuatana na yeye ili tukaangalie utekelezaji huo na tuone namna ya kuboresha zaidi maeneo ambayo hajafika.

Na. 95

**Kuviwezesha Vikundi vya Kuweka na Kukopa**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Wananchi wengi wamehamasika sana kuanzisha vikundi vya kuweka na kukopa, lakini pamoja na juhudi zao hizo bado walio wengi hawajaweza kukopesheka:-

Je, Serikali inawasaidiaje wananchi hao ili waweze kukopesheka?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya jitihada mbalimbali ili kuwasaidia wananchi waweze kukopesheka. Pamoja na jitihada hizo, Serikali kwanza imeweka taratibu na kanuni za kuanzisha, kusajili na kuendesha vikundi vya ushirika ikiwa ni pamoja na vikundi vya kuweka na kukopa *(SACCOS)* Benki za Jamii Vijijini (VICOBA).

Aidha, Serikali kwa kupitia dirisha la uwezeshaji imeweza kufanikisha uwezeshaji wa makundi mbalimbali yakiwemo wanawake kupitia mifumo inayoratibiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji *(National Empowerment Council)*, mifuko ya uwezeshaji wanawake na vijana inayoratibiwa na Wizara ya Kazi na Ajira na Mfuko wa Rais wa Uwezeshaji. *(Makofi)*

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kufanya jitihada nyinginezo ikiwa ni pamoja na kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo ambayo itatoa mikopo ya muda mfupi, kati na mrefu katika sekta ya kilimo ambayo inajumuisha uvuvi na mifugo; kwa kutambua umuhimu wa Benki ya Wanawake katika kuwakomboa wanawake na wananchi wake.

Serikali imeendelea kuiongeza mtaji benki hii ili iweze kuwahudumia wanawake wengi. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2013 Benki hiyo imekwishatoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 11.6 na chini ya mpango wa kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge Tanzania, wananchi wanaweza kumiliki mali husika kwa kutumia mali zao zilizokwisha rasimishwa kama dhamana katika kupata mikopo na fursa zingine katika uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi zilizotajwa, Serikali pia inafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Taasisi ndogo ndogo, Huduma ya Kifedha ya mwaka 2002 yenye lengo la kuboresha huduma ili kuendana na mabadiliko yanayojitokeza katika sekta ya fedha. Shughuli hiyo inatarajia kukamilika mwezi Juni mwakani ambapo Serikali itaandaa mapendekezo ya sheria ya kusimamia taasisi hizo ambazo itaweka utaratibu wa usimamizi, udhibiti na utoaji leseni, mikopo pamoja na viwango vya riba. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa wanawake wengi na vijana wamehamasika kuanzisha Vikundi vya Kuweka na Kukopa na kwa kuwa Mabenki mengi hutoa mikopo kwa *SACCOS* na VICOBA vilivyoko mjini.

Je, Serikali inatoa tamko gani la kusukuma Mabenki kukopesha *SACCOS* na VICOBA. Mfano katika mikoa ya pembezoni hususan katika Wilaya ya Kasulu, ili wanawake na vijana waweze kunufaika na mikopo hiyo? *(Makofi)*

Kwa kuwa Taasisi za Fedha zinazomilikiwa na Serikali kwa asilimia 100%, Benki ya *Tanzania Postal Bank* na *Twiga Bancop* zinajitahidi sana kuweza kutoa mikopo kwa SACCOS na Vijana. Lakini pamoja na jitihada hizo, zinakabiliwa sana na changamoto ya mtaji kufikia bilioni 15 kama matakwa ya Benki Kuu ili ziweze kuwa Benki za Biashara.

Je, Serikali inatoa tamko gani kuziwezesha Benki hizo ili ziweze kuwa Benki kamili, hatimaye ziweze kutoa huduma ya Benki kikamilifu kwa wanawake na vijana? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Genzabuke kama ifuatavyo:-

Kwanza, nampongeza sana sana kwa jinsi anavyofuatilia kuhakikisha kwamba wanawake pamoja na Vijana wanawezeshwa. Nampongeza sana. Lakini suala la kusukuma Mabenki kwenda vijijini, hili ni kweli Mabenki ni mengi. Tuna Mabenki 52 sasa hivi ya Biashara, mengi yao yapo mjini. Kutokana na hili, kupitia Benki Kuu, tayari mwongozo umeshatolewa wa Mabenki kutumia *Agency Banking*. Yaani siyo lazima wao kama Benki, uende *physically* pale, lakini unaweza kutumia *agency* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba hizi *financial services* zinawafikia walengwa kule vijijini.

Kwa hivyo, hilo linafanyika na najua kwamba kuna Mabenki mengi sasa hivi yanapanua huduma zao kupitia *agency banking*. Sisi kama Serikali tutaendelea kushajiisha na tutaendelea kuwezesha Benki ili tuwawekee mazingira mazuri kwa ajili ya kufanya hiyo *agency banking*.

Ni jana tu hapo tumezindua mpango kabambe wa *financial inclusion*, yaani kuhakikisha kwamba wengi hususan wanawake, hususan vijana; ambao wako vijijini

tunawawezesha kifedha *financial inclussion* jana tumezindua pale Dar es Salaam. Kwa hivyo hilo nalo tutaendelea kulifuatilia kwa makini tuhakikishe kwamba mpaka mwaka 2015 asilimia 50 ya Watanzania hususani Vijana na Wanawake wanakuwa *included* katika hizi *financial services*.

Kuhusiana na kuongeza mitaji, kweli sisi kama Serikali tumekuwa tuna-*allocate* fedha lakini hazitoshi kuwezesha hizi Benki ambazo za Serikali, *ownership* ni ya Serikali asilimia 100 kuweza kuongeza mtaji. Sasa hivi nje ya bajeti lakini angalau tumepata mapendekezo tumepata maombi ya *Seven Billion* kuwezesha Benki ya Twiga Bankcorp kuongeza mtaji. Lakini iko nje ya Bajeti kwahivyo ni kitu ambacho pengine si rahisi sasa hivi kufanya lakini vilevile tutaendelea kushajiisha.

Benki ya Posta sasa hivi wanarekebisha sheria kuhakikisha kwamba ile sheria yao ambayo Benki Kuu inawataka sasa wawe wanatumia Sheria ya Makampuni ili waweze kuwa kama ni Benki inabidi lazima tuibadilishe ili nao waweze kwenda katika soko la mitaji kuweza ku-*raise capital* na kuwawezesha hivi kuongeza mtaji wao ili wananchi wengi zaidi kuweza kupata mikopo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa David Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maeneo ya vijijini ndiko ambako wanawake wengi ni maskini kuliko maeneo ya mijini. Maeneo ya vijijini ndio ambayo yanahitaji sana huduma za kifedha kwa maana ya mikopo kuliko maeneo ya Mijini kwa sababu yao yameshawezeshwa sasa. Serikali itueleze ni mkakati gani wa haraka ambao unaweza kusaidia wanawake wa vijijini kufikishiwa hiyo mikopo kuliko ilivyo hivi sasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kujibu swali moja la nyongeza Mheshimiwa Silinde kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema katika majibu yangu ya ziada kwamba ni jana tu tumezindua mkakati wa *Financial Inclussion*. Mkakati huo *aim* yake kubwa ni kuhakikisha kwamba asilimia 50, sasa hivi tuko 17.9, asilimia 50 ya wananchi wa Tanzania wanakuwa *financially included*.

*Target* hasa ni huko vijijini ambako kweli kama unavyosema kwamba huduma nyingi za kibenki hazipo pale na wale kweli kutokana na *research* mbalimbali imeonekana kwamba wanawake walio vijijini ni maskini zaidi ukilinganisha na wanawake ambao wako mjini.

Kwa hivyo ni jana tu mkakati tumezindua *financial inclussion* tukiwa pamoja na Malkia Maxima wa Netherlands tumezindua pale mkakati na umekuwa ume-*include* takribani vyombo vingi vya fedha. Kwa hivyo tuhakikishe kwamba huo ni mkakati ambao ni wa miaka mitatu mpaka 2015.

Kwa hivyo *this is a quickest way* ambayo tunaweza kufanya lakini vilevile nimesema mwongozo tayari umeshatolewa kwa mabenki kutumia *agency*. Maduka yote yaliyoko vijijini kuweza kutoa huduma za kibenki pamoja na mikopo.

Kwa hivyo hilo nalo lipo ni ma-*banks* tu wao kuweza kutumia fursa hii ambayo Serikali imeweka kuweza kuwafikishia wananchi kule huduma za kibenki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aliko Kibona.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kuwaondolea umaskini wananchi ilikuwa na mpango wa kutengeneza Hatimiliki kwa ajili ya zile hati miliki za kimila kwa wananchi vijijini ili ziwawezeshe kuwa na *access* ya kupata mikopo kwenye mabenki. Nataka kufahamu ni kwa kiwango gani mpaka sasa hivi Hatimiliki za kimila zimewasaidia wananchi hapa nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kibona kama ifuatavyo:-

Ni kweli Serikali kupitia mkakati huu wa MKURABITA imewezesha wananchi kuweza kurasimisha mali zao pamoja na kufanya kupata Hatimiliki za ardhi ili iweze kukopesheka. Hii ni changamoto. Ina changamoto kubwa sana kwa sababu bado baadhi ya Benki zimeendelea kukataa zile Hatimiliki za Kimila kwa ajili ya kuwapa mikopo wananchi.

Lakini naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kulifuatilia na hakika kwamba baadhi ya *Banks* hususani *CRDB* imeanza kukubali kuchukua hizi Hatimiliki kwa ajili ya kuweza kuwakopesha wananchi lakini tutachukua juhudi maalum kuweza kuhakikisha kwamba ni tatizo gani hasa linachangia hizi *banks* zisiweze kukubali zile Hatimiliki za Kimila kwa ajili ya kuwapatia mikopo wananchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea. Swali Namba 96 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Mturano, kwa niaba ya Mheshimiwa Richard Ndassa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Na. 96

**Mechi za Mpira wa Miguu Kusababisha Uchafuzi wa Mazingira**

**MHE. PHILIPA G. MTURANO** aliuliza:-

Mechi zinazochezwa Uwanja wa Taifa huvutia watu wengi na biashara mbalimbali kama vile uuzaji wa Maji, Juice, Mahindi, Karanga na kadhalika hufanyika ambapo baada ya mechi Mazingira huwa machafu kwa utupaji hovyo wa takataka unaofanywa.

(a) Je, Manispaa ya Temeke hupata mgao wowote kutokana na mechi hizo ambazo husababisha uchafuzi wa Mazingira?

(b) Je, ni nani anastahili kuwajibika kwa uharibifu huo wa Mazingira?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philipa Geofrey Mturano, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu a na b kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Temeke haipati mgao wowote wa moja kwa moja kutokana na mechi zinazochezwa Uwanja wa Taifa. Mgao wa Serikali unaotokana na matumizi ya Uwanja wa Taifa huenda moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, kodi inayotozwa kutokana na mapato ya mechi hizo hukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kwa niaba ya Serikali. Mapato yote hayo hutumiwa na Serikali katika kutoa huduma mbalimbali kama vile afya, elimu, miundombinu na kilimo kwa fedha ambazo hutolewa na Serikali kupitia Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kwa njia ya Halmashauri za Wilaya, Miji, Majiji na Manispaa ikiwemo Manispaa ya Temeke.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ujio wa watu wengi katika eneo la Uwanja wa Taifa wakati wa mechi, kwetu sisi tunaona kuwa ni fursa kwa wananchi wa eneo hilo la Manispaa ya Temeke. Matukio yanayofanyika uwanja wa Taifa ni fursa muhimu kwa wananchi wa Temeke kujipatia kipato hususani kwa wafanyabiashara ambao hutoa huduma ya chakula na vinywaji mbalimbali kwa wageni wanaokuja eneo hilo.

Changamoto ya uchafuzi wa mazingira inapojitokeza wakati wa matukio yanayofanyika Uwanja wa Taifa bado imo ndani ya uwezo wa Manispaa ya Temeke.

Tunawashauri Uongozi wa Manispaa ya Temeke kuiona changamoto hiyo kama fursa mojawapo ya kuboresha mapato yao, kuboresha maisha ya wananchi wa eneo hilo na kuweka mipango endelevu ya kuboresha usafi na mazingira katika maeneo yanayouzunguka Uwanja wa Taifa, ikiwa ni pamoja na kusimamia sheria ndogondogo tulizonazo na kuwabana wachafuzi wa Mazingira.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Waziri yasiyokuwa na afya hata kidogo kwa Manispaa ya Temeke, naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mechi zinazochezwa Uwanja wa Taifa pale ni nyingi sana na Wabunge karibu wote mnafahamu. Mechi hizo zinasababisha uuzwaji wa Ubuyu, T-Shirt, Mahindi, vitu vingi na hakuna uzio kwamba sasa Wauzaji mipaka yao itakuwa eneo fulani. Wanazagaa mpaka karibu na maeneo ya Manispaa kabisa, na ni hapohapo ndipo ulipo Uwanja wa Taifa.

Hivi Wizara inashindwa nini kuifikiria Manispaa ya Temeke kuipatia basi angalau hata 0.3 ya mapato yao kwa kusaidia ule usafi kwa sababu hicho kiwango unachokitaja Mheshimiwa Waziri ambacho kinakwenda *TRA* kuhusu masuala ya elimu hiyo ni kwa nchi nzima.

[MHE. PHILIPA G. MTURANO]

Mimi nasemea Manispaa ya Temeke, kwanini msichukue hata fungu kidogo tu likasaidia kufanya usafi huo. Watu wanajisaidia ovyo pale, Mheshimiwa Waziri tafadhali sana naomba jibu zuri kwa Manispaa ya Temeke na Watanzania wanakusikiliza?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa kwamba wakati wa mechi mbalimbali zikichezwa pale katika viwanja vyetu Kiwanja cha Taifa pamoja na Kiwanja cha Uhuru ni nafasi tosha ya Manispaa ya Temeke kuweza kutengeneza biashara.

Lakini pamoja na kusema hivyo niseme tu kwamba tunategemea Manispaa ya Temeke ichukue jukumu hilo lakini pia wachukue utaratibu wa kwa kutengeneza sheria ndogo ndogo kuweza kuhakikisha kwamba wanaweza wakatumia yale maeneo ambayo yako nje ya Uwanja huu wa Taifa pamoja na Uwanja wa Uhuru kuweza kupata mapato mbalimbali.

Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, mapato yale yanayotokana na kiingilio cha Viwanja vyetu vya Taifa pamoja na Kiwanja cha Uhuru. Mapato yale yanaingia ndani ya Serikali ndio mipangilio ilivyo.

Sasa kama yeye anavyofikiria kwamba ingekuwa ni vizuri tukizipata tuwapatie Manispaa ya Temeke waweze kushughulikia masuala ya Mazingira, na mimi niiombe tu kwa nia njema kabisa kwamba tuiombe Halmashauri ya Temeke ichukue jukumu la msingi kabisa la kuhakikisha wanatengeneza mazingira yanayozunguka ule uwanja kuhakikisha kwamba vijana na wananchi wa Temeke wanaweza wakapata mapato mbalimbali. Hawazuiwi kufanya hizo biashara, basi watumie pia kuweza kutoza faini kama wale wanaotumia yale maeneo yanayozunguka wanayatumia kwa namna mbaya. Hizo ndio namna mojawapo ya kuweza kuhakikisha kwamba tunatunza pia mazingira yaliyoko pale pembeni.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Lakini pia lile wazo la kusema kwamba tuweze kuwapatia pesa zile tunazozipata ambazo zinakwenda Serikalini na sisi pia kama Wizara ni kitu ambacho tumekifikiria kwa kiasi kikubwa. Sio kwa kuzipeleka Manispaa ya Temeke lakini pia ziweze kubaki kuweza kushughulikia kile kiwanja/ viwanja mbalimbali pale mahali palipo.

Tabia ya watu kwenda hovyo hovyo kuchafua mazingira maana yake amezungumza hata masuala kwamba wanakojoa pembeni pembeni, sasa hiyo ni utamaduni mchafu ambao unahitajiwa upigwe vita kwa bidii zote sio katika viwanja tu vya pale Temeke lakini ni katika sehemu zote za jiji na kadhalika, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein.

**MHE. YUSUPH SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Nakushukuru sana na naomba niulize swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikisoma Ripoti ya Mazingira ya nchi ya Sweden, niliona kwamba mifuko ya *plastic* na *filter* za sigara zinachukua kati ya miaka 200 hadi 400 kufaitika katika ardhi. Suala la msingi lililoulizwa hapa ni kuhusu linahusiana na vitu hivi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba hili suala la *plastic* tunalizuia katika nchi yetu kama ambavyo Zanzibar wameanza sasa hivi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajaribu kujibu hili swali la Mheshimiwa Yussuf Salim Hyssein ambalo kwa kiasi kikubwa naliona limetoka mno nje ya masuala yangu ya Michezo. Lakini kimsingi takataka za *plastic* ni takataka ambazo si huko Sweden tu hata hapa kwetu nchini tumeanza kuweka mikakati maalum ya kuhakikisha tunapambana nazo.

Labda nizungumzie kwa upande wa Sweden kwa wenzetu ambako wameshapiga hatua na utamaduni madhubuti wa kuweza kudhibiti takataka mbalimbali. Huwa wanazitenganisha. Sasa sisi bado tumefikia mahali hata

ukichukua pipi au ukienda madukani unataka utiliwe vitu vyako ndani ya mfuko wa *plastic.* Sasa niseme tu kwa taarifa nilizonazo ambazo nadhani zinaweza zikafanyiwa kazi zaidi au Waziri wa Mazingira au wanaohusiana na mazingira wakazizungumzia zaidi ni kwamba sheria ambayo inatuweka sasa hivi viko matakataka ya plastic ambayo hayaruhusiwi kuingia humu nchini lakini hata ile mifuko ya *plastic* ambayo inachukua miaka mingi sana kuharibika kuweza kuoza hairuhusiwi kuingizwa humu nchini.

Kwa hiyo, mimi nadhani kwa kiasi kikubwa Serikali inatambua hilo lakini kubwa zaidi ni wananchi wenyewe wachukue jukumu mikononi mwao kwa sababu mwisho wa siku Serikali ndio hiyo hiyo ambayo ni sisi wananchi tunaitengeneza, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto utamalizia na Ndassa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba Michezo na hasa Soka inaunganisha sana Watanzania. Ni dhahiri kwamba ukitaka kuona namna gani ambavyo Watanzania wanaipenda nchi yao ni pale ambapo Timu yetu ya *Taifa Stars* inacheza. Hata hivyo, kuna changamoto kubwa sana ya uendelezaji wa vipaji.

Serikali haioni kwamba imefikia wakati muafaka, kodi ambazo inakusanya kutoka kwenye viingilio viwanjani zikatumika kuanzisha Mfuko wa kuendeleza soka ili kujenga viwanja vya kutosha na kuhakikisha kwamba tunakuwa tunaendeleza vipaji vya vijana kuwa na timu ya Taifa imara?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zitto ambalo kwa kiasi kikubwa nadhani ni swali la muhimu sana. Lakini pia na angalizo na kutuelekeza kwamba wananchi wanapenda sana soka. Ni kweli katika michezo tunapozungumzia michezo hasa kwa upande wa Tanzania na wananchi kwa ujumla soka ndio wanaiangalia kwa kiasi kikubwa kama ndio mchezo ambao unavuta watu wengi sana na unawaweka pamoja.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Ni mchezo ambao unaweza ukawezekana kwa hapa kwetu Tanzania kama tukijipanga vizuri. *(Makofi)*

Nakubaliana kwa kiasi kikubwa kama kungekuwa kuna uwezekano kwa Serikali kuweza kutenga hayo mapato yanayotokana na viingilio kuweza kuendeleza soka nchini ingekuwa ni vizuri.

Sisi kama Wizara tumejipanga ni wazo zuri lakini linaendana na ombi ambalo sisi kama Wizara pia tumekwishaiomba Serikali kuweza kuangalia vile viingilio vinavyopatikana na yale mapato tunayoyapata katika viingilio mbalimbali tuweze kuvirudisha moja kwa moja vibaki wizarani kusudi tuweze kuvirudisha moja kwa moja katika kusimamia masuala ya maendeleo ya michezo na hasa soka kuweza kutengeneza miundombinu mbalimbali.

Pamoja na kutafuta vifaa lakini pia kuweza ku-*train* Makocha mbalimbali; lakini kubwa kabisa kusimamia kile Chuo chetu cha Michezo cha Malya ambacho kinaweza kikatoa viongozi mbalimbali wa kuweza kuendesha michezo mbalimbali katika ngazi mbalimbali za Taifa. Ahsante sana.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani *(FIFA)* mliahidi kutengeneza uwanja wa Nyamagana na kuuwekea nyasi bandia.

Je, mpango huo sasa umefikia wapi?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ndassa kuhusu ahadi ambayo *FIFA* iliitoa kuweza kuutengeneza Uwanja wa Nyamagana na kuuweka Nyasi za bandia na kwamba hadi sasa hivi imefikia wapi.

[WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO]

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme tu hilo ni suala ambalo hata sisi kama Wizara tumekuwa tunafuatilia kwa muda mrefu sasa kwa kupitia *TFF,* lakini kimsingi ni kwamba *FIFA* walikuwa wameahidi watatoa Dola laki tano *(USD. 500,000)* kwa ajili ya uwekaji Nyasi za bandia kwenye Uwanja wa Nyamagana.

Lakini kabla ya kufanya hivyo ilipangiwa kwamba Manispaa lazima ichangie Dola 118 ili kuziba pengo ambalo litaweza kujitokeza. Kwa hiyo kwa maana hiyo basi kwa ujumla tunatakiwa tupate zaidi ya Dola 618,000 kutoka *FIFA* ili ule uwanja uweze kukamilika.

Lakini mpaka sasa hivi *TFF* kwa taarifa nilizonazo ni kwamba *TFF* imekwishatayarisha na kuandaa Rasimu ya Makubaliano ya Mkataba kwa Uongozi wa Manispaa ili waweze kuuona na kuweza kujiridhisha.

Mpaka sasa hivi Manispaa bado haijajibu. Kwa hiyo nataka nichukue nafasi hii niwahimize kabisa Manispaa ya hapo iweze kushirikiana kwa karibu, waweze kurudisha majibu kamili kwa *TFF* ili *TFF* iweze kushirikiana na *FIFA* kuhakikisha ule uwanja unajengwa haraka iwezekanavyo.

Kimsingi ni uwanja ambao ni muhimu tuwe nao pale Mwanza kama msemaji aliyemaliza alivyozungumzia ni miundombinu mojawapo ambayo ni muhimu tuwe nayo. Tukiwa na miundombinu mizuri ya namna hiyo itakuwa ni vizuri, itakuwa inatupa na sisi pia biashara kubwa ya kuweza kupata mechi nyingine mbalimbali kubwakubwa za Kimataifa kuweza kuchezwa hapa zaidi ya kutumia hivi viwanja vyetu viwili hapa Dar es Salaam. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Wizara ya Katiba na Sheria.

Na. 97

**Kuongezeka kwa Tatizo la Ubakaji wa Watoto Nchini**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Tatizo la ubakaji wa watoto wadogo nchini limekuwa likiongezeka siku hadi siku hasa katika Mkoa wa Iringa na kwingineko.

Je, ni kesi ngapi za ubakaji wa Watoto wadogo ziko Mahakamani hadi sasa na zimefikia hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na kwa ridhaa yako, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Ernesphar Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba tatizo la ubakaji wa Watoto wadogo limekuwa likiongezeka siku hadi siku na hasa katika Mkoa wa Iringa na kwingineko nchini. Lakini sio matukio ya ubakaji kwa watoto pekee, matukio ya ubakaji kwa ujumla yamekuwa yakiongezeka katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na takwimu za Makosa ya Ubakaji yaliyoko Mahakamani kuhusiana na ubakaji wa watoto; kwa sasa hatuna mfumo mahsusi wa kuyasajili pekee na hivyo kupata takwimu sahihi. Hii inatokana na ukweli kwamba makosa yatokanayo na ubakaji wa watoto ikiwa ni pamoja na ubakaji husajiliwa Mahakamani kama makosa mengine ya jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuyapa kipaumbele makosa haya kwenye upelelezi na katika uendeshwaji wa Mashtaka Mahakamani.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Wizara kupitia Mahakama ya Tanzania na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali lakini pia kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tunaendelea na zoezi la kufanya uchambuzi wa nchi nzima ili kuweza kupata takwimu za kesi za ubakaji zilizofunguliwa kuhusiana na watoto zinazoendelea kusikilizwa Mahakamani, zilizotolewa maamuzi lakini vilevile zoezi hili litakapokamilika tutakuwa na uwezo wa kutoa takwimu sahihi za kesi za ubakaji wa watoto nchini.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swai la nyongeza. Kwanza kabisa kabla sijauliza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, amekuwa akitupa ushirikiano mkubwa sana na ninakumbuka kwamba kuna wanawake waliokuja hapa Bungeni wakakutane naye ambao kesi zao zimechukua muda mrefu pale Iringa. Baada ya pongezi naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, Mkoa wa Iringa kesi hizi za ubakaji zimeongeka kutoka 64 zilizoripotiwa wa mwaka jana, na mwaka huu zimeripotiwa kesi 121 ambayo ni sawa sawa na asilimia 89. Kesi hizi zimekuwa zikichukua muda mrefu sana kwisha.

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuharakisha kezi hizo kwa sababu zimekuwa ni kesi ambazo kwa kweli kijinsia watoto zimekuwa zikiwaathiri hata sisi wenyewe akinamama. Tunaathirika sana kwa sababu sasa hivi huwezi kumwacha mtoto wa kike nyumbani, ukamwachia baba, ukamwachia mjomba, ukamwchia kaka kwa sababu tumekuwa tuna wasiwasi sana?

(c) Kwa kuwa Serikali imejitahidi kuweka madawati ya kijinsia katika vituo vya polisi, lakini madawati haya mengi yapo katika Miji. Je, Serikali sasa haioni huu ni wakati muafaka wa kuanzisha Madawati hayo katika vijiji na vitongoji ambako kuna vituo vya Polisi, kwa kuwa kuna ukatili mkubwa sana unaoendelea katika vijiji, lakini hawana sehemu ya kwenda kuripoti matukio haya? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ukiangalia kwa nchi nzima kwa mwaka huu kuanzia Januari mpaka Septemba, ni matukio takriban 4,511 ambayo yamefikishwa katika Mahakama zetu.

Kwa kutambua ongezeko hili, Serikali ina mkakati kupitia Mahakama ya Tanzania kuanzisha Vikao Maalum vya Mahakama pekee kwa ajili ya kusimamia masuala ya unyanyasaji wa kijinsia, lakini vilevile masuala ya ubakaji pamoja na matukio mengine ya unyanyasaji dhidi ya watoto. Kwa hiyo, tunao mpango na tunatarajia kuanzia na Mikoa ambayo vitendo hivi vimeshamiri zaidi huenda tukaanza na Mkoa wa Mara na baadaye Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la pili la madawati ya Kijinsia na kwamba tunao mkakati gani ya kuhakikisha kwamba madawati haya ya jinsi na watoto yanafikishwa katika sehemu nyingine vijijini. Kwanza kabisa ukiangalia kwa takwimu za hivi sasa madawati haya yapo kote nchini yapo takribani madawati jinsi na watoto 417. Lakini ambayo yanafanya vizuri zaidi au yapo katika vigezo ambavyo vimewekwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ni vituo takribani 8.

Nipende tu kumpongeza Mheshimiwa Ritta Kabati kwa sababu Iringa pia ni kituo chake ni moja ya kituo ambacho kimekidhi vigezo kwani ili kiweze kituo hiki kuwa na ufanisi zaidi kinatakiwa na vyumba visivyopungua nne. Lakini pia nimpongeze Ritta Kabati kwani katika Dawati hili la Iringa aliweza kutoa kompyuta na hivi sasa bado wana tatizo la *printer*. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge akipata fursa basi aweze kumalizia na *printer* huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, siyo kufungua tu vituo inajitahidi hivi sasa kuhakikisha kwamba pia inapeleka Mapolisi mbalimbali na katika mwaka huu mpango wao ni kuhakikisha wanapeleka takriban Mapolisi 8,000 ambao wataweza kuhudumia vituo hivi katika ngazi mbalimbali za Kata. (*Makofi*)

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa matukio haya ya ubakaji wa watoto wakati mwingine yanawahusisha wazazi binafsi kwa watoto wao na yamekuwa yakiripotiwa kila mara kwa wazazi kujihusisha na kuwabaka watoto wao na watoto wengi hushindwa kufika kwenye vyombo vya Sheria kwa kuwaogopa wazazi wao.

Je, pale inapothibitika kwamba wazazi wamebaka watoto wao kwa nini Serikali isiandae Sheria Mahsusi na kuwapa adhabu mara mbili wazazi hao waliojihusisha na vitendo vya kubaka watoto wao? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niseme wanaofanya vitendo hivi wana matatizo ya kisaikolojia, haiingi akilini hata siku mtu mzima na akilli zako unawezaje kumbaka mtoto.

Kwa hiyo, napenda tu kuchukua fursa hii kupitia hadhara hii kuanza kukemea vitendo vyote vinavyofanywa vya ukatili dhidi ya watoto. Lakini niseme tu Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo Kauli Mbiu ya Mwaka huu ilivyokuwa ikisema ni kwamba Funguka Tumia Mamlaka yako Zuia Ukatili wa Kijinsia na Watoto Kuboresha Afya ya Jamii.

Masuala haya kwanza yana athari kubwa sana, mengine yamekuwa yakisababisha maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, mengine yamekuwa yakisababishia watoto mimba za utotoni, lakini vilevile yamekuwa yakiwasababishia matatizo ya athari za kisaikolojia.

Sisi kama Wizara kupitia Vyombo mbalimbali vya kisheria tuombe sana ushirikiano wenu kila mmoja atumie mamlaka yaliyonayo kuhakikisha vitendo hivi havitokei.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Vitendo hivi vinatokea katika nyumba zetu, ni matukio tu takribani asilimia 4.4 yanayotokea ndiyo ambayo yamekuwa yakiripotiwa. Sasa ujiulize zile asilimia 95.6 matukio haya yanafanywa nini?

Lakini sisi kama Wizara kupitia Sheria ya Kanuni za Adhabu zipo wazi kabisa masuala haya ni ubakaji na yamekuwa yakichukuliwa hatua stahiki yanapofikishwa katika Vyombo vya Sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msabaha atamalizia Mheshimiwa Mlata.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa ruksa na mimi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa, kuna wanawake wengi wa vijijini ambao wanafanyiwa vitendo vya ukatili pamoja na watoto hao, lakini wanawake hawa wamekuwa wakikosa haki zao.

Je, Serikali na Wizara hii ina mikakati kuwasaidia wanawake wa pembezoni na wao wapatiwe haki zao wanapofanyiwa vitendo vya kikatili na vya kijinsia kama kubakwa na kunajisiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi *please, short and clear.*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kama ambavyo nimeeleza katika maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Ritta Kabati nimekuhusiana na uanzishwaji wa madawati ya kijinsia na watoto.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Lakini vilevile sisi kama Wizara tunao Mpango ambao tuna utekeleza kuhusiana na msaada wa Kisheria, na kwa kweli watoa huduma mbalimbali wa msaada wa kisheria wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana, na hivi sasa lengo letu kubwa ni kuhakikisha kwamba watu wengi wanakuwa na uelewe zaidi wa sheria na haki zao za msingi, na tumekuwa kwa kweli tukifanya kazi nzuri sana.

Huko nyuma ilikuwa kijiografia si Wilaya nyingi ambazo zimekuwa zikifikiwa na huduma hizi za msaada wa kisheria. Hivi sasa kupitia Mfumo wa *Legal Service Facility* tumetajihidi kuhakikisha kwamba tunafikia Wilaya takribani 107 na lengo letu ni ifikapo mwaka 2015 kuhakikisha kwamba tunafikia Wilaya zote na sehemu zote za pembezoni. (*Makofi*)

**MHE. MARTH M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lilitumika jina la Fataki, watoto wengi wakawa na tahadhari wanapoona dalili za Ufataki. Kwa nini hawa wabakaji wanapotuhumiwa tu tuwape jina la magubeli ili watoto wote wanaposikia gubeli anakuja wakae chonjo na watu hawa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli yamekuwepo majina mbalimbali Fataki na mengineyo, na hivi sasa ameanzisha msamiati mpya wa magubeli. Tuseme tu kwamba Waheshimiwa Wabunge, tujitahidi wote kwa jina lolote liwalo, tutumia mbinu zozote zinazowezekana kuhakikisha kwamba vitendo hivi vitokomezwa katika jamii zetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Naibu Waziri, sasa tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, swali linaulizwa na Mheshimiwa Rweikiza.

Na. 98

**Kupeleka Umeme Kata za Jimbo la Bukoba Vijijini**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Je, ule mpango wa kupeleka umeme katika Kata za Buhendangabo, Kaagya, Kishanje na Rubafu katika Tarafa ya Bugabo na Kata ya Rujugo umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE**) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kupeleka umeme katika Kata za Buhendangebo, Kaagya, Kishanje na Rubafu zilizomo katika Tarafa ya Bugambo pamoja na Kata ya Rujugo upo katika Awamu ya II ya upelekaji umeme vijijini (*REA* II).

Mradi huu unahusisha Ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 29; ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 15 na kufunga transfoma 14 na kuwaunganisha wateja wa awali wapatao 450. Mradi huu unakadiriwa kugharimu jumla ya bilioni 1.85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zabuni ya kumpata mkandarasi atakayefanya kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivyo ilitangazwa mwezi Agosti, 2013 na kufunguliwa tarehe 18 Oktoba, 2013 na mchakato wa kumpata makandarasi na utatangazwa mwisho wa mwezi huu wa Desemba, 2013.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nimeyasikia, lakini sina imani nayo. Napenda nimwulize swali moja ndogo la nyongeza.

Nitamwamini vipi kama majibu aliyotoa endapo tarehe 25 Julai, 2012 alijibu hivyo hivyo na kusema kwamba katika Awamu ya Pili ya Mradi *REA* kuna bilioni 3.2, kuna kilomita 54, kuna njia ya umeme wa kilovoti 33 na kadhalika kadhalika imeishaandaliwa na kwamba mradi huo umefanyika katika mwaka wa fedha uliopita. Tarehe iliyofuata tarehe 8 Novemba, 2012 akarudi majibu hayo hayo na leo anarudia majibu hayo hayo na hakuna kilichofanyika.

Sasa mimi na wananchi wa Kata hizi Buhendangabo, Kaagya Kishenje Rubafu na Bujugo watamwamini vipi majibu haya yanayotoa mara kwa mara ambayo hayatekelezeki?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tulitangaza kazi hizi mara ya kwanza, lakini mchakato wa upatikanaji wa wakandarasi unatumia Sheria ya Manunuzi ambayo kwa hakika vipo vigezo vingi sana vinavyosemwa na Sheria ile katika kumpata mkandarasi.

Tulifanya hivyo, na tulibahatika kupata wakandarasi katika Mikoa 14, katika Mikoa hiyo 14 Mkoa haukuwemo. Hivi sasa nichukue nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kama Serikali hii hii iliweze kutekeleza *REA* Awamu ya Kwanza ambayo Mheshimiwa Mbunge ameweka historia kubwa katika Jimbo lake kwa kuweka umeme vijiji vingi sana vyenye umeme kwa sasa katika *phase one* aendelee kutuamini haya tunayomwambia Serikali kwamba Awamu ya Pili muda wowote mwaka huu tutampata mkandarasi na ataanza kazi hiyo maana mchakato wa kumpata mkandarasi uliorudia baada ya ule wa kwanza kuwa wamekosa kumpata mkandarasi unakaribia kukamilika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jiji la Mbeya suala la umeme limekuwa ni tatizo sugu na Mheshimiwa Naibu Waziri kilio changu hiki cha muda mrefu anakielewa. Sasa nataka Mheshimiwa Naibu Waziri atoe tamko hapa hususan katika Kata za Itenzi, Mtaa wa Igombe Kaskazini, Idunda, Mwanasekwa na kadhalika. Hili jambo nataka Mheshimiwa Naibu Waziri aeleze utekelezaji wa Ilani na Mpango wa Vijiji na Mitaa hii kupatiwa umeme umefikia wapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umefikia wapi kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE**): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba tumekuwa na Programu ya umeme vijijini, hatukuweza kuwa na Programu Maalum kwa ajili ya umeme pembezoni ya Miji ambayo inatambulika kama Manispaa au Majiji. Kazi hii kwa kawaida ilipaswa ifanywe na *TANESCO*, lakini uwezo wa *TANESCO* tunaujua.

Nafikiri Mheshimiwa Mbunge kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza tumekuwa tukizungumza sana juu ya Kata za Itenzi Idunda na nyingine ambazo zipo pembezoni mwa Jiji la Mbeya na majibu yetu mara zote yamekuwa tutaona namna ya kufanya.

Nichukue nafasi hii kumhakikishia kwamba tumepata jibu la kufanya, kwa sasa tunafikiria kuzihusisha Benki kupitia *TANESCO* na baadhi ya Mabenki yamekubali kutoa mikopo kwa ajili ya kusambaza umeme pembezoni mwa Miji na kutumia fedha zile zitazolipwa na wateja kwenda moja kwa moja kulipa mikopo ile na baadhi ya Benki kama *CRDB* wameonyesha kukubaliana na Mpango ule. Ninaamini tutaweza kutekeleza maeneo ya umeme pembezoni mwa Miji mikubwa ikiwemo ya Dare s Saalam, Mwanza, Arusha na Miji mingine kwa ujumla.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Jiji la Arusha ilifungwa mitambo ya kuzalisha umeme katika eneo la Njiro *Block C* na kwa bahati mbaya sana mitambo hiyo iliitwa ya dharura na ilifungwa katikati ya makazi ya watu. Imekuwa ikileta mateso makali kwa watu wanaoishi katika eneo lile.

Sasa naomba kuiuliza Serikali ni lini mitambo ile iliyoitwa ya dharura itaondolewa maeneo yale kwa sababu hata wakazi wengine wa maeneo yale sasa wameshaanza kuhama kwa sababu ya kelele na *pollution* inayosababishwa na mitambo ile?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi, hii ni Wizara *sensitive* ina wachangiaji wengi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaona, tuone busara itasema nini? Lakini nichukue nafasi hii kuwaondoa hofu wananchi wa maeneo ya Njiro *Block C* kwamba tunalitambua tatizo hili, tutaona tufanye nini muda si mrefu.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote naomba niishukuru Serikali kwa azma ya kuvipatia vijiji 13 umeme katika Wilaya ya Kondoa kwa kukamilisha upimaji. Sasa napenda niulize.

Je, ni lini uwekaji wa nguzo na usambazaji wa nyaya za umeme utafanyika kwani wananchi wanasubiri kwa matumaini makubwa kwa ajili ya maendeleo yao? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli vijiji 13 katika Jimbo lake Mheshimiwa Mbunge vitapatiwa umeme.

Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, kwa namna anavyofuatilia kazi hii na mkandarasi nilikutajia na nimekupa mawasiliano yake. Nina imani kabisa mkandarasi huyu kwa maneno anayoyasema,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



ana kampuni inaitwa *Demi Electric* naamin unawasiliana naye, atatekeleza kazi hii. Anasema kwa sasa vifaa vinakuja, vipo bandarini. Baada ya kazi hii iliyofanyika ya kupima sasa, wataanza kazi hii mapema mwaka kesho, 2014. *(Makofi)*

Na. 99

**Utekelezaji wa REA Wilaya ya Ludewa**

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE** aliuliza:-

Wakati Wilaya nyingine nchini zina vijiji tele vinavyopelekewa umeme kupitia mpango wa *REA,* Wilaya ya Ludewa haina hata kijiji kimoja ambacho kimo kwenye Mpango wa kupatiwa umeme kupitia mpango huo.

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE**) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa inapeleka umeme katika maeneo yote nchini, yakiwemo maeneo ya Wilaya ya Ludewa. Katika kutekeleza azma hii, Serikali inatumia vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoka kwa Washirika wa Maendeleo wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ludewa haimo katika utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili chini ufadhili wa Serikali kupitia Wakala wa Nishati vijijini (*REA*). Hata hivyo Ludewa ni miongoni mwa Wilaya zilizojumuishwa katika mpango wa utekelezaji wa mradi wa umeme wa Makambako - Songea unaofadhiliwa na Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo *SIDA.*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Vijijji vinavyotarajia kupata umeme kupitia mradi huu ni pamoja na Ludewa kijijini, Muhoro, Madindo, Ludende, Milo, Luana, Mbilwa, Lugarawa, Mkongobaki, Shaurimoyo, Mudindi, Mbugani, Mavanga, Madindo, Mkiu na Mlangali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za Mradi huu zinahusisha:-

(i) Ujenzi kwa njia ya umeme Msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 61.2;

(ii) Ujenzi wa njia ya umeme Msongo kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 90; na

(iii) Kufunga *transofoma 22* na kuunganisha wateja wa awali wapatao 1300.

Mradi huu unakadiriwa kugarimu jumla ya shilingi bilioni 5.32 kwa ujumla Mradi wa Makambako Songea unahususha vijiji 117 toka Makambako hadi Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mradi huu Makambako Songea, Mradi mwingine kupitia *TANESCO* pia vinatarajia kuvipa umeme vijiji vya Nindi, Mtumbati na Lupingu vilivyomo Wilayani Ludewa. Kazi za Mradi huu zinahusisha:-

(i) Ujenzi wa njia ya umeme, Msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 27;

(ii) Ujenzi wa njia ya umeme wenye msongo wa kilovoti 0.4 wenye urefu wa kilometa 5;

(iii) Nakufunga transfoma tatu; na

(iv) Kuwaunganisha wateja awali wapatao 380.

Mradi huu unakadiriwa kugarimu jumla ya shilingi bilioni 1.2. Kazi za ujenzi za Mradi zinatazamia kuanza mwezi Januari, 2014 na kukamilika mwezi Mei, 2014. *(Makofi)*

Aidha katika mwaka huu wa fedha Miradi iliyotekelezwa na *TANESCO* ni kupeleka umeme katika vijiji vya Ludewa Kijijini, Muhoro na Luwana.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Deo Filikunjombe.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE**: Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Wananchi wa Ludewa naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri, kumshukuru sana Naibu Waziri, kuishukuru Serikali, pamoja na *TANESCO* kwa kuhakikisha wananchi wa Ludewa kijiijni wanapata umeme. Ninakuja hapa mbele ya Bunge lako tukufu kushudia kwamba kazi zinafanyika umeme sasa hivi unaenda Luana, Muhoro. Napaenda pia niishukuru sana Serikali kwa kukubali kupeleka umeme Lindi, Mtumbatu na Lupingu. *(Makofi)*

(a) Naomba nimwombe Mheshimiwa Waziri umeme ukikamilika kwenda Luana pamoja na Lupingu akubali kuja Lupingu na Luana watapowasha umeme mara ya kwanza, ili na yeye aje awashe. Wananchi wajue umeme unakwenda kule kwa jitihada za Mbunge wao mimi na Serikali.

(b) Huu umeme wa kutoka Makambako, Madaba hadi Songea. Ambao umeme wake utakwenda Mlangali, Ludende na Mundindi kazi yake nayo itakamilika lini? Mheshimiwa Waziri naomba majibu.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana kubali mwaliko na lini umeme unakwenda.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Filikunjombe, kama ifuatavyo:-

(a) Nishukuru kwa kuwambia hapa pia Mheshimiwa Mbunge anaishukuru pia Serikali kwasababu kwa kweli ni watu wachache wanaofanya hivyo.

Lakini pia nimpongeze pia kwakuwa na vijiji vyenye umeme. Alikuwa na kijiji kimoja (1) tu chenye umeme cha Ludewa Mjini, lakini sasa ana vijiji sita (6) vyenye umeme na tukiweka umeme kupitia Mradi wa Makambako Songea tutaweka pia vijiji vingine kumi na tisa (19).

Mimi naamini wananchi wa Ludewa watakubali kwamba umefanya kazi. Mimi nimekubali tutakapowasha umeme Luana na Lupingu nitakuja. *(Makofi)*

(b) Bado mradi wa Makambako Songea upo katika hatua za mwisho za kupata Wakandarasi na kulipa fidia. *(Makofi)*

**MHE. MODESTUS KILUFI**: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Mwenyekiti Wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa Wilaya ambayo ina Kata 20 lakini katika Kata 20 ni Kata nne tu ambazo angalau zimepata umeme kidogo.

Imekuwa nikiomba katika Bunge hili mara nyingi kwamba ni lini sasa Wilaya ya Mbarali nayo itapata umeme Kata ambazo zimebaki hasa zile nyingine ambazo zimepitwa na nguzo za umeme kama vijiji vya Irongo, Igalako, Uturo zote nguzo za umeme zinapita pale lakini umeme hawana. Madibira ya Mheshimiwa Rais alihaidi angepeleka umeme pale lakini hadi leo ahadi ile bado haijatimia.

Naomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie ni lini huduma hii ya umeme itapelekwa Wilayani Mbarali?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kilufi la nyongeza kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbarali ipo katika *phase two* ya Miradi ya *REA,* na nichukui nafasi hii kumhakikishia sana Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Kata ya Ilongo, Galako, Ituro na Madibira mchakato katika awamu hii ya *REA* tutajaribu kuona namna tunavyoweza tu ka-*extend* hata kwa maeneo yale ambayo yalikuwa ya mekosa na hasa yale ambayo umeme unapita juu tuone namna tutakavyo ushusha.

Tunao Mradi wa underline transfoma ambao ndio wenye majibu. Tutajaribu kuona namna gani tutaweza ku-*adjust* katika eneo lile tukaelekaza katika maeneo haya ambayo unasema yana shida kubwa na kwamba kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais na hasa Madibira.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niipongeze Serikali kwa kupeleka umeme katika vijiji vya Busheshe, Nyakayanja katika Wilaya ya Karagwe pamoja na Iyembe.

Lakini kwa masikitiko makubwa sana umeme huu umepita katika vijiji hivi hasa vitongoji vya Karee, Kamuli, Busheshe, Bwandaro, Nyakayanja, Nyaishozi, Yembe 1 na 2, lakini wananchi wa vijiji hivyo zaidi ya asilimia 95 wameshafanya *wiring* kwenye majumba yao, wanasubiri *TANESCO* iwapo umeme lakini ni karibu mwaka mzima wananchi wa vijiji hivyo hawajapata umeme na wakienda *TANESCO* wengine wameshailipia nguzo *TANESCO* wanaambiwa vifaa havipo.

Je, Serikali inatamka nini katika hili na lini itawawashia wananchi wa vijiji hivi umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Blandes, kama ifuatavyo:-

Kwanza nay eye nimshukuru kwa kushukuru maana yake mambo yanaenda vizuri. Nilipita maeneo haya na kuona namna watu walivyofurahi, lakini kazi iliyobakia hapa nikuwapatia kuwasambazia umeme.

Tunayo changamoto Shirika letu la Tanesco limeweza kufanya kazi kwa nguvu kubwa kwa sababu kwa kweli baada ya kushusha bei ya umeme wananchi wote wanamudu kuweza kulipia gharama za kuingiza umeme kwenye majumba yao. Kwa muda wa miezi kama nane tu tumeweza kuwafungia wananchi laki moja na ishirini na tano, ni idadi ambayo hajawahi kutokea tangu tumepata uhuru.

Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge tuvute subira changamoto hizo za ukosanaji wa vifaa kwa Shirika la *TANESCO* otunazifanyia kazi tupate jibu la kudumu na hapa tatizo kubwa ni fedha. Tunajitahidi sana kutafuta fedha ili tulijengee uwezo *TANESCO* iweze kuwafungia wateja ndani ya muda uliopo kisheria.

**MHE. ZAINAB M. VULLU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuuliza swali. Wananchi wanapoomba umeme uwambiwa walipie nguzo, mita na vitu vingine.

Je, kwanini baada ya kulipa hiyo mita na nguzo inakuwa mali ya Serikali haiwi mali ya mteja ambaye amelipia? Serikali inaweza ikatoa maelezo ili wananchi wajue hiyo ni haki yao au wanaitengenezea Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vullu kama ifuatavyo:-

Mimi nadhani kusema nguzo, kusema mita na vitu vingine katika kumpatia mwananchi umeme sio kwamba ananunua vile vitu, ni kwamba analipia gharama za kuipata ile huduma.

Lakini hata akilipia vitabakia anatumia yeye katika maisha yote na kwa hivyo mantiki hapa ya kusema ana miliki mimi naweza nikasema ndio ana miliki lakini pia hawezi kuzuia mtu mwingine kuchukua kutoka kwenye nguzo hiyo kwenda sehemu anayounganisha kwa madai kwamba yeye ana miliki.

Kwa hiyo mtu mwingine asijiunganishe pale mimi nadhani ili jambo ni kama majibu yote mawili kama ana miliki ama hamiliki ni sawa, kwa sababu kazi ya ile miundombinu ni kumhudumia mteja.

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tarehe 26 mwezi wa saba wakati Mheshimiwa Rais anazindua barabara ya Kigoma Rusaumba, Mheshimiwa Waziri aliwaahidi wananchi hao kufikia mwezi wa nane watakuwa wamepata umeme.

Wananchi walifurahi hata wale wananchi waliotoka kwa jirani yangu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli nao pia walifurahi ahadi imefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbassa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mbassa anajua hata hatua tuliofikia. Mimi nikuhakiikshie tu kwamba ahadi ile ni ya ukweli na wananchi watapata umeme kama tulivyokubaliana na kama tulivyopanga na kama tulivyoahidi.

**MWENYEKITI:** Wizara ya Mambo ya ndani Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Na. 100

**Kambi ya Wakimbizi Nchini**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Nchi yetu imekuwa miongoni mwa nchi zinazohifadhi Wakimbizi wanaotoka katika maeneo mbalimbali yenye migogoro.

(a) Je, kuna Kambi ngapi za Wakimbizi hapa nchini?

(b) Je, ni Wakimbizi wangapi wamebaki nchini na ni kutoka katika nchi zipi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ta Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa nchi yetu imebakiwa na Kambi/Makazi Matano ya Wakimbizi ambayo ni Kambi ya Nyarugusu iliyoko Mkoa wa Kigoma, katika Wilaya ya Kasulu, Makazi ya Ulyankulu Wilaya ya Urambo Mkoa wa Tabora, makazi ya Katumba Na Mishamo yaliyoko Wilaya ya Mlele na mpanda mkoa wa Katavi na Makazi ya Chago yalioko Wilaya ya Handeni, Mkoa wa Tanga.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Idadi ya Wakimbizi katika nchi yetu imeendeleea kupungua na hadi kufikia Oktoba, 2013 walikuwepo jumla ya Wakimbizi wapatao 102,513 kati yao Wakongo ni 64,975 Warundi ni 35,184 Wasomali ni 2,131 na kutoka nchi za Rwanda, Sudan ya Kusini, Uganda na Kenya ni 233.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MHE.FAKHARIA SHOMAR KHAMIS**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jawabu zuri alilolotoa ambayo ametoa elimu kwa Watanzania. Lakini na maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Ni sababu zipi za msingi zilizopelekea Wakimbizi waliokuwepo Tanzania wakawa hawakai kambini na wakati huo huo wakimbizi wanaokuwa katika nchi za nje wanakaa mijini?

(b) Kuna hatua gani zilizochukuliwa ili kupunguza tatizo hilo la wakimbizi hapa nchini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ta Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Kwa nini wakimbizi wanaishi Mijini kwenye Nchi nyingine na kwenye makambi hapa Tanzania. Madhumuni ya kuwaweka wakimbizi Mijini ni kutumia *Skills* walizonazo katika kuishi kufanya maisha yaende pale walipo. Pamoja na uzuri huo wa ukuwatumia wakimbizi wale katika pengine kuinua uchumi au kutoa huduma ni hatari sana kwa usalama kwa sababu huwezi kuwafuatilia wakimbizi ambao wako kwenye maeneo ya Miji wanakutana na nani, wanafanya nini na kadhalika.

Kwa hiyo, sisi Tanzania tunapendelea tuhakikishe usalama wetu kwanza, na kubwa zaidi kwa hawa wakimbizi ambao wanakuja Tanzania wengi wanakuwa na elimu ya chini yaani elimu ya kawaida. Kwa hiyo, wanaweza kutumika hata kwenye makambi katika kusomesha wenzao au shule au hospitali ambazo zipo karibu nao.

(b) Tunafanya nini katika kuhakikisha kwamba wakimbizi wanapungua. Wakimbizi ni zao la kukosekana na Utawala Bora. Kwa hiyo, jambo la kwanza ni kuhakikisha kwamba sisi na wenzetu tunakuwa na Utawala Bora na hili linafanywa sio

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



tu kwa kupitia hapa Tanzania lakini pia kupitia kwenye Taasisi za Kimataifa kama Jumuiya ya Afrika Mashariki au *SADC* tunasisitiza kwamba nchi hizi hasa majirani wawe wana usalama wa kutosha.

Tanzania yenyewe inajitoa katika kuhakikisha kwamba inasadia kwenye upatanishi katika nchi ambazo zina migogoro. Lakini hata ikilazimika kulinda usalama ili kuhakikisha kwamba nchi hizo zina utulivu na wananchi wao wanakaa huko kwao.

**MHE. MUHAMMAD I. SANYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kukuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwakuwa dunia nzima leo imesimama kidete kusimamia uharibifu wa Mazingira na kwakuwa Wakimbizi mara nyingi wanakuwa wanaharibu Mazingira kwa kiasi kikubwa mno.

Je, Serikali huwa inapata fidia ya kiasi gani kutoka katika shirika la Wakimbizi la Kimataifa *UNHCR* ili kufufua ardhi yake baada ya wakimbizi hao kurejea makwao au kuondoka katika maeneo waliyopo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ta Nchi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimia Sanya Mji Mkonge kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba maeneo mengi ambayo yana mkusanyiko mkubwa wa Wakimbizi wanaharibu Mazingira hasa katika kujitafutia kuni na wakati mwingine miti kwa ajili ya nyumba ambazo wanaishi. Kwa utaratibu wa Kimataifa ni kwamba katika mambo ambayo yanakuwa yanafanywa wakati wakimbizi bado wapo, ni kuhakikisha kwamba kuna miti inapandwa mbali na elimu ya namna ya kuhifadhi na namna ya kuiendeleza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Lakini jingine ni kwamba kabla ya Kambi yoyote ya Wakimbizi kurejeshwa kwa nchi iliyoitoa kuna utaratibu wa kuhakikisha kwa rehabilitation imefanywa ikijumuisha utengenezaji wa uharibifu wa Mazingira uliotokea wakati wakimbizi wapo pale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wetu ni mdogo sana tuendelee na swali linguine la Mheshimiwa Amina Abdallah Amour. Kwa niaba.

Na. 101

**Kuongeza Vituo Vya Uhamiaji Nchini**

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR** aliuliza:-

Uingiaji holela wa Wakimbiza nchini unaweza ukadhibitiwa kwa kuongeza Vituo vya Uhamiaji:-

(a) Je, vituo vingapi vya Uhamiaji vimeongezwa kuanzia 2010 2013?

(b) Je, Vituo vipo sehemu gani?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uingiaji wa Wakimbizi nchini linasimamimiwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakimbizi Sura 37 ya Mwaka 2002. Kwa mujibu wa Sheria hiyo mwomba hifadhi ya Ukimbizi anapaswa kupitia kwenye kituo cha kuingilia pale panakuwa na huduma hiyo.

Hata hivyo ikiwa hakuna kituo hicho mwomba hifadhi hulazimika kuingia nchini kupitia kituo/eneo lolote kuwa siyo rahisi kwake kupitia kwenye vituo rasmi wakati akiwa anakimbia maafa yatokanayo na machafuko ya kisiasa, mapigano ya kikabila, vita au njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo mafupi naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo.

(a) Katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2013 Vituo vya Uhamiaji vipya (vya kuingilia nchini ) Vinne (4) vimeongezwa.

(b) Vituo hivyo Vinne (4) ni Namtumbo (Wilaya ya Namtumbo Mkoani Ruvuma ), Uwanja wa Ndege wa kimataifa Songwe (Mkoani Mbeya) Mtambaswala (Mkoani Mtwara) na Mkenda (Nakawale, Muhukuru Wilaya ya Songea Mkoani Ruvuma).

**MHE. THUWAYBA IDRIS MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti Ahsante sana. Kwa kuwa sababu zinazowafanya wakimbizi kuingia nchini ni vita, siasa za kiuchumi.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwapa haki watu hawa yaani hawa wakimbizi?

Swali la pili kutokana na majibu yako msingi umesema kwamba kumeongozwa vituo vinne lakini bado wimbi la uhamiaji linaongozeka na hata kupelekea matatizo kwa Maafisa wa Uhamiaji wakati wanapowakamata hawa wahamiaji kutokana na lugha ambazo hawafahamiani.

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]
Utaona kwamba wahamiaji wanajua lugha zao kama Kisomali au Kiethiopia na wakati huo huo Watanzania ambao Maafisa wetu hawajui lugha hizo za Kisomali wala Kiethiopia isipokuwa wanajua Kiingereza.

Lakini wale wengine Kiingereza hawajui. Sasa utawasaidiaje Maafisa maafisa hawa ili wapate mafunzo waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi wanapokutana na hawa wakimbizi? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kwamba dhamana au dhima ya nchi yoyote ile ambayo ni mdau kwenye *convention* ya Umoja wa Kimataifa ya Vienna ni kuhakikisha kwamba mtu yoyote mwenye shida ya ukimbizi kwa sababu yoyote ile anahitaji kwanza apokelewe, apewe hifadhi ya mwanzo ili asikilizwe tatizo lake.

Baada ya hapo kuna utaratibu wa kuchambua kwamba ile sababu yake inatosha na tunaiamini. Ikiwa inatosha basi tunampa *status* ya ukimbizi na kama haitoshi pengine anataka tu kuhama na hasa wanaohama kwa ajili ya uchumi basi mara nyingi huwa hawakubaliwi mpaka watumie njia nyingine ya kawaida ya kutoka nchi nyingine na kwenda nyingine.

Kuhusu vituo, vituo vilivyoongezwa ni vinne na tatizo hasa alisema hapa ni lugha. Ni kweli ni vigumu sana kuwafanya Maafisa Uhamiaji wajue na lugha zote za dunia.

Lakini kwa kiasi kikubwa pale ambapo wanakutana na wageni basi wanatumia lugha ya Kiingereza au Kiswahili na ikishindikana basi miongoni mwao wapo ambao wana lugha za Kifaransa na lugha za Kitaliano ambazo zinaweza zikawa ni rahisi wao kusaidiana. Ikindikana basi wana haki ya kutafuta *interpreter* ambaye anaweza kusaidia. Hata hivyo katika Chuo chetu tunawapa mafunzo ikiwemo mafunzo ya lugha mara kwa mara.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Na. 102

**Watoto Uenye Ulemavu wa Ngozi**
**Katika Shule za Serikali**

**MHE. REBECCA M. MNGODO** aliuliza:-

Mojawapo ya malengo ya Milenia ni elimu kutolewa kwa wote.

Je, watoto wangapi wenye ulemavu wa ngozi wanasoma katika Shule za Serikali hapa nchini?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza malengo ya milenia ya kutoa elimu kwa watoto wote wakiwemo wenye ulemavu wa ngozi, Serikali imefanya uhamasishaji mkubwa kwa jamii kupeleka watoto wenye ulemavu wa ngozi Shuleni. Hivyo wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi wanaosoma Shule za Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari hadi mwaka 2012 walikuwa ni jumla ya wanafunzi 2,212. Wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi wanaosoma katika Shule za Serikali za Elimu ya Awali ni 142 wakiwemo wavulana 72 na wasichana 70 na wanafunzi wanaosoma katika shule za Msingi za Serikali wenye ulemavu wa ngozi ni 1,337 wakiwemo wavulana 680 na wasichana 657. Aidha, kwa upande wa Shule za Sekondari za Serikali kuna jumla ya wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi 393. Wakiwemo wavulana 211 na wasichana 182.

Mnamo mwezi Novemba mwaka 2013 Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *Under The Same Sun (UTSS)* imezindua mwongozo wa utoaji wa huduma za kielimu kwa watoto wenye ulemavu wa ngozi na uoni hafifu ili kuhakikisha huduma bora za kielimu zinatolewa kwa walengwa hao.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa wapo watoto wenye ulemavu wa ngozi ambao hufichwa na wazazi wao na hivyo kukosa ile nafasi ya kufaidika na kupata elimu.

Je, Serikali imeweka njia zipi kudhibiti tabia hiyo ya kuwaficha watoto wenye ulemavu wa ngozi?

Lakini swali la pili mojawapo ya changamoto kubwa kwa watoto wenye ulemavu wa ngozi siyo kuuawa na kunyanyaliwa katika jamii inayowazunguka lakini pia ni ule mtazamo uliopo kwamba hawana uwezo wa kutosha kusoma na kucheza kama watoto wengine. Serikali imekuja na kuanzisha kitabu hiki cha kielelezo kwa ajili ya kutoa huduma ya elimu.

Je, kuna maandalizi gani ambayo yemewekwa ili watoto wengi wenye ulemavu wa ngozi waweze kufaidika kama vile kuwa na walimu wa kutosha na pia kuwa na kitabu chenyewe kuwa na *font* au herufi kubwa kuna maandalizi gani ambayo yamewekwa ili watoto wengi zaidi waweze kufaidika hasa watoto wenye ulemavu wa ngozi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza mikakati ya kuwafichua watoto hawa. Serikali juhudi inayofanya hivi sasa ni kuwahamasisha wananchi na kuwaelimisha ili jamii mzima itambue umuhimu wa kuwalea vijana wetu hawa.

Kwa hivyo, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Viongozi kwa ujumla na wananchi wote kuhakikisha kwamba wanaisaidia Serikali katika juhudi yake ya kuwapeleka watoto hawa wote shuleni kama ambavyo inaonekana hivi sasa kazi imefanya nzuri iendelee hivyo hivyo mpaka kila mtoto mwenye ulemavu iwe wa ngozi, uhafifu wa kuona au ulemavu mwingine aweze kuwa shuleni.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Swali la pili kuhusu kunyanyapaliwa pia tunatumia elimu kwa wananchi ili jambo hili liondokane. Lakini kuwasaidia vijana hawa Serikali imefanya juhudi kubwa ya kuandaa visaidizi vya kuwawezesha vijana hawa waweze kusoma vizuri, ikiwemo kuwapa miwani.

Lakini pia tumechapisha vitabu vyenye maandishi makubwa na machapisho mengine ambayo wanapewa katika maandishi makubwa ili yawasaidie wao kuweza kusoma vizuri na kila aina ya vifaa ambavyo vinatakiwa kwao na walemavu wa aina nyingine tunajitahidi kuongeza bajeti kwa ajili ya kuwahudumia vizuri vijana hawa wapate mafanikio. La kisera, tuna Sera ya kuwajumuisha vijana walemavu na vijana wasiokuwa walemavu katika shule moja hatuweki shule maalum kwa ajili ya walemavu tu na zingine wasiokuwa walemavu.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Waheshimiwa muda wetu umekwisha. Wizara ya Uchukuzi Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar.

Na. 103

**Malipo ya harama za Bandari Kulipiwa Benki**

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR** aliuliza:-

Vyombo vya bahari vinavyobeba abiria na bidhaa huondoka Zanzibar usiku na kufika Dar es Salaam saa kumi na mbili asubuhi kutokana na utaratibu mpya wa kulipia gharama za bandari benki, abiria hao hulazimika kusubiri mpaka saa tatu wakati benki zinafunguliwa ili kulipia bidhaa zao.

(a) Je, Serikali haioni kuwa abiria na wafanyabiashara wanapata usumbufu mkubwa kutokana na utaratibu huu mpya?

(b) Je, ni kwa nini benki zisifunguliwe saa moja ili kutoa huduma kwa abiria hao na kuwaondolea usumbufu?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kuomba kujibu swali la Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa abiria na wafanya biashara kutoka Zanzibar wanapata usumbufu kutokana na utaratibu mpya wa kulipia gharama za bandari benki badala ya utaratibu wa zamani wa kulipia katika Ofisi za Bandari ambapo hulazimika kusubiri kuanzia saa 12 asubuhi wanapowasili Dar es Salaam hadi saa 3 asubuhi benki zinapofunguliwa ndipo waweze kulipia bidhaa zao.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kulitambua hilo Serikali iko katika mchakato wa kuzifanya benki zote zinatoa huduma kwa wateja wa bandari zianze kufanya kazi kwa masaa 24 siku zote saba za wiki. Mchakato huu unatarajiwa kuwa umekamilika na mabenki husika kuanza kufanya kazi kwa masaa 24 ifikapo mwezi Januari, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio ya Wizara yangu kuwa benki hizo kufanya kazi kwa masaa 24 kutaongeza ubora wa huduma kwa abiria, wafanya biashara na wateja wote kwa ujumla na hivyo kuondoa usumbufu na kuongeza ufanisi katika bandari ya Dar es Salaam.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa jibu lake zuri ambalo linatia moyo. Nina swali moja la ziada. Kuna mashine moja tu ya upekuzi kwa binadamu na mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam kwa wale abiria ambao wanakwenda Zanzibar.

Kutokana na kwamba mashine hii ni moja kuna watu wengi wanajipanga mpaka wanakaribia mlangoni pale nje. Kwa hivyo, namtaka Mheshimiwa Waziri anieleze lini atachukua ya kuongeza mashine nyingine ili suala hili limalizike kwa haraka? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa sasa iko moja tu ya upekuzi wa mizigo na binadamu katika bandari ambayo wasafiri kutoka Zanzibar wanatumia na hii ni ile *walk through* yaani ambayo mtu unapita pale unaangaliwa kama unavyo vyuma au nini.

Lakini tumekwisha elekeza na labda nitumie nafasi hii kusema tu kwamba jambo hili linafanyiwa kazi na litatekelezwa mara kwamba badala ya kutumia ile *walk through* peke yake moja ile wachukue hivi vitu vya mkononi *hand metal detectors* ili kurahisisha kupekua abiria baldala ya kutegemea mashine moja ile. *(Makofi)*

Na. 104

**Usajili na Utaratibu wa NGO's Nchini**

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

(a) Je, Tanzania kama nchi imesajili *NGOs* ngapi hadi sasa?

(b) Je, kuna utaratibu gani wa kuzisimamia *NGOs* hizo?

(c) Je, kwa kiasi gani *NGOs* hizo zimesaidia kuongeza pato na ajira nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

[NAIBU WAZIRI WA MAENDDELEO YA JAMII, NA WATOTO]

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya mwaka 2002 Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, imesajili jumla ya *NGOs* 5,992 hadi Januari, 2013.

Kati ya hizo *NGOs* 5,179 zimepatiwa cheti cha usajili na *NGOs 813* ambazo zilisajiliwa kabla ya Sheria mpya na au zimesajiliwa chini ya Sheria nyingine zimepatiwa cheti cha ukubalifu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya *NGOs* kama ilivyorekebishwa mwaka 2005 kifungu 29 Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwuliza swali asome kifungu 29 badala ya kifungu 19 kinayataka mashirika yaliyosajiliwa chini ya Sheria hii kila mwaka kuwasilisha Serikalini taarifa za kazi na taarifa ya fedha iliyokaguliwa na Mkaguzi anayetambulika kisheria. Kupitia zoezi hili Serikali imeweza kutambua utendaji kazi wa mashirika haya na kutoa ushauri kulingana na mahitaji husika ya jamii na pia kuziwajibisha pale zinapoonekana kwenda kinyume na malengo ya usajili wao. Aidha, Serikali imeweza kuanzishwa kwa Bodi ya Taifa ya uratibu wa *NGOs* yenye mamlaka ya kukagua shughuli za *NGOs* nchini.

(c) Mhehismiwa Mwenyekiti, yasiyo ya kiserikali yamekuwa ni wadau na nguzo muhimu katika maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi, masharika haya yanajihusisha na shughuli mbalimbali za kukuza uchumi na kupunguza umaskini miongoni mwa jamii kama vile kuhudumia watoto walio katika mazingira hatarishi, masuala ya afya, *VVU* na ukimwi, Kilimo na Utawala Bora na Haki za Binadamu. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa kuwa yako malalamiko ya wananchi wa Kitanzania walio wengi kuwa zipo *NGO* za mifukoni ambazo zinapata fedha na mali nyingi kutoka kwa wafadhili mbalimbali duniani ambazo fedha hizo huzitumia kujinufaisha kwa viongozi hao binafsi.

Lakini hivi karibuni zimeonekana *NGO* nyingi badala ya kufanya kazi zilizosajiliwa kwake zinafanya siasa badala ya kutumiza ule wajibu unaotakiwa. Je, Serikali imechukua hatua gani kudhibiti viongozi hao na pia ni NGO zipi zimewajibishwa kwa kukiuka malengo ya kusajiliwa kwao?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli kuna baadhi ya *NGOs* ambazo matumizi yao ya fedha hayaendani na masuala ambayo wameombea.

Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Wizara imeshachukua hatua katika baadhi ya *NGOs* ikiwemo kuzifutia usajili, lakini kwa mfano tuna *NGOs* ambazo zinasema zinataka kufanya kazi ya kuhudumia watoto yatima lakini hazifanyi. Kwa hiyo, kuna *NGO* kwa mfano, Mlinzi wanachukua fedha halafu hawapo, tulishawafuta na tumefutia cheti cha usajili. Lakini *NGO* kwa mfano Mtandao wa *NGO* Mkuranga ambapo wameshindwa kupatana na tumeweza pia kufuta usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ambalo ameuliza Mheshimiwa Mbunge ni muhimu sana. Tunaona kweli siku hizi baadhi ya *NGOs* badala ya kufanya kazi za kuanzishwa kwao zinajihusisha na masuala ya kisiasa. Nitumie Bunge lako Tukufu kuzitaka *NGO* hizi kwamba wafanye kazi kwa mujibu wa Katiba zao. *NGO* haziruhusiwi kufanya siasa. Lakini zinaruhusiwa kufanya ushawishi, Utetezi na elimu kuhusu masuala ya Utawala Bora.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo Baraza la Taifa la *NGOs* litafanyakazi kazi zake na niombe Waheshimiwa Wabunge kutoa taarifa Wizarani pale ambapo mnaona *NGOs* zinajihusisha na siasa badala ya kufanya kazi zao. Lakini la pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya tumeteua sasa hivi Maafisa wa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ndiyo Wasajili Wasaidizi wa *NGOs.* Wale ndiyo wanajua *NGO* hii imefanya kazi gani, haijafanya kazi gani.

Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge mtusaidie sana kutuletea taarifa, sisi tutachukua hatua ya kuzifutia usajili bila kusita. Hatutakubali Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge muda wetu umekwenda sana na niruhusu Wajumbe kama 11 kuchangia Wizara ya Nishati kutokana na umuhimu wa Wizara ile. Kwa hiyo, mniwie radhi itabidi tumalize. Maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha. Sasa natanagaza wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 10 wa Mhehismiwa Aggrey Mwanri, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wapo kwa ajili ya kushiriki Mkutano wa Shirika lisilo la Kiserikali la *TANFED* hapa Dodoma. Kati hao watatu wanatoka nchini Zimbabwe. Wapo? Wameshatoka.

Wageni 12 wa Mheshimiwa Modestus Kilufi, kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo. Karibuni. Wageni 12 wa Mheshimiwa Charles Tizeba, Mbunge, Naibu Waziri wa Uchukuzi na Wakuu wa Shule za Sekondari kutoka Sengerema. Karibuni sana Dodoma.

Mgeni wa Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Mbunge kutoka Jimboni kwake ambaye ni Ndugu Moshi Bundala. Karibu na wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo Bungeni. Bi. Mary Kigosi, ameambatana na watoto wake, ambao ni Mourini Owen, Mwandumbya, Ndugu Lightness Mlongwa na Ndugu Gofrey Elias Sanya, kutoka hapa hapa Dodoma. Karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Tangazo Kikao cha Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Mohamed Missanga, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Uchumi, Viwanda na Biashara anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuwa leo tarehe 13 Desemba, 2013 saa saba (7.00) mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo ya Viwanda na Biashara. Kikao hicho kitafanyika katika Ukumbi wa Msekwa B.

*[MWENYEKITI]*

Mheshimiwa Habib Juma Mnyaa, Mkufunzi wa Mazoezi ya Viungo wa *Bunge Sports Club*, anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa Kikundi cha Mazoezi ya Viungo kuwa, wanatakiwa Uwanja wa Jamhuri kesho Jumamosi saa 12 asubuhi.

Pamoja na mazoezi, kutakuwa na kikao kitachohusu safari ya kwenda Zanzibar kwenye *Sports Bonanza,* ikiwa ni Maadhimisho ya Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar, wakiwa na ndugu zao wa Kitambi Noma.

Mheshimiwa Saidi Mtanda, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Maendeleo ya Jamii, anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuwa, leo tarehe 13 Desemba, 2013, saa saba mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi wa *Basement;* nyote mnaombwa kuhudhuria.

Mheshimiwa Mwambalaswa, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge wa Nishati ya Madini, anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuwa, leo tarehe 13 Desemba, 2013, saa tano asubuhi, mara baada ya kipindi cha maswali kwisha, kutakuwa na kikao. Nafikiri itabidi mkutane saa saba, sidhani kama mmepata kibali, kama mmepata kibali cha Spika, mtakutana saa tano asubuhi.

Mheshimiwa Anna Abdallah, Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara, anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara wote kuwa kesho tarehe 14 Desemba, 2013, kutakuwa na Semina Dodoma Hoteli, kuanzia saa tatu asubuhi, itakayoendeshwa na Shirikisho la *AMREF.*

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa za Kamati za Bunge za Huduma za Jamii na Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Mapendekezo na Maoni yaliyomo katika Taarifa hizo

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Sitta!

**MHE. MARGARET S. SITTA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, naomba kuwasilisha Taarifa kuhusu utekelezaji wa kazi za Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kwa Mwezi Machi hadi Disemba, 2013, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha taarifa ya shughuli za Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Ninachukua pia nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, kwa ushirikiano wao ambao umewezesha kupatikana kwa Taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Mezani pamoja na muhtasari ninaosoma, viingie kwenye *Hansard.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kuhusu majukumu ya Kamati, Wajumbe wa Kamati, shughuli zilizopangwa na kutekelezwa na Kamati, Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na changamoto zinazozikabili Wizara hizo, zinapatikana katika ukurasa wa kwanza hadi wa nane wa Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa

moja kwa upande wa Moani na Ushauri wa Kamati kuhusu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliamua kuanza na Mpango wa Matokeo Makubwa sasa katika Sekta ya Elimu Nchini. Sekta ya Elimu ni nguzo mama ya sekta nyingine zote ikiwemo Uchumi, Afya, Kilimo, Sheria na kadhalika. Elimu ndiyo njia pekee inayowezesha nchi kujenga rasilimali watu ili waweze kupambana na adui umaskini, ujinga na maradhi na hatimaye kujenga nchi yenye uchumi bora. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa katika Sekta ya Elimu. Imani ya Kamati ni kwamba, Mpango huu ukitekelezwa ipasavyo na kupewa kipaumbele cha ELIMU KWANZA, Dira ya Elimu itafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza Mpango huu kwa ufanisi, Kamati inapendekeza maeneo yafuatayo kupewa msisitizo na Serikali. Kwanza kabisa ni kuongeza bajeti kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Pia kuboresha Vyuo vya Ualimu Nchini ili kuwe na mazingira stahiki ya utoaji wa mafunzo ya elimu kwa walimu. Aidha, ufundishaji wa stadi tatu muhimu, yaani za KKK (Kusoma, Kuandika na Kuhesabu), uzingatiwe ipasavyo, hatua ambayo tunaamini itasaidia wanafunzi kudumu masomo na kujenga msingi imara katika Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufundishaji katika Vyuo vya Ualimu uzingatie:-

- Uhodari katika masomo *(Subject Competence),* pamoja na njia za kufundishia;

- Kuongeza kiwango cha sifa za kujiunga na mafunzo ya ualimu, ili kusajili wanafunzi waliofaulu kujiunga katika mafunzo ya ualimu, ikiwemo kubuni mbinu ya kupata wanafunzi wenye kuipenda kazi ya ualimu siyo wanaojiunga na kozi ya ualimu kwa sababu wamekosa kozi nyingine.

- Kutoa umuhimu kwa mafunzo kwa vitendo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



(*practical*) kama ilivyokuwa zamani kwa kutenga fedha za kutosha kutekeleza suala hilo;

- Kuongeza walimu wa elimu maalumu pamoja na kuandaliwa ipasavyo;

- Kuwezesha mafunzo kazini kwa walimu ili kuwa na mafunzo kazini endelevu na kutolewa kwa kupitia mpango ulioandaliwa maalumu wa mafunzo kazini kama ilivyokuwa enzi za MTUU;

- Kuboresha mfumo wa kuhudumia walimu kwa kuwa na chombo kimoja cha kuhudumia walimu;

- Kutoa posho ya mazingira magumu kwa walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu;

- Kuboresha Elimu ya Watu Wazima;

- Kuongeza mafunzo ya *VETA* ili kuwezesha wahitimu wengi zaidi kupata stadi za ufundi ili waweze kujiajiri na kuajiriwa; na

- Kuimarisha Idara ya Ukaguzi wa Elimu kwa kuiwezesha kuwa Wakala unaojitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kuhusu majukumu ya Kamati hii yameainishwa katika Kanuni ya 118 ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 6(6) na Kifungu cha 7(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ambayo ni kusimamia shughuli za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kama ifuatavyo:-

(i) Kushughulikia bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati;

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge chini ya Wizara hizo;

(iii) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo;

(iv) Kufuatilia utendaji wa Mashirika ya Umma yanayosimamiwa na Wizara; na

(v) Kufuatilia Utekelezaji wa shughuli unaofanywa na Wizara husika kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii walioteuliwa katika Kipindi cha Pili cha Bunge la Kumi kwa mujibu wa Kanuni ya 116 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2013, na kwa pamoja wakanichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii ni pamoja na:-

Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Zabein Mhaji Mhita, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mheshimiwa Faki Haji Makame, Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mheshimiwa Riziki Omari Juma, Mheshimiwa Ezekia Dibogo Wenje, Mheshimiwa Antony Gervase Mbassa, Mheshimiwa Ali Juma, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Mch. Dkt. Getrude Pagalile Rwakatare, Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari, Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, Mheshimiwa Mohamed Gulam Dewji, Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mheshimiwa Hasnain Mohamed Murji, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso na Mheshimiwa Abdulaziz Mohamed Aboud.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake Kikanuni, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, iliandaa Mpango Kazi wa Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2012/2013, ulioainisha shughuli mbalimbali zinazotarajiwa kutekelezwa na Kamati. Shughuli hizo ni pamoja na kupitia na kujadili Bajeti za Wizara zilizo chini ya Kamati kwa Mwaka 2013/2014; kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara husika kwa mwaka 2012/2013; na

kufuatilia utendaji kazi wa Wizara husika pamoja na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Aprili hadi Disemba, 2013, Kamati ilifanya shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Kujadili Bajeti za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka 2013/2014, pamoja na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara hizo kwa kipindi cha mwaka 2012/2013;

(ii) Kupata semina na mafunzo mbalimbali kuhusu utendaji kazi wa Taasisi za Wizara husika;

(iii) Kufuatilia utendaji kazi wa Wizara zinazosimamiwa na Kamati pamoja na Taasisi zake;

(iv) Kujadili Azimio la Bunge la Kuridhia Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru Kujitegemea Kiutendaji;

(v) Kushiriki katika kujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Namba Tatu) wa Mwaka 2013, ambao moja ya sehemu yake ilikuwa na maudhui ya kuanzisha Mfuko wa Elimu; na

(vi) Kufanya vikao mbalimbali na wadau katika kupata taarifa za kiutendaji za Taasisi za Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2013/2014: Katika kutekeleza jukumu hili, kwa upande wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Kamati ilipitisha jumla ya shilingi 689,681,055,428.00 kwa Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hali kadhalika, kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Kamati ilifanikiwa kupitisha jumla ya Sh. 753,856,475,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Aidha, Kamati ilitoa maoni yake kuhusu Bajeti za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



2013/2014 katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata semina mbalimbali zifuatazo: Rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo ambayo inapendekeza mabadiliko katika Sera ya Elimu ya Mwaka 1977; huduma ya maji safi na vyoo shuleni; Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now*) katika Sekta ya Elimu nchini; Watu wenye Ulemavu wa Ngozi; na uzazi salama na uzazi wa mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilishiriki kujadili na kutoa maoni yake katika Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Namba 3) wa Mwaka 2013, ambao moja ya sehemu yake ilikuwa na maudhui ya kuanzisha Mfuko wa Elimu, pamoja masharti ya utoaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara katika Taasisi mbalimbali za Wizara inazozisimamia, kufuatilia utekelezaji wa majukumu yao.

(a) Ziara katika Taasisi za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

(i) Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania;

(ii) Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo; na

(iii) Mradi wa Taasisi ya Moyo Muhimbili.

(b) Ziara katika Taasisi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

(i) Tawi la Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Zanzibar;

(ii) Chuo cha Sayansi za Bahari Zanzibar;

(iii) Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima;

(iv) Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru, Arusha; na

(v) Mamlaka ya Elimu ya Ufundi *(VETA),* Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya vikao na Taasisi za Wizara kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Upangaji wa madaraja na alama za ufaulu katika Mitihani ya Elimu ya Sekondari.

(ii) Matokeo ya Kidato cha Nne ya Mwaka 2012.

(iii) Utekelezaji wa shughuli za Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE).*

(iv) Taarifa ya Robo Mwaka ya Usambazaji wa Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi kutoka *MSD.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zifuatazo zilibainika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi:-

(i) Baraza la Mitihani Tanzania (*NECTA)* kutohusishwa katika upangaji wa madaraja na alama za ufaulu katika Mitihani ya Elimu ya Sekondari;

(ii) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara kujumuisha Fedha za Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu;

(iii) Mfumo wa kuhudumia walimu unaohusisha Vyombo zaidi ya kimoja na hivyo kusababisha urasimu katika upatikanaji wa haki za walimu nchini;

(iv) Mfumo unaotumika kupata na kuajiri Wahadhiri katika Vyuo Vikuu vya Serikali nchini;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



(v) Uwezo mdogo wa kiutendaji wa Idara ya Ukaguzi wa Elimu nchini;

(vi) Matumizi ya Lugha ya kufundishia na kujifunzia nchini yanayoainishwa na Sera ya Elimu;

(vii) Ongezeko la Uhitaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini;

(viii) Kasi ndogo ya ujenzi wa Chuo Kimoja cha *VETA* kwa kila Wilaya; na

(ix) Upungufu katika Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Mafunzo ya Ufundi *(NACTE)* na Sheria ya Mamlaka ya Elimu ya Ufundi Stadi *(VETA*) katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zifuatazo zilibainika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii:-

(i) Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kama sehemu ya Bajeti ya Sekta ya Afya nchini kutokidhi uhitaji wa Azimio la Abuja la Mwaka 2001 la kutenga asilimia 15 ya bajeti ya Serikali kwa ajili ya Sekta ya Afya;

(ii) Sehemu kubwa takribani asilimia 90 ya Miradi ya Maendeleo ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hutegemea fedha za wahisani;

(iii) Kasi ndogo ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) 2007 - 2017;

(iv) Upungufu wa Watumishi katika Sekta ya Afya hususan katika maeneo ya vijijini;

(v) Upatikanaji wa huduma ya afya ya mama na mtoto (uzazi salama), ikiwemo matumizi ya huduma ya uzazi wa mpango nchini;

(vi) Uwepo wa Deni la Serikali kwa Bohari Kuu ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Dawa *(MSD)* la shilingi 52 bilioni (Machi, 2013) ambalo linaathiri upatikanaji wa dawa nchini;

(vii) Uhitaji wa huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa Wananchi wote (*Universal Coverage*);

(viii) Gharama kubwa ya kufanya ukaguzi (*Service)* katika mitambo, mashine na vifaa mbalimbali vya kisasa vinavyotumika kutoa huduma mbalimbali za afya;

(ix) Uendelevu wa Miradi mbalimbali muhimu ya utoaji huduma za afya nchini, baada ya wafadhili kumaliza muda wa kuhudumia Miradi hiyo;

(x) Uhitaji wa teknolojia za kisasa za kielektroniki katika kukusanya mapato ya ndani yatokanayo na utoaji wa huduma za afya katika hospitali na taasisi mbalimbali za afya nchini;

(xi) Uzinduzi wa Baraza la Utendaji la Taifa la Watu Wenye Ulemavu ili kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu 2010; na

(xii) Upungufu katika Sheria ya Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TFDA)* na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu *(NIMR)* katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Elimu ni nguzo mama ya Sekta nyingine zote zikiwemo Uchumi, Afya, Kilimo, Sheria na kadhalika. Elimu ndiyo njia pekee inayowezesha nchi kujenga rasilimali watu ili waweze kupambana na adui umaskini, ujinga na maradhi na hatimaye kujenga nchi yenye uchumi bora. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa katika Sekta ya Elimu. Ni imani ya Kamati kwamba, Mpango huu ukitekelezwa ipasavyo na kupewa kipaumbele cha ELIMU KWANZA**,** dira ya elimu itafanikiwa**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza Mpango huu

kwa ufanisi, Kamati inapendekeza maeneo yafuatayo kupewa msisitizo na Serikali:-

- Kuongeza bajeti kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

- Kuboresha Vyuo vya Ualimu nchini ili kuwa na mazingira stahiki ya utoaji mafunzo ya elimu kwa walimu. Aidha, ufundishaji wa stadi tatu muhimu za KKK (Kusoma, Kuandika na Kuhesabu) uzingatiwe, hatua itakayosaidia wanafunzi kumudu masomo.

- Ufundishaji katika Vyuo vya Ualimu uzingatie uhodari katika masomo (*Subject Competence*) pamoja na njia za kufundishia.

- Kuongeza kiwango cha sifa za kujiunga na mafunzo ya ualimu ili kusajili wanafunzi waliofaulu kujiunga katika mafunzo ya ualimu, ikiwemo kubuni mbinu za kupata wanafunzi wenye kuipenda kazi ya ualimu.

- Kutoa umuhimu kwa mafunzo kwa vitendo (*practical*) kama ilivyokuwa zamani kwa kutenga fedha za kutosha kutekeleza suala hilo.

- Kuongeza walimu wa elimu maalumu pamoja na kuandaliwa ipasavyo.

- Kuwezesha mafunzo kazini kwa walimu kuwa endelevu na kutolewa kwa kupitia Mpango Maalumu wa Mafunzo Kazini.

- Kuboresha mfumo wa kuhudumia walimu kwa kuwa na chombo kimoja cha kuhudumia walimu.

- Kutoa posho ya mazingira magumu kwa walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu.

- Kuboresha Elimu ya Watu Wazima.

- Kuongeza mafunzo ya *VETA* kuwezesha wahitimu wengi kupata stadi za ufundi ili kujiajiri na kuajiriwa.

- Kuimarisha Idara ya Ukaguzi wa Elimu kwa kuiwezesha kuwa Wakala unaojitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kujadili Taarifa ya Wizara kuhusu Mfumo wa Upangaji wa Madaraja ya Utunuku na Alama za Ufaulu uliotangazwa na Serikali hivi karibuni, ilibaini kwamba Baraza la Mitihani Tanzania *(NECTA)*, halikushiriki katika utekelezaji wa jukumu hili. Hivyo, Kamati inashauri kwamba, Baraza la Mitihani Tanzania lenye jukumu kisheria la kusimamia Sera ya Mitihani lishiriki kikamilifu katika suala hili; na mfumo wa zamani wa kupanga madaraja ya utunuku na alama za ufaulu uendelee kutumika mpaka mfumo mpya unaopendekezwa na Serikali utakapokamilika katika hatua zake zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida (*Recurrent Budget*), imekuwa ikijumuisha fedha za Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini. Pamoja na takwimu kuonesha kiasi kikubwa cha fedha hutengwa kwa Wizara hii, sehemu kubwa ya fedha hizo hutumika kwa ajili ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na kubakisha kiasi kidogo kutumika kwa Wizara kutekeleza majukumu yake. Hali hii inasababisha utekelezaji hafifu wa baadhi ya shughuli nyingine za Wizara ikiwemo kuhudumia Vyuo Vikuu vya Serikali na taasisi zingine za Wizara. Kamati inapendekeza kwamba, Serikali itenganishe Bajeti ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba, bajeti inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi haitolewi kwa wakati kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Sayansi za Bahari Zanzibar ulioanza tangu mwaka 2002 mpaka sasa haujakamilika. Aidha, fedha nyingi kiasi cha takribani shilingi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



bilioni sita zimetumika kuweka jamvi lililokaa kwa muda mrefu hadi nondo zake kushika kutu kutokana na ukosefu wa fedha takribani shilingi bilioni moja zilizoidhinishwa katika mwaka 2012/13 kutotolewa, mradi kuzorota. Kamati inashauri fedha zilizoidhinishwa kiasi cha shilingi bilioni moja zipelekwe mara moja kukamilisha jengo husika ili lianze kutumika. Vilevile Serikali inapojipanga kutekeleza Miradi mikubwa, ianze kwa kujenga jengo moja na kulikamilisha, badala ya kutumia fedha nyingi kutandaza jamvi kubwa, hali inayoleta upotevu wa rasilimali fedha.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Tawi la Chuo cha Mwalimu Nyerere Bububu – Zanzibar, Kamati ilisikitishwa na ujenzi wa Jengo la Utawala la Chuo lililojengwa chini ya kiwango. Kamati iliielekeza Serikali kurekebisha upungufu uliopo mapema iwezekanavyo na kuwasilisha taarifa ya marekebisho hayo mapema kwa Kamati ili ipate fursa ya kuhakiki marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilisikitishwa kupata taarifa ya ufunguzi rasmi wa jengo hilo muda mfupi baadaye bila kushiriki katika kuhakiki ili kujiridhisha na marekebisho yaliyofanyika. Kamati inashauri jengo husika lifanyiwe marekebisho ya hali ya juu na pia mkandarasi alietekeleza Mradi huu na wasimamizi wake wakiwemo wahandisi kutoka Serikalini, wawajibishwe kutokana na ujenzi uliofanyika chini ya kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kusimamia viwango vya elimu inayotolewa nchini sambamba na ongezeko la taasisi mbalimbali za utoaji elimu, Kamati inasisitiza kwamba, Serikali iiwezeshe Idara ya Ukaguzi wa Elimu nchini kuwa Wakala unaojitegemea ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, Kamati imebaini kwamba, lugha ya kufundishia na kujifunzia inaleta changamoto kubwa katika suala zima la utoaji elimu nchini. Hali hii inasababisha wanafunzi kukariri masomo kwa lengo la kujibu maswali ya mitihani kuliko kujenga uwezo wa mwanafunzi kimaarifa. Kamati

inapendekeza kwamba, Serikali ichukue hatua madhubuti kupata ufumbuzi wa suala hili muhimu, ili kuwa na Taifa lililoelimika na lenye maarifa kukabiliana na mazingira yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mrefu sasa walimu wamekuwa wakihudumiwa na vyombo zaidi ya kimoja, hali inayosababisha adha nyingi ikiwemo urasimu katika kupanda madaraja, kujiendeleza kimasomo, utekelezaji wa malipo ya haki zao mbalimbali kama mishahara na fedha za likizo. Kamati inashauri kwamba, Serikali iangalie upya mfumo wa kuhudumia walimu haraka iwezekanavyo kuwezeshwa kuwa na chombo kimoja ili kukabiliana na adha zinazowakabili walimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa za Serikali kulipa madeni ya Walimu nchini kwa kutenga shilingi bilioni 52 (Mwaka 2009 - 2012), imeonekana bado kuna idadi ya walimu takribani 502 (2012/2013), waajiriwa wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ambao madai yao yalikataliwa kutokana na kutokidhi vigezo vya malipo. Kamati inashauri taarifa za madai ambayo yamekataliwa kutokana na kutokidhi vigezo vya ulipaji ziwafikie wahusika mapema iwezekanavyo ili waweze kukidhi vigezo vinavyohitajika na walipwe haki zao. Serikali iwe na mpango endelevu wa kulipa madai ya walimu kadiri yanavyojitokeza ili kuondokana na tatizo la mlundikano wa madai ya walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umuhimu wa kuhakikisha maeneo ya pembezoni yanakuwa na walimu. Imejidhihirisha kwamba, upungufu wa walimu hasa katika maeneo ya pembezoni au vijijini unasababishwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa mazingira magumu katika kutekeleza majukumu ya walimu. Katika kukabiliana na suala hili Kamati inashauri Serikali ikamilishe mapema iwezekanavyo, mchakato wa kutoa posho ya mazingira magumu kwa walimu wanaofanya kazi katika mazingira hayo ili kuwafanya wabaki katika mazingira hayo na kuipenda taaluma yao. Zamani posho hiyo ilikuwepo wala siyo mpya. Serikali iainishe maana ya dhana “mazingira magumu” ili kuwezesha mchakakato mzima wa utoaji posho

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



ya mazingira magumu. Vilevile Serikali itoe ufafanuzi wa matumizi ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge katika bajeti ya mwaka 2012/13 kwa ajili ya posho ya mazingira magumu kwa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya Serikali ya kujenga Chuo kimoja cha *VETA* katika kila Wilaya, Kamati inashauri hatua hiyo ya Serikali ipewe nguvu ya kutosha kibajeti ili kuongeza idadi ya Vyuo hivyo nchini. Hatua hii itawawezesha idadi kubwa ya wahitimu wa elimu ya msingi na sekondari ambao hawakubahatika kuendelea na masomo kupata stadi za ufundi ili kuweza kujiajiri na kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*National Council for Technical Education – NACTE),* lina jukumu la msingi la kusimamia utoaji wa mafunzo ya elimu ya ufundi nchini. Imebainika kwamba, kuna idadi kubwa ya vyuo vinatoa mafunzo ya elimu ya ufundi bila kukamilisha vigezo vilivyoainishwa na *NACTE* kupata Ithibati ya kutoa mafunzo husika. Kamati inashauri Sheria ya *NACTE* ifanyiwe maboresho ili kuipa taasisi hii uwezo wa kuvichukulia hatua ya kuvifungia vyuo ambavyo vinatoa mafunzo hayo bila kupata ithibati kutoka *NACTE;* na *NACTE* itoe taarifa kwa umma kuhusu vyuo ambavyo vinatoa mafunzo bila kupata ithibati ya utoaji mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba, utaratibu unaotumika kutoa mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu haukidhi mahitaji ya wanafunzi waliotoka katika familia zenye kipato duni. Kamati inashauri Serikali iboreshe mfumo wa kupata wahitaji wa mikopo *(Means Testing)* ili kuweza kujumuisha watoto wanaotoka katika familia zenye vipato duni. Aidha, juhudi za makusudi zitumike kuongeza makusanyo ya mikopo iliyokwishatolewa tangu mwaka 1991, kwani kiasi cha takribani shilingi bilioni 8.8 (Februari, 2013) zilizokusanywa kati ya matarajio ya makusanyo ya shilingi bilioni 18 kwa mwaka 2012/2013 ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Marekebisho ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Sheria mbalimbali (Namba 3) ya Mwaka 2013: Kamati ilipata fursa ya kuwasilisha maoni yake kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu marekebisho ya Sheria zifuatazo:-

- Sheria ya Mfuko wa Elimu (*The Education Fund Act*) *Cap 412:* Katika kifungu cha marekebisho ya Sheria hii kinaeleza kwamba, vyanzo vya fedha vya Mfuko wa Elimu viwe sawa na vile vya *VETA.* Tafsiri yake ni kwamba, hakuna vyanzo vipya endelevu vya mapato vinavyopendekeza kuhudumia Mfuko wa Elimu. Kamati inasisitiza kwamba, juhudi za makusudi zichukuliwe mapema iwezekanavyo kuwezesha Mfuko huu uwe na vyanzo endelevu vya fedha.

Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu *(The Higher Education Student's Loans Board Act) Cap 178:-*

(a) Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ibainishe lengo mahususi la utungwaji wa Sheria hii ambayo ni kuwawezesha wanafunzi ambao wazazi wao hawana uwezo wa kugharamia mafunzo ya elimu ya juu kupata mkopo kwa ajili ya mafunzo hayo.

(b) Sheria ioneshe wazi mgawanyo wa matumizi ya asilimia 64 za fedha zinazopelekwa katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa walengwa. Aidha, Kati ya asilimia 64 za fedha za Mfuko wa Elimu zinazopendekezwa kupelekwa katika Bodi ya Mikopo kwa ajili ya kutoa mikopo husika, kiasi kisichopungua asilimia 60 ya fedha hizo (64%), zitumike kuhudumia wanafunzi ambao wazazi wao hawana uwezo wa kugharamia mafunzo ya elimu ya juu, bila kujali aina ya masomo mwanafunzi anayosomea.

(c) Sheria itoe tafsiri ya mwanafunzi mhitaji ambaye wazazi wake hawana uwezo wa kugharamia masomo ya elimu ya juu.

(d) Kifungu cha Sheria kifanyiwe maboresho kumtaka mwajiri atoe taarifa za waajiriwa wake, ambao ni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



wadaiwa wa Mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, kwenye Bodi ya Mikopo ili kufanikisha zoezi la urejeshwaji wa mikopo hiyo. Aidha, kuwepo na ukomo wa muda unaomtaka mwajiri kutoa taarifa za mwajiriwa kwenye Bodi ya Mikopo, bila kujali jukumu la Bodi la kutafuta wadaiwa wa mikopo.

(e) Ili kuwezesha urejeshwaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, kigezo cha ulipaji wa mkopo kwa mnufaika wa mkopo kitumike na Mamlaka ya Uhamiaji katika kutoa Hati za Kusafiri.

(f) Mhitimu wa mafunzo ya elimu ya juu ambaye ni mnufaika wa mkopo, apewe Taarifa ya Mkopo wake *(Loan Statement),* wakati wa kuhitimu ili kujua deni analotakiwa kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu unaotumika kuajiri Wahadhiri katika Vyuo Vikuu vya Serikali wa kutumia Sekretarieti ya Ajira umesababisha upungufu mkubwa wa Wahadhiri katika Vyuo Vikuu vya Serikali nchini. Kamati inashauri kwamba, suala la kuajiri Wahadhiri katika Vyuo Vikuu vya Serikali litekelezwe na Vyuo Vikuu chini ya uratibu wa Serikali. Aidha, utaratibu uliokuwa unatumika wa kuwaandaa wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo yao kuwa Wahadhiri urejeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeridhia Azimio la Abuja la Mwaka 2001 linaloelekeza kila Nchi Mwanachama wa Umoja wa Afrika *(African Union*), kutenga asilimia 15 ya Bajeti ya Serikali katika Sekta ya Afya ifikapo mwaka 2015. Takwimu zinaonesha kwamba, bajeti zinazotengwa katika Sekta ya Afya nchini hazikidhi Mkataba wa Azimio husika. Kamati inashauri kwamba, Serikali ijizatiti katika kuongeza vyanzo zaidi vya mapato ya ndani ili kuweza kutenga asilimia 15 ya bajeti yake katika Sekta ya Afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu unaonesha kwamba, Bajeti ya Wizara katika shughuli za maendeleo hutegemea kwa kiasi kikubwa fedha za wahisani. Kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



mwaka 2013/2014, jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni shilingi 471,282,941,000.00, ambapo fedha kutoka vyanzo vya ndani vya Serikali ni shilingi 36,100,000.00 na fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo wanaosaidia Sekta ya Afya ni shilingi 435,182,941,000.00, sawa na asilimia 92**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, inajidhihirisha kwamba, wahisani kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakipunguza na wengine kujitoa katika kufadhili Miradi mbalimbali ya Maendeleo nchini. Kamati inashauri kwamba, Serikali itenge fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo kutoka fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba, teknolojia ya kisasa ya kielektroniki ikitumika kukusanya maduhuli ya Serikali, huongeza ufanisi katika kutekeleza jukumu hilo kama ilivyothibitika katika Hospitali ya Rufaa ya Mbeya na Hospitali ya Taifa Muhimbili. Hivyo, Kamati inashauri kwamba, Serikali ichukue juhudi za makusudi, kutumia Mfumo wa Kisasa wa Kielektroniki kukusanya maduhuli katika Wizara na Taasisi zake zikiwemo Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania *(TFDA),* Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali *(Chief Government Chemist)* na Taasisi ya Mifupa *(MOI)* ili kupunguza mianya ya upotevu wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) 2007 – 2017, Serikali imedhamiria kuboresha huduma ya afya vijijini na kusogeza huduma za afya hususan tiba na kinga, karibu na Wananchi. Katika kufanikisha lengo la Mpango huu, Kamati inashauri Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa MMAM kwa kuwezesha upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba nchini. Kasi hii iende sambamba na kuboresha miundombinu, kupata Wataalamu na Watumishi wengine wa Afya katika ngazi zote ili kutoa huduma za afya kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Spika, afya ya mama na mtoto ni kigezo kikuu cha ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za utoaji wa

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



huduma ya afya nchini. Hali kadhalika, upatikanaji wa huduma za uzazi wa mpango ni nyenzo muhimu katika kuimarisha afya ya mama na mtoto. Ili kufikia ahadi ya Rais kuhusu upatikanaji wa huduma za Uzazi wa Mpango kwa asilimia 60 ya wanawake walio katika umri wa kupata mtoto nchini ifikapo mwaka 2015, Kamati inashauri ifuatavyo:-

- Serikali itenge fedha za kuwezesha kufikia angalau asilimia 20 ya mahitaji ya huduma ya Uzazi wa Mpango kwa sasa.

- Halmashauri nazo zitenge fedha kuwezesha upatikanaji wa huduma ya uzazi wa mpango katika maeneo yao.

- Serikali pia iwezeshe upatikanaji wa vifaa vya kujifungulia akina mama wanaokwenda kujifungua.

- Serikali pia iendelee kuhamasisha matumizi bora ya huduma ya uzazi wa mpango hususan katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu wa upatikanji wa dawa katika hospitali na vituo vya afya nchini. Baada ya Kamati kubaini changamoto katika suala zima la upungufu wa dawa katika hospitali na vituo vya afya nchini, ikiwemo Hospitali za Wilaya na mojawapo tuliyoitembelea ya Bagamoyo, inashauri ifuatavyo:-

- Serikali itumie Mfumo wa kielektroniki wa kutunza kumbukumbu za mtiririko wa utoaji wa huduma za afya kwa wagonjwa ili kudhibiti upungufu na matumizi mabaya ya dawa hospitalini. Halikadhalika, vituo vya afya nchini viandae taarifa za kuona wagonjwa wa kituo husika.

- Mfumo wa usimamizi wa uendeshaji wa shughuli za utoaji wa shudhuli za afya nchini uimarishwe. Aidha, Serikali izijengee uwezo Kamati za Usimamizi ngazi ya Mkoa mpaka Wilayani kudhibiti matumizi mabaya dawa na vifaa tiba. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



- Serikali ihimize Wananchi kujiunga na Mifuko ya Afya ya Jamii nchini *(CHF)* na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* ili kupata huduma stahiki za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bohari Kuu ya Dawa *(Medical Stores Department),* ina jukumu la kununua, kuhifadhi na kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika Hospitali na Vituo vya Afya vya Serikali nchini. Katika kuboresha utendaji kazi wa *MSD,* Kamati inashauri ifuatavyo:-

- Serikali iharakishe zoezi la kufanyia maboresho ya kimfumo na kiutendaji ya Taasisi ya *MSD* ili kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma hiyo muhimu.

- Fedha ya bajeti ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, zitolewe na Hazina kwa mkupuo mmoja ili kumaliza tatizo la urasimu katika ununuzi na usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi nchini.

- Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha hadi leo hii Serikali haijalipa deni la *MSD* lipatalo shilingi bilioni 52 hadi kufikia mwezi Machi, 2013; ni muhimu Serikali ilipe deni lake, ili kuiwezesha Taasisi hii kutekeleza majukumu yake kiufanisi na hata kuiwezesha Serikali kuipima kiuwezo *MSD.*

- Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri nazo zipewe ratiba ya muda wa kuwasilisha mahitaji ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi *MSD* mapema iwezekanavyo ili kutoa muda wa kutosha kwa *MSD* kufanya ununuzi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imedhihirika kwamba, Taasisi za Serikali zikiwemo Mamlaka ya Chakula, Dawa na Vipodozi *(TFDA),* Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali *(Government Chemistry),* Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu *(NIMR),* Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili *(MUHAS)*, Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa *(MOI)* na nyinginezo, hutumia fedha nyingi kugharamia utaalamu kutoka nje ya nchi, kufanya matengenezo ya mitambo,

mashine na vifaa mbalimbali katika kila mwaka wa fedha. Kamati inashauri ifuatavyo:-

- Serikali itekeleze Mpango Maalum wa Kuandaa Wataalam wa Teknolojia za Kisasa watakaotoa huduma hiyo muhimu katika Taasisi za Serikali nchini. Hatua hii itapunguza gharama kubwa kwa Serikali kwa kila taasisi na kwa kila mwaka wa fedha kutekeleza jukumu hilo.

- Serikali iboreshe mazingira ya utendaji kazi ya wataalamu wa kufanyia matengenezo vifaa waliopo ili wadumu katika fani zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii asilimia 80 ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi zitolewazo na *MSD* huagizwa kutoka nje ya nchi. Kamati inashauri kwamba ni vyema Serikali kufanya mapitio ya Sera ya Viwanda vya ndani ili kuvipa uwezo ikiwemo kutengeneza mazingira rafiki yanayovutia uwekezaji na ukuaji wa viwanda hivyo. Hatua hii itaviwezesha viwanda hivyo kutengeneza dawa, vifaa tiba na vitendanishi vinavyotumia teknolojia nyepesi kwa kuzingatia ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa huduma za Bima ya Afya kwa Wananchi wote *(Universal Coverage*) ni muhimu sana. Imedhihirika kwamba, umekuwepo uhitaji mkubwa wa huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* katika kuwezesha upatikanaji wa huduma ya afya kwa Wananchi wote. Ili kutekeleza suala hili muhimu, Kamati inapendekeza kwamba, Serikali iandae Mpango Maalum utakaowezesha upatikanaji wa huduma za Bima ya Afya kwa Wananchi wote ikiwemo wasio na kipato kuweza kupata huduma za afya nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia upatikanaji wa Watumishi katika Sekta ya Afya ni tatizo kubwa na ni changamoto kwa Wizara ya Afya na katika uotoaji wa huduma ya afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi leo kuna Zahanati na

*[MHE. M. S. SITTA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII]*

Vituo vya Afya ambavyo vimekamili na havina Watumishi. Ili kukabiliana na changamoto hii ya ufungufu wa Watumishi katika Sekta ya Afya katika maeneo ya vijijini au pembezoni, Kamati inapendekeza ifuatavyo:-

- Serikali iweke utaratibu maalumu wa kuhakikisha wahitimu wa mafunzo katika Sekta ya Afya wanaosomeshwa na Serikali watumike kutoa huduma za afya katika maeneo ya pembezoni kwanza kwa muda maalumu kabla hawajaenda katika maeneo mazuri yenye nafuu.

- Serikali iweke motisha maalum kuwezesha watumishi wanaofanya kazi katika maeneo ya pembezoni kubaki katika utumishi huo.

- Aidha Serikali ifanye utaratibu wa kuajiri Watumishi katika Sekta ya Afya kwa kuwapata wanaotoka katika maeneo ya pembezoni na kuwaendeleza kimafunzo, kama mkakati mmojawapo wa kupata Watumishi watakaoweza kufanya kazi katika maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ustawi wa Jamii ni ya maana sana na ni muhimu sana katika jamii na inapaswa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kamati inashauri ifuatavyo:-

- Kwanza kabisa Idara ya Ustawi wa Jamii iliyoko ndani ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, iongezewe fedha katika Bajeti ya Idara ili itekeleze majumu yake kwa ufanisi. Kwa kuwa utolewaji huduma kwa watu wenye ulemavu ni Sekta mtambuka, Kamati inapendekeza kuwa ni vyema pengine Serikali ikaona umuhimu wa kuihamisha Idara ya Ustawi wa Jamii, itoke kule iliko na iende katika Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kuamini kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu, ina mamlaka ya kutoa maelekezo kwa Wizara zote kutoa huduma kulingana na utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo. Hatua hii itawezesha ufanisi katika upatikanaji wa huduma kama afya, elimu, ulinzi, miundombinu, sheria na nyinginezo kwa kundi hili muhimu.

Pia Serikali iharakishe uundwaji wa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu litakalosimamia utekelezaji wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya Mwaka 2010. Suala hili limesharudiwa, tunaamini sasa karibu litafikia mwisho wake. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa, ukarabati wa miundombinu ya Vituo vya Ustawi wa Jamii ikiwemo Makazi ya Wazee nchini, Vituo vya Watoto Yatima, Walemavu na Mahabusu ya Watoto utekelezwe mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kutoa huduma stahiki kwa Kundi la Watu wenye Ulemavu wa Ngozi. Kamati inashauri ifuatavyo:-

- Kuziwezesha Hospitali za Wilaya kutoa huduma za awali za matibabu ya saratani nchini ili kuwasaidia wale ambao hawana uwezo kusafiri hadi Dar es Salaam kupata huduma hiyo.

- Kukiwezesha Kiwanda cha ndani kinachotengeneza mafuta ya kujikinga na mionzi ya jua *(sun skin creams)* kwa watu wenye ulemavu wa ngozi, yaani kiwezeshwe hicho kiwanda kufanya kazi yake ipasavyo. Aidha, huduma hii Serikali iangalie uwezekano wa kutoa bure kwa walengwa. *(Makofi)*

- Pia kutengeneza mazingira rafiki ya elimu kwa watu wenye ulemavu wa ngozi, ikiwemo kuwezesha upatikanji wa kifaa cha kukuza maandishi *(monoculus),* kuongezewa muda wa kufanya mtihani, mwalimu kutumia ubao mweusi, mwanafunzi kukaa nafasi ya mbele na kadhalika, yale ambayo yatawawezesha wanafunzi wa aina hiyo kuendelea na masomo vizuri ipasavyo.

- Serikali iharakishe kusikiliza kesi zinazohusu mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi. Hali kadhalika, kutekeleza adhabu kali kwa watu wanaopatikana na makosa ya mauaji ya ukataji wa viungo.

- Serikali pia, iendelee kutoa elimu kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Wananchi kuhusu fikra potofu zinazochochea mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha upatikanaji wa matibabu ya figo na saratani nchini, Hospitali za Rufaa za Kanda ziwezeshwe kivifaa na wataalamu kutoa huduma za msingi za matibabu haya na Hospitali za Wilaya zijengewe uwezo kutoa huduma za awali za matibabu husika. Hatua hii ni muhimu katika kusogeza huduma karibu na Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipaka ya nchi yetu hususan katika mpaka wa Tunduma, Mkoani Mbeya, udhibiti wa chakula, dawa na vipodozi katika mipaka hiyo umekabiliwa na changamoto nyingi na hivyo kufanya zoezi hilo kuhitaji juhudi kubwa za Serikali kukabiliana nao. Kamati inashauri kwamba:-

- Serikali ifanye makubaliano ili kupata *harmonization* ya sheria kuhusu matumizi bora ya chakula, dawa na vipodozi na nchi jirani za Afrika ya Mashariki na za Kusini mwa nchi yetu (*SADC).* Makubaliano hayo yawe katika kutumia Sheria ya Pamoja katika kutekeleza jukumu hilo. Hatua hii itawezesha udhibiti wa chakula, dawa na vipodozi visivyo na kiwango kuingizwa nchini.

- Sheria ya *TFDA* ifanyiwe marekebisho ili kuipa uwezo Taasisi hii kufikisha watuhumiwa katika Vyombo vya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza jukukumu la kufanya tafiti za magonjwa ya binadamu inayotekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu *(NIMR)* nchini, Kamati inasisitiza:-

- Sheria inayosimamia utekelezaji wa tafiti iongezewe uwezo kudhibiti matumizi mabaya ya tafiti.

- Serikali iwe na maandalizi kamili ya kuhudumia Miradi mbalimbali ambayo wafadhili wake wakimaliza muda wa kuhudumia wataondoka. Aidha, iweke mikakati ya

matumizi bora ya wataalamu na vifaa vya Miradi husika. Mfano, Mradi wa Udhibiti wa Malaria Korogwe, wafadhili wanamaliza muda wao mwezi Desemba, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ni afya, hivyo, Kamati inaamini Serikali ikichukua hatua za makusudi katika kutekeleza Maoni na Ushauri wa Kamati, huduma za afya zitaboreka kwa kiwango fulani nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa fursa hii muhimu ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi cha Aprili, 2013 mpaka Desemba, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuwashukuru Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi - Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Dkt. Seif Rashid na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi - Mheshimiwa Philipo Mulugo, kwa kuipatia Kamati ushirikiano mzuri wakati wote wa kutekeleza majukumu yake. Vilevile nawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii pamoja na Watendaji wote wa Wizara hizo, kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa shukrani za dhati, kwanza, kwa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, kwa ushirikiano wao wa dhati ambao wanaendelea kuutoa na kuwezesha kufanya kazi hii vizuri sana. Aidha, ninaishukuru Ofisi ya Bunge inayoongzwa na Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas D. Kashililah, kwa msaada mkubwa walioipatia Kamati wakati wote wa kutekeleza majukumu yake. Hali kadhalika, ninamshukuru Katibu wa Kamati - Ndugu Stella Mlambo, kwa kuihudumia vyema Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. RIZIKI OMARI JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Said Mtanda!

**MHE. SAID M. MTANDA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu shughuli zake kwa kipindi cha Machi, 2012 hadi Desemba, 2013 kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, yameainishwa katika Fasili ya Nne ya Kifungu cha (6), pamoja na Fasili ya Kwanza ya Kifungu cha (7), Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la Aprili, 2013. Majukumu haya ni kusimamia Wizara tatu ambazo ni Wizara ya Kazi na Ajira, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya majukumu haya ya kusimamia Wizara, Kamati pia ina majukumu mengine manne yaliyoainishwa kwenye Kifungu cha 2(a) cha Fasili ya Saba ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo Aprili, 2013. Majukumu hayo ni:-

(i) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia;

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

(iii) Kushughulikia Taarifa za kila mwaka za utendaji wa Wizara hizo; na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (b) ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati hii waliteuliwa Mwezi Machi, 2013 kwa mujibu wa Kanuni ya 116 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013. Wakati wa uteuzi, uliteua jumla ya Wajumbe 22. Naomba kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama - Mwenyekiti, Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Capt. John Damian Komba, Mheshimiwa Salvatory Naluyaga Machemli, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Mohamed Said Mohamed, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, Mheshimiwa Joshua Nassari, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde na Mheshimiwa Juma Othman Ali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa dhati kwa jinsi ulivyozingatia vigezo muhimu vilivyoainishwa katika Fasili ya Tano ya Kanuni ya 116 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013. Kwa namna hiyo, Kamati imeweza kuwa na Wajumbe wenye taaluma, uzoefu na sifa nyingine muhimu kwa utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kazi zilizotekelezwa. Katika kipindi hicho, Kamati ilisimamia Wizara tatu zilizo chini yake, shughuli zilizofanyika katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii ni:-

Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara. Katika kutekeleza jukumu la Kamati kuchambua

Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara zilizo chini yake, Kamati ilitekeleza jukumu hili kwenye Mkutano wa Kumi na Moja. Maoni yaliwasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

Katika Mwaka 2013, Kamati ilipitia na kuchambua Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Akiba wa *GEPF* wa Mafao ya Wastaafu wa Mwaka 2013 *(The GEPF Retirement Benefit Fund) Act*. Maoni kuhusu Sheria hii yaliwasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Mwaka 2013, Kamati ilishiriki semina moja iliyoandaliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Semina hiyo ilihusu namna bora ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa Wanawake wenye kipato kidogo, kuongeza ajira na kuwaimarisha kiuchumi wanawake kwa njia ya mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka 2013, Wajumbe walipata fursa ya kujifunza mambo mbalimbali yanayohusu Sekta ya Hifadhi ya Jamii ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya ziara hizi ilikuwa kujifunza masuala yanayohusu Hifadhi ya Jamii kutoka nchi husika hususan mafao mbalimbali yanayotolewa, hatua wanazochukua kupanua wigo wa Wanachama na aina ya uwekezaji wanaoufanya. Pia kutumia uzoefu wa nchi hizo kuendeleza maboresho ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii katika nchi yetu. Katika ziara hiyo, Wajumbe walijifunza masuala mbalimbali kama ifuatavyo:-

- Michango ya Wanachama kuwasilishwa siku kumi na tano baada ya mwezi ambapo kila mwajiri anayechelewa kupeleka mafao ya Mwanachama anatozwa adhabu ya asilimia mbili ya makusanyo.

- Umuhimu wa kupanua sekta ya hifadhi ya jamii na kuwafikia watu wote walio katika sekta isiyo rasmi. Fao la kujitoa *(Withdrawal),* ambalo limekuwa mjadala mkubwa katika Bunge hili katika vipindi mbalimbali, pia nalo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

tulipata nafasi ya kujifunza. Katika nchi ambazo Kamati ilitembelea, *withdrawal* siyo kitu ambacho kinakubalika kimsingi.

- Uwekezaji katika miundombinu ni sehemu ambayo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaweza kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

- Umuhimu wa kuwa na Mfuko wa kuhudumia Wafanyakazi wanaoumia kazini *(Workmen's Compensation Fund),* Mfuko ambao utachangiwa na Wanachama wenyewe na utajiendesha wenyewe, nalo ni sehemu ya mambo muhimu tuliyofunza sehemu tulizotembelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa jamii yetu, Kamati ina ushauri ufuataо:-

- Mageuzi makubwa katika Sekta ya Hifadhi ya Jamii yanahitaji utayari wa muda mrefu na pia utashi mkubwa wa kisiasa, uwekezaji mkubwa wa kiteknolojia, kwa kuwa hifadhi ya jamii inahusisha sekta nyingi sana.

- Mahitaji makubwa ya rasilimali kwa upande wa Bajeti ya Serikali kwa kuzingatia uwepo wa makundi yasiyojiweza ikiwemo Wazee na wasiojiweza.

- Ili kupata mafanikio katika Sekta hii katika kupanua wigo na kufikia Sekta Isiyo Rasmi ni muhimu Serikali kuweka vivutio ikiwemo ruzuku kwa Wanachama waliojiunga na Mifuko mbalimbali. Uzoefu huu unapatikana katika nchi ya China, ambapo Serikali wanatoa ruzuku kwa watu ambao wamejiunga katika Mifuko hii mbalimbali ili kuwamotisha.

- Kwa kuzingatia umuhimu wa teknolojia na mawasiliano, Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii ni vizuri kuwepo na *Recording Center* moja ili kuimarisha upatikanaji wa taarifa za Mwanachama kwa njia rahisi na kwa wakati.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara zilizo chini ya Kamati, Kamati ilibaini mambo mbalimbali kama yanavyofafanuliwa katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Kamati ilikutana na Shirika la Taifa la Utangazaji *(TBC)* kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka 2011/2012 na Malengo ya Mwaka 2012/2013. Vilevile Kamati ilitembelea Vituo vya TBC kujionea hali halisi ya utendaji kazi wa Shirika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwa Shirika la Utangazaji la Taifa limefanikiwa kujenga vituo tisa vya redio *FM* pamoja na Mradi wa kuboresha Studio ya Mikocheni kuwa ya dijiti. Aidha, Shirika limefanikiwa kupata shilingi bilioni sita kwa ajili ya kupanua na kukuza usikivu wa Radio na Televiseni. Kwa hiyo, tunaamini sasa mnato na mgando wa picha utatoweka sasa katika *TBC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, Shirika la Utangazaji Tanzania bado linakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- Kushindwa kulipia huduma ya kukodi mitambo ya *satellite segment* kwa kuwa Shirika linadaiwa na watoa huduma mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kwa kiasi cha takribani shilingi bilioni mbili nukta moja. Kutokana na hali hiyo, mapato ya Shirika yamekuwa yakishuka siku hadi siku kwa sababu *TBC* inashindwa kujiendesha vizuri na hivyo kushindwa kuandaa vipindi vingi bira vinavyovutia wafanyabiashara kupeleka matangazo yao.

- Baadhi ya Wizara, Taasisi, Wakala na Idara za Serikali zimekuwa zikihudumiwa na *TBC* kwa kurushiwa vipindi vyao kwenye Redio na Televisheni bila kulipia huduma hiyo na hivyo kuwa wadaiwa sugu.

- Kutotekelezwa kwa Mkataba wa utendaji

wa Mradi wa Dijiti ambapo Serikali haijatoa udhamini wa mkopo unaotolewa na *China Development Bank.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizi, Kamati inaushauri kuwa Serikali itambue umuhimu wa Shirika la Utangazaji Tanzania kwa kulitengea Fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Fedha za maendeleo zitolewe kwa muda mwafaka ili kurahisisha utekelezaji wa Miradi mbalimbali ambayo *TBC* inaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Filamu Tanzania ilianzishwa kwa lengo la kusimamia na kuhakikisha maadili ya Kitanzania yanazingatiwa katika filamu zetu. Pia kuratibu masuala ya utengenezaji, uoneshaji wa filamu, utengenezaji wa nyumba na maeneo ya sinema, michezo ya kuigiza, weledi na viwango stahili vya usanii na vibali vya utengenezaji wa tasnia ya filamu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua mchango mkubwa unaotolewa na Bodi hii pamoja na changamoto mbalimbali ambazo wanakabiliana nazo. Mfano, Bodi imefanikiwa kukuza tasnia ya filamu nchini na kutoa elimu kwa umma, kusimamia tuzo mbalimbali za filamu ndani na nje ya nchi, kusimamia vibali vya utengenezaji wa filamu na kufanya ukaguzi wa filamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya, Bodi inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

Kwanza, mmomonyoko wa maadili. Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana na Kamati kwamba, hivi sasa katika baadhi ya filamu utaona maadili ya Kitanzania hayazingatiwi kwa kiasi kikubwa. Kutozingatia Sheria kwa wadau wa filamu, ufinyu wa bajeti na vitendea kazi vya Bodi, kuwepo na vibanda maktaba, ambavyo havijasajiliwa kihalali kutokana na ukosefu wa Sheria Ndogo katika Halmashauri zetu za Wilaya na uelewa mdogo kwa baadhi ya Wajumbe au Viongozi wa Bodi za Wilaya ni changamoto kubwa ambayo inaikabili Bodi ya Filamu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizo, Kamati inashauri kuwa:-

(i) Bodi ya ukaguzi wa filamu iongezewe fedha kwa ajili ya kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

(ii) Serikali iweke mkakati wa kudhibiti nyimbo za wasanii katika vifaa vya mawasiliano mfano simu za mikononi ili wasanii wetu wanufaike na kazi zao. Tunaishukuru na kuipongeza Serikali kwa kuwa baadhi ya wasanii sasa wameanza kupata malipo yao kutokana na nyimbo zao kutumika kama miito ya simu. Kwa hiyo, tunaishukuru na kuipongeza Serikali, iendelee na kazi hiyo.

(iii) Wizara ifanye udhibiti wa matangazo ambayo hayana maadili ya Kitanzania yanayotolewa katika vyombo vya habari.

(iv) Wizara iweke mikakati madhubuti ya kupambana na kudhibiti mitandao ya uharamia wa kazi za wasanii, ikiwa ni pamoja na kudhibiti utengenezaji wa stika bandia zinazotumika kwenye kanda za filamu na muziki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajira kwa vijana linaweza kupunguzwa kwa kiasi fulani kupitia Sekta ya Michezo kwa Vijana. Michezo ni Sekta inayoweza kuondoa wimbi la umaskini kwa vijana hata wale ambao hawakupata elimu ya kutosha. Michezo ni Sekta inayoweza kutangaza nchi yetu na kusaidia kukuza Sekta nyingine kama vile Utalii. Kwa fursa hii pia tunawapongeza Vijana wa *Kilimanjaro Stars,* kwa hatua ambayo waliifikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuweka mkazo na kuhakikisha michezo inafanyika kuanzia ngazi ya Shule za Msingi na pia kujenga Shule za Michezo *(Sports Academy)* ili kupata vipaji vyao wakiwa bado wadogo. Aidha, viwanja vyote ambavyo vipo wazi katika maeneo ya shule na maeneo mengine ya miji, vitumike kwa matumizi ya michezo. Hivyo, Wizara inapaswa kutekeleza

majukumu hayo kama yalivyokusudiwa na kuweka mikakati ya kuwaongezea ujuzi Wataalamu wetu wa Michezo ndani na nje ya nchi ili kukuza soko la ajira kwa njia ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la Muswada wa Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari linatokana na Sera ya Habari ya Mwaka 2003, kutokana na mabadiliko mbalimbali ya sayansi na teknolojia na masuala ya utandawazi kwa ujumla ambapo Sheria iliyopo haikidhi mahitaji hususan Sheria ya Magazeti ambayo ilitungwa mwaka 1976.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko haya ya teknolojia ya kisasa, Kamati inaamini kuwa, Serikali itachukua hatua za haraka za kuleta Muswada huu ili kutunga Sheria yenye manufaa kwa Watanzania na kupunguza changamoto zinazoikabili tasnia ya habari na vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana Tanzania ulianzishwa kwa lengo la kutoa mikopo midogo midogo yenye gharama nafuu itakayowawezesha vijana kujiajiri wenyewe. Suala la kuwawezesha vijana kujiajiri kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ni changamoto kubwa inalolikabili Taifa kwa sasa na hii ni kutokana na ukweli kwamba, Vijana ndiyo kundi kubwa katika jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua juhudi za Serikali na inaipongeza kwa hatua iliyofikia kwa kuwaendeleza vijana kwani kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 6.1 zitakazowawezesha vijana wengi kujiajiri kwa kubuni na kuanzisha Miradi ya Uzalishaji Mali kupitia Halmashauri zote nchini. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaamini fedha hizi ni kidogo ukilinganisha na idadi kubwa ya Vijana ambao hawana ajira. Hivyo, kwa umuhimu huo Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali ihakikishe inafuatilia na kutathmini kwa umakini ili kuhakikisha malengo ya Miradi ya Vijana inafikiwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


na pesa zilizokopeshwa zinarudishwa ili waweze kukopeshwa Vijana wengi zaidi;

(ii) Ni vyema Wizara na Halmashauri zote nchini kushirikiana kwa ukaribu ili kufuatilia vizuri fedha ambazo zinatolewa na Halmashauri, asilimia tano kwa ajili ya kuimarisha Mfuko huu wa Vijana; na

(iii) Waajiri wapunguze vigezo vya uzoefu (*Working Experience*) vinavyohitajika katika kuajiriwa kazini kwa kuwa vigezo hivyo vimekuwa vikwazo vikubwa hasa katika upatikanaji wa ajira mpya, unakwenda kuomba kazi tangazo linasema uwe na uzoefu wa miaka sita wakati wewe umetoka Chuo Kikuu jana, kwa hiyo, hili ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*Women Development Fund*), ulianzishwa kutokana na Azimio la Bunge lililopitishwa mwaka 1993 kwa mujibu wa *Exchequer and Audit Ordinance* ya Mwaka 1961 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001 *(Public Finance Act, 2001)*. Mfuko huu unachangiwa fedha kutoka Serikali Kuu na Halmashauri zinapaswa kuchangia asilimia tano ya mapato yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Mfuko huu ni kutoa mikopo kwa Wanawake ili kuwaimarisha kiuchumi. Aidha, madhumuni ya Mfuko huu ni kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa Wanawake wenye kipato kidogo, kuongeza ajira na kipato kwa Wanawake, kujenga tabia ya kujiwekea akiba kwa ajili ya upanuzi wa shughuli zao za dharura na kutafuta vyanzo vingine vya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua juhudi zinazofanywa kwa kutenga bajeti ya shilingi bilioni mbili zitakazowawezesha kuwakopesha Wanawake kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali na kupambana na umaskini kwa kuunda vikundi vidogo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo

kwa Serikali, Kamati inashauri kuwa Vikundi vyote vya Wanawake vihimizwe kurejesha mikopo hii kwa wakati ili Halmashauri ziweze kuchukua mikopo tena Serikalini na kuwakopesha Wanawake wengi zaidi. Vilevile Halmashauri zote zichangie asilimia tano ya mapato yake kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ili kuendelea na kuwepo ushirikiano kati ya Maafisa wa Maendeleo ya Jamii na Wabunge wa maeneo husika. Hatua hii itahamasisha kuwakwamua Wanawake wengi hasa waliopo vijijini hadi kule Kigoma Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ifanye tathmini ya kina kuhusu utendaji wa Mfuko na kupata taarifa ya kina ikiwemo kupata uzoefu wa Mifuko mingine ili Mfuko huu uwe endelevu kama mkakati wa muda mrefu.

Wizara iboreshe mwongozo wa kutoa mikopo kwani mwongozo unahitaji kuboreshwa kwa kuainisha vigezo vitakavyotumika katika kugawa fedha kwa kila Halmashauri na Vikundi vya Wanawake na pia kuweka utaratibu wa ufuatiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake Tanzania *(TWB),* ilianzishwa kwa lengo la kuwakomboa Wanawake kiuchumi kwa kuwawezesha kupata mikopo kwa riba nafuu na kwa ajili ya kukuza mitaji ya kibiashara. Benki ya Wanawake Tanzania hupokea mtaji wa shilingi bilioni mbili kutoka Serikalini. Benki hii inalazimika kuchukua amana toka Mashirika makubwa ili kukidhi mahitaji yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Benki imeweza kuongeza amana za wateja hadi kufikia shilingi bilioni 13.6 hadi Desemba, 2010 kutoka shilingi 12.7 ilivyokuwa mwisho wa mwaka 2009, ikiwa ni ongezeko la shilingi 10.9 bilioni. Ongezeko hilo hutolewa kwa mafunzo kwa vikundi mbalimbali vya Mkoani Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Mwanza na Pwani. Aidha, Benki imeweza kutoa mikopo kwa watu binafsi, *SACCOS,* Makampuni na Vikundi mbalimbali vikiwemo Vikundi Maalumu vya Wajasiriamali wadogo wadogo. Pia kwa kipindi cha miaka minne, mikopo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


iliyotolewa na Benki ni zaidi ya wateja 27,000 yenye thamani ya shilingi bilioni 35.0.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya, Benki ya Wanawake Tanzania bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

- Bado inatumia akiba za wateja; hivyo, kutoa mikopo bila kufuata taratibu za Benki Kuu.

- Kuwa na mtaji mdogo ambao hairuhusu kufungua matawi mengi mikoani ambacho kimekuwa ni kilio cha Wabunge wengi, Benki haipo hata Zanzibar kwa hiyo ni tatizo.

- Kushindwa kuuza dhamana kwa wakati mwafaka sababu ya ucheleweshwaji wa kesi mahakamani.

- Utumiaji wa huduma za washindani, Benki bado hairuhusiwi kushiriki *clearing house*, inalazimika kutumia huduma za washindani kama *NBC.* Aidha, benki inashindwa kutoa huduma za haraka kwa wateja kwa sababu ya kusubiria cheki kutoka *NBC,* pia inapoteza mapato kwa sababu ya kulipa ada kubwa ya kupitishia cheki na uhamishaji fedha kupitia washindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizi, Kamati inaushauri kuwa:-

- Serikali kuangalia namna ya kuwatumia Wanahisa katika kukuza Mtaji wa Benki ya Wanawake Tanzania, ili kuiwezesha Benki kupata Leseni ya Benki ya Biashara pia itaiwezesha kufungua matawi sehemu nyingi nchini na kuwafikia walengwa.

- Wizara, Idara za Serikali, Taasisi za Serikali na watu binafsi, watumie huduma za Benki ya Wanawake Tanzania kulipia mishahara na kuchukua mikopo.

- Benki hii ianzishe huduma ya kuweka na

kutoa pesa katika akaunti kwa njia ya simu kama ambavyo mabenki mengine wanafanya ili kwenda sambamba na ushindani.

- Serikali ione umuhimu wa kutoa mtaji kwa benki hii ili kuongeza na kuwawezesha Wanawake wa Tanzania kijikwamua kiuchumi. Serikali itekeleze ile ahadi yake ya kutoa kiasi cha shilingi bilioni mbili kila mwaka kwa Benki hii.

- Kamati inaishauri benki iuze hisa zake ili kuongeza mtaji na Wanawake na Wanawake wenyewe kuwa mstari wa mbele kununua hisa kwa sababu ni walengwa wakuu wa Benki hii.

- Benki ya Wanawake Tanzania ione umuhimu wa kufungua huduma zake Tanzania Visiwani, yaani Zanzibar, ili kutimiza azma ya kuwawezesha akina mama wa Visiwa vya Zanzibar kunufaika na mikopo hii kupitia benki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008) ni kuhakikisha kwamba, watoto wote wanastawi na kuwa na maisha bora kutokana na kupatikana kwa haki zao za msingi ambazo ni kuishi, kuendelezwa, kulindwa na kushiriki katika mambo yanayowahusu bila ubaguzi wa hali yeyote. Kwa kuzingatia haya, Kamati inashauri yafuatayo:-

- Halmashauri zote zifuate na kuzingatia sheria ndogo zinazohusu watoto ili kuwapatia haki zao za msingi ili kupunguza wimbi kubwa la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi;

- Serikali iweke utaratibu wa uimarishaji wa mifumo ya kijamii ya kutunza watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi;

- Serikali kuyachukulia hatua za kisheria Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayojinufaisha kupitia

migongo ya watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi.

- Serikali kuhakikisha mara kwa mara inatoa ripoti Bungeni kuhusu takwimu zinazoonesha hali ya watoto walio katika mazingira hatarishi na hatua zilizochukuliwa kwa wote wanaovunja haki za watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inatamka umri wa kufunga ndoa kwa kijana wa kiume ni miaka 18 na kwa kijana wa kike ni miaka 15. Sheria hii inakinzana na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, ambayo inamtaja mtoto kuwa ni yule aliye chini ya miaka 18, hivyo, kufanya Sheria ya Ndoa kuruhusu ndoa kwa watoto. Kamati inaishauri Serikari ilete marekebisho ya Sheria ya Ndoa kutokana na changamoto zinazojitokeza kwa hivi sasa. Serikali na jamii iendelee kutoa elimu kuhusu athari za ndoa za utotoni.

Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto, pamoja na kuwepo kwa Sheria na Vyombo vya Kiutawala. Bado matukio ya Wanawake na Watoto kuendelea kuteswa na kunyanyaswa ni mengi mno. Wanawake wanapigwa na kufanyiwa vitendo vya ukatili vinavyopelekea baadhi yao kupata ulemavu wa viungo na wakati mwingine kufa au kupoteza heshima na utu wao, wengine kubakwa na kunyanyaswa kijinsia katika maeneo mbalimbali. Kamati inasikitika kuona unyanyasaji huu bado unaendelea na hatua za kutosha za kukabiliana na janga hili hazijafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira za watoto siyo tu ukiukwaji wa haki za watoto, pia ni ukiukwaji wa Sheria na Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia. Tatizo la ajira kwa watoto bado ni kubwa kwenye maeneo ya migodini, mashamba ya chai, mashamba ya tumbaku na sehemu za uvuvi. Serikali ichukue hatua za haraka zitakazosaidia kuwanusuru watoto hao. Aidha, Serikali itekeleze wajibu wake wa kulinda raia wake ikiwemo watoto wanaotumikishwa katika ajira mbaya, kuwarejesha watoto hao kwenye maisha ya kawaida (kuwarejesha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

shuleni au katika familia zao). Jamii ipewe elimu ya kutosha kuhusu utumikishwaji wa watoto katika kazi za hatari na kutambua haki za mtoto na kuwafikisha mbele ya Sheria wale wote wanaoajiri watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kazi na Ajira: Usalama na Afya za Wafanyakazi Mahali pa Kazi vinapaswa kuzingatiwa kwa kiwango cha juu sana, vikipuuzwa vinaweza kuwa na madhara si kwa mwajiri au mwajiriwa pekee, bali hata kwa Uchumi wa Taifa. Ingawa ni jukumu la wadau wa ajira (Waajiri na Wafanyakazi), kuhakikisha afya na usalama mahali pa kazi, bado Serikali ina wajibu wa kuhakikisha inaweka viwango vya usalama na afya mahali pa kazi na kusimamia kikamilifu utekelezaji wake ili kunusuru afya za Wananchi wake na hivyo kulinda ukuaji wa Uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona ingawa *OSHA* imepewa majukumu makubwa ya kuhakikisha afya na usalama vinazingatiwa mahali pa kazi, bado Serikali kupitia Wizara, haijaiwezesha kikamilifu kutekeleza majukumu haya. *OSHA* inakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo uhaba wa rasilimali watu, rasilimali fedha, majengo ya ofisi hayakidhi mahitaji ya nafasi na ubora unaotakiwa, pamoja na vitendea kazi na vifaa vya ofisini. Pamoja na changamoto zilizopo, tunaupongeza Utawala na Mkurugenzi Mkuu kwa utendaji wao mzuri wa kazi kwa kuhakikisha sheria na taratibu zinazohusu afya mahali pa kazi zinafuatwa; hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo kwa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sheria Namba 6 ya Mwaka 2004, bado kumekuwepo na migogoro kadhaa katika Viwanda, Mashirika na Makampuni. Migogoro hii inasababishwa na sababu mbalimbali zikiwemo:-

- Waajiri kutokutoa mikataba ya ajira kwa muda mrefu.

- Waajiri kutozingatia hali ya afya na usalama

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

mahala pa kazi (Wafanyakazi kutokuwa na vitendea kazi na vifaa vya kujikinga na madhara yatokanayo na kazi wanazozifanya).

- Uelewa mdogo wa waajiri katika kutambua sheria na taratibu za ajira kwa kutambua stahili za ajira za kudumu na ajira za muda.

- Waajiri kutotekeleza masharti ya sheria za kazi.

- Kushindwa kutoa stahili za Kisheria kwa Wafanyakazi kama vile likizo za ugonjwa, uzazi, likizo ya mwaka na kadhalika.

- Waajiri kutokuwa na *Job Description* hivyo Wafanyakazi kufanya kazi bila mipaka na kwa kutumikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za hapa nchini kwetu zinaonesha kuwa Vijana walio na ajira katika sekta rasmi ni 188,000, sawa na asilimia 1.2 na Vijana walio katika Sekta binafsi ni 1,000,000 sawa na asilimia 6.2 na Vijana 1,100,000 sawa na asilimia 6.8. Sehemu ya Vijana wanaohitimu Shule na Vyuo Vikuu wapo katika kipindi cha mpito na utagundua kuwa kuna kiwango kikubwa cha ukosefu wa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Vijana, nguvu kazi ya Taifa inakadiriwa kuwa ni watu milioni 17.9 ambapo asilimia 65 ni Vijana wenye umri kati ya miaka 15 mpaka 35. Ripoti ya Serikali ya Mwaka 2012 inaonesha kuwa, idadi ya Vijana waliokuwa na ajira wenye umri wa kati ya miaka 15 mpaka 35 ni 9,056,217, ambao ni sawa na asilimia 86.6 na Vijana wasio na ajira ni 1,398,677 ambao ni sawa na asilimia 13.4. Kamati inaishauri Serikali kulishughulikia kwa kina jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazee ni kundi muhimu sana katika jamii yoyote ile duniani na kwa Tanzania, Wazee

wamekuwa nguzo muhimu katika kuhimiza maadili mema, malezi bora, usalama na kuwa washauri wakuu katika masuala mengine muhimu ya kitaifa hasa katika kipindi hiki ambacho jamii inapitia mabadiliko makubwa ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Takwimu zinaonesha kuwa, wazee hapa nchini wanakadiriwa kufikia milioni 2.1, sawa na asilimia 4.5 ya Watanzania wote *(Population Projection 2010)*. Asilimia 83 ya wazee wote wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kila kaya inakadiriwa kuwa na mzee mmoja ambaye anahitaji msaada kutoka kwa wategemezi. Kiwango cha umaskini katika kila kaya zenye wazee na watoto ni kikubwa na kinakadiriwa kuwa ni asilimia 22.4, ukilinganisha na kiwango cha umaskini kitaifa, ambacho ni asilima 33.4. Hali hii pamoja na mambo mengine, inasababisha wazee na familia zao kukabiliwa na changamoto ya gharama kubwa za kuwawezesha kupata huduma muhimu za maisha kama vile matibabu ya magonjwa mbalimbali yanayowakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa, kundi kubwa la wazee lipo katika hatari kubwa zaidi ya kukabiliwa na matatizo ya kiafya na ulemavu kuliko kundi lingine lolote. Mpaka sasa asilimia 33 ya wazee wote nchini ni walemavu. Pamoja na kukabiliwa na hali hii, inakadiriwa watoto yatima ni milioni moja wanaoishi katika mazingira magumu na wanatunzwa na wazee. Aidha, Kamati inasisitiza Serikali itekeleze na kuhakikisha kuwa, Wazee wanapata matibabu bure mahali walipo. Aidha, Kamati inasisitiza Serikali kuandaa mchakato wa pensheni kwa Wazee.

Kufuatia uwepo kwa wadaiwa sugu katika Taasisi, Wizara, Wakala na Idara za Serikali, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa wadaiwa hawa wanalipa madeni yao mara moja, wale ambao wanadaiwa na *TBC*. Kwa hiyo, hata kama Bunge mnadaiwa basi Kamati inaelekeza hapa kwamba, tulipe madeni hayo *TBC* iweze kujiendesha.

Serikali itoe dhamana kwa *TBC* ili Shirika liweze

kushirikiana na *NSSF* kujenga Jengo la Utawala lililopo Mikocheni, ambalo litatumika kama kitega uchumi na hatimaye Shirika la Utangazaji *(TBC)*, kujiendesha lenyewe. Tumependekeza hili ili pia itoe fursa kwa Wizara ya Habari ambayo inakodi jengo kwa sasa kuhamishia ofisi zake pale, endapo jengo hili litakuwa limekamilika, kwa sababu ni fedheha kwa Wizara kuendelea kupanga katika majengo mbalimbali.

Kwa kutambua kuwa tatizo la ajira kwa Vijana limekuwa kubwa, Kamati inaitaka Serikali kuja na mpango mkakati wa namna ya kukabiliana na changamoto hii.

Serikali kwa kushirikiana na Balozi zetu ziainishe namna ya kutoa taarifa juu ya uwepo wa ajira katika maeneo mbalimbali ya dunia; kwa sababu tumejifunza katika nchi ya Malaysia na wanakaribisha Watanzania na watu wengine, kuchangamkia fursa ambazo zipo katika maeneo hususan ya Bandari. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali sasa kupitia Ubalozi wetu waweze kufanya kazi hii na kutoa taarifa kwa umma ili Vijana wetu waweze kuajiriwa.

Kuhusu fao la kujitoa, ni vizuri Serikali kwa kushirikiana na Msisimamizi na Mdhibiti wa Mifuko ya Jamii *(SSRA)*, kufanya utafiti wa kina kuhusu fao la kujitoa, athari yake ni nini na faida yake ni nini, ili kubainisha mazingira mahususi ya Mwanachama kujitoa katika mfumo kwa sababu siyo jambo la kawaida unapojiunga katika Mfuko wa Pensheni kujitoa, inakuwa haikusaidii wakati wa uzee. Aidha, Serikali iondoe sharti la muda wa uzoefu wa miaka kadhaa kabla Vijana wanaomaliza masomo ya juu kufanya kazi ili kurahisisha kupata ajira. Sharti la miaka ya uzoefu *(working experience)* litumike pale tu mtumishi anapotaka kupandishwa daraja *(promotion).*

Serikali ilete Muswada wa Vyombo vya Habari na uhuru wa kupata habari haraka iwezekanavyo.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru, nakushukuru sana, maliza muda wako umekwisha.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. SAID M. MTANDA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahitimisha kwa kusema, Serikali ilete Muswada wa Vyombo vya Habari na Uhuru wa Habari ili Bunge hili liweze kupitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Mawaziri ambao tunashirikiano nao; Mheshimiwa Sophia Simba - Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangala - Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka - Waziri wa Kazi na Ajira. Vilevile napenda kuwashukuru Mheshimiwa Ummy Ali Mwalimu - Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Amosi Makala - Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga - Naibu Waziri wa Kazi na Ajira kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati. Kamati hii imekuwa kama familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inawapongeza pia Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo, kwa uteuzi wao. Tunawahakikishia ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namshukuru Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas Kashililah na Katibu wa Kamati - Ndugu Happiness Ndalu, kwa kuihudumia Kamati wakati wote. Nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kuyakubali Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu wa sasa hivi watakuwa sita. Tutaanza na Mheshimiwa Barwany, Mheshimiwa Owenya, Mheshimiwa Marombwa, Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Nassib Omari na Mheshimiwa Makilagi. Tunaanza na Mheshimiwa Barwany!

**MHE. SALUM H. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa kuchangia Kamati mbili hizi.

Kwanza, nielezee umuhimu wa hizi Kamati mbili ambazo tunaweza tukasema ni pacha. Umuhimu wake ni kwamba, hatuwezi kupata maendeleo kama bado hatujapata huduma muhimu za jamii na huduma muhimu za jamii zikiimarika, ndipo maendeleo ya kweli yanaweza kupatikana. Kwa maana hiyo, Kamati hizi mbili ni muhimu kabisa katika maendeleo ya Taifa letu. Hayo mengine yote yanakuja baada ya huduma kupatikana na maendeleo tunayaona yanapatikana kwa kukamilika hizo huduma.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia hoja yangu juu ya eneo muhimu kabisa la watu wenye ulemavu wa ngozi katika Taifa letu. Kwa muda mrefu tulikuwa tunazungumzia suala hili, mauaji yameanza takribani miaka mitano, sita iliyopita na inasemekana bado yanaendelea kuwepo katika Taifa hili, hata kama Serikali inasema mwaka huu watu watatu tu wenye ulemavu wa ngozi ndiyo waliopoteza maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vituo au shule ambazo tayari ziliandaliwa na Serikali katika maeneo mbalimbali hapa nchini mara tu baada ya janga la mauaji kupatikana. Pamoja na nia nzuri ya Serikali, lakini imeonekana athari kubwa katika maeneo yale hasa katika

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



shule ambazo zimewekwa maalum kwa ajili ya watoto wenye ulemavu wa ngozi katika maeneo ya Mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, kule wale watoto na kama wametelekezwa, hawapati huduma muhimu ambazo zinahitajika katika vituo vile au katika Shule zile. Inapelekea hata wazazi ambao wamewapeleka watoto katika shule zile, wamefanya kama wameshatua mzigo, wameitulia Serikali, hawashughuliki kabisa kuona jinsi gani watoto wao katika vituo vile wanapata elimu bora, wanapata matunzo mazuri na wanahifadhiwa kama vile wamekusudiwa waboreshwe katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, imefikia mahala tunaishauri Serikali kama imeshindwa kutoa huduma muhimu, basi ni bora watoto wale warejeshwe katika familia zao. Itasaidia katika maeneo mawili au moja; kwanza, watapata maadili bora ya jamii yao; na pili, watachanganywa na jamii nyingine kupata uzoefu wa maisha yao ya siku za baadaye kuliko ambavyo wametengwa pale katika vituo vile, lakini bado huduma muhimu ambazo zilikuwa zinatarajiwa katika kuwaweka pale zinakosekana kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Walimu ni la muda mrefu, limekuwa sugu na limekuwa ni donda ndugu katika Taifa hili, kiasi kwamba, imefika mahala sasa kuna chuki baina ya Serikali na Walimu. Imefikia mahala Mwalimu anaona kwamba, kususia kutoa huduma katika shule basi anaikwaza Serikali. Vilevile inafikia mahala pia siyo kuikwaza Serikali tu, lakini pia watoto ambao wanahitaji kupata elimu na msaada mkubwa unaotokana na Walimu inafikia mahala Wanafunzi nao wanakata tamaa.

Kuna shule moja katika Jimbo langu, kuna mwalimu yupo zaidi ya miaka 30 hajahama katika shule ile. Amekuwa kama mwanakijiji wa kawaida. Sisi katika umri wetu kule nyuma wakati tunasoma Mwalimu alikuwa mtu adimu. Mwalimu alikuwa mfano wa kuigwa, mtu anafika mahala

anasema mimi katika maisha yangu ya baadaye ninataka kuwa kama Mwalimu fulani lakini leo hiyo haipo. Kwa maana kwamba, Walimu wamewekwa katika mazingira ambayo wametengenezewa hata wasijitambue, wasijue wana majukumu gani ndani ya Taifa letu.

Hivyo, ni vyema tukaangalia upya, tumepiga kelele sana, Walimu katika Vyama vyao vya Walimu nao wamepiga kelele, lakini Serikali yetu bado imeweka pamba katika masikio, imekuwa kiziwi na vipofu katika hoja ya Walimu. Sasa ni vyema tukaanza upya kuangalia matatizo ya Walimu jinsi gani tunaweza tukaboresha na wakaishi katika maisha mazuri na sisi watoto wetu wakapata elimu bora, tukawaachia urithi wa nchi hii watu ambao tayari wanaweza kumudu kuiendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Benki ya Wanawake, limezungumzwa kwa muda mrefu, lakini masikitiko yetu na tumekaa katika Kamati kuzungumzia suala hili. Benki ya Wanawake inakwenda mijiini tu. Tunasema Benki ya Wanawake ipo Dar es Salaam, lakini ukiangalia mazingira ya miji ni maeneo ambayo tayari kuna maisha mazuri, *Alhamdulillah,* kule kuna kipato kinachotosheleza lakini hebu tuangalie mazingira ya Wananchi wetu huko vijijini jinsi wanavyoishi. Tulifikiria huduma hizi za kibenki zingekwenda kuwasaidia watu wa daraja la chini huko katika Wilaya zetu katika Tarafa zetu na Vijiji vyetu.

Tukiangalia takwimu, benki hizi ziko wapi; zipo Dar es Salaam tu. Tunaweza tukasema labda benki hizi zimetengenezwa kisiasa zaidi, lakini haja ya msingi kabisa kwa benki hizi ni kuboresha maisha ya Wanawake wanaoishi vijijini, ambao bado wanaishi katika mazingira magumu kabisa; hawana maji, hawana elimu, hawana nini, kuwapa uwezo wa kiuchumi kutawasaidia kumudu kupata huduma hizo ambazo tayari zipo mbali na wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la pensheni ya wazee. Suala hili limekuwa ni kigugumizi kwa

Serikali, kwa muda mrefu kabisa, tumezungumzia suala la pensheni ya wazee. Hivi hatuoni kazi waliyofanya wazee kwa muda mrefu ndani ya Taifa hili? Sisi tumekuwa wenyeji hapa katika Dunia hii baada ya Wazee wetu kutangulia, wamefanya mengi, wametoa huduma nyingi, lakini bado Serikali haijaona umuhimu wa Wazee hawa walipofikia hapa kuwasafirisha katika safari yao ya mwisho wakiwa salama na kufurahia matunda waliyoyapata katika kazi ambazo walizifanya huko nyuma.

Tunasema kwamba, sasa hivi huduma za Wazee zinawapata wale tu ambao walikuwa katika ajira rasmi, walikuwa Walimu, walikuwa Madaktari au walikuwa katika fani mbalimbali, lakini kuna ambao hawakuwa katika ajira rasmi, wamefanya kazi kubwa, walikuwa madereva leo hawawezi tena kuendesha magari, walikuwa wakulima hawawezi tena kulima, walikuwa wavuvi, walikuwa wakwezi, walifanya kazi mbalimbali wamechoka sasa uwezo wa kufanya kazi hawana. Je, tunawatazamaje Wazee hawa? Tunawaweka katika mazingira gani Wazee hawa? Tunasema kwamba, wakati sasa wa kulipa pensheni kwa Wazee umefika.

Hili siyo suala la kisiasa tena, ni suala la maendeleo ya kijamii. Wazee wetu wanataka msaada kutoka kwetu. Tumekwenda katika nchi mbalimbali tumeona ni jinsi gani WAzee wanaenziwa na wanatunzwa. Niseme kwamba, mambo mengine haya ambayo tunayaona, tunapanga mipango hapa haiendi vizuri, vikwazo chungu nzima, lakini inatokana na kutokuwa na baraka ya Wazee wetu.

Wazee kama bado hata waumini wa dini zote wanasema pepo ipo chini ya nyayo ya wazee wetu. Wazee wana huduma nzuri, Wazee wetu wanaambiwa wachawi huko, siyo wachawi kwa sababu tayari wanaishi vibaya, macho mekundu na hawapati huduma zozote ambazo zinastahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema sasa Serikali ikaacha kigugumizi chake na ikaona kuna haja kabisa ya

kuwaandaa wazee wetu, wana ulezi mkubwa, tumeambiwa hapa kwa mujibu wa maelezo ya Makamu Mwenyekiti katika Kamati yake, anasema kwamba, asilimia nne ya Watanzania ni wazee. Zaidi ya watoto yatima milioni 1.2 wanaishi katika mazingira magumu, wazazi wao wamefia mijini huko kwa magonjwa mbalimbali, wanarudi wanachukuliwa na Wazee wao kupelekwa vijijini huko. Unamkuta babu yake au bibi yake hana uwezo wowote wa kujimudu, unampa mzigo tena wa kuwa na ulezi, alishamaliza ulezi zamani, lakini leo tayari kwa matatizo yaliyowapata, wazee wale wanachukua tena jukumu la ulezi wa watoto yatima ambao tayari walipaswa kusaidiwa ili kubadilisha mazingira yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazee tuwaenzi na tuwahudumie ili waweze kuishi katika mazingira bora. Nasi naamini kabisa, Mwenyezi Mungu, ataleta baraka na maisha yetu yatakuwa bora.

Mwisho, nimalizie na suala la *TBC.* Sasa hivi kuna ushindani mkubwa wa vyombo vya habari. Hakuna nchi yoyote Duniani chombo chake cha Serikali kikawa dhaifu kama ilivyo *TBC.* *TBC* ni Chombo cha Taifa, mambo yetu yote muhimu yanatakiwa yazungumzwe kupitia Chombo chetu cha Serikali. Vyombo vingine ni vya kibiashara tu, lakini *TBC* ni Chombo cha Taifa, kinahitaji msaada mkubwa kabisa.

Tunaambiwa kuna madeni mengi hapa na tunaambiwa kwamba, madeni mengi ni ya Serikali yenyewe, inapewa huduma lakini inashindwa kuifanya *TBC* ipate bajeti nzuri iweze kumudu kufanya shughuli zake.

Tunapata taarifa kwamba tayari kuna maeneo kuna usikivu dhaifu, wanasikiliza redio za nje kuliko redio za Taifa lao. Hili tuliangalie upya na tuone namna gani tunaweza tukaiboresha *TBC*, tukawa na chombo ambacho tutajivunia. Pia tunashauri chombo hiki sasa kijiendeshe

kibiashara ili kiingie katika ushindani. Huu mpango wa kutumia *TBC* tu kwa maana ya kuona ni chombo chetu wakati ... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Barwany. Sasa namwita Mheshimiwa Owenya!

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika Ripoti za Kamati. Awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote ili iweze kuendelea ni lazima iwe na watu wenye afya nzuri na elimu nzuri. Cha kusikitisha, Bajeti ya Afya bado Serikali haijaweza kuipatia asilimia 15 ya bajeti kama Azimio la Abuja la Mwaka 2011 lilivyoelekeza. Kwa kutokuwa na bajeti ya kutosha kwenye Wizara ya Afya, inachangia washindwe kufanya maendeleo na vilevile wanashindwa kutekeleza majukumu yao, wanakuwa na uhaba wa watumishi, uhaba wa vifaa na kadhalika.

Serikali imekuwa ikitueleza hapa Bungeni kwamba, wazee, akina mama wajawazito na watoto chini ya miaka watibiwe bure, lakini mpaka sasa kwenye hospitali nyingi unakuta akina mama bado wanapeleka vifaa kwa ajili ya kujifungulia. Kwa hiyo, ina maana Serikali bado inahitaji kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia ina mikakati ya kujenga Zahanati katika kila Kijiji na Vituo vya Afya katika kila Kitongoji. Hili ni jambo zuri, lakini ningeshauri kwamba, kwanza, Serikali iboreshe vituo vilivyopo kwa sababu havina wahudumu, havina vifaa na wafanyakazi kule wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Vilevile Wafanyakazi wa zahanati kule chini wanafanya kazi kwa

saa tisa, wanafanya kazi kuanzia saa 1.00 mpaka saa 9.00. Tuzingatie kwamba, mgonjwa hana muda wa kuugua na hasa vijijini, zahanati zipo mbali sana na Hospitali za Wilaya. Kwa hiyo, ningeshauri Hospitali zile ziboreshwe ili ziweze kufanya kazi kwa saa 24 tuweze kuokoa maisha ya watu walioko vijijini.

Vilevile Serikali izisaidie zahanati za vijijini zipate mafriji, maana wengi wanalalamika kwamba, dawa nyingi inabidi zihifadhiwe kwenye mafriji na vijijini, sehemu nyingi hazina umeme, wawapatie majenereta ili waweze kuhifadhi dawa na kuokoa maisha ya watu walioko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali za Wilaya kwa sasa nyingi zimezidiwa na wagonjwa. Naomba nitolee mfano, Hospitali Teule ya Moshi ya St. Joseph. Hospitali ile wamejitahidi sana, naomba nimpongeze Sr. Lyimo, amejenga wodi kwa ajili ya akina mama lakini kwa sasa hawana vitanda wala hawana mashuka. Nimekuwa nikiongea mara nyingi hapa Bungeni, kuiomba Serikali iwasaidie Hospitali ile kwa sababu imekuwa mkombozi kwa Wakazi wa Moshi.

Unakuta Hospitali ya Mawenzi haifanyi kazi, haina *theatre*, wala haina wodi kwa ajili ya akina mama, kwa hiyo wengi wanaenda katika Hospitali ya St. Joseph. Hivi sasa hospitali ile imeelemewa. Kwa hiyo, chonde chonde Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimeshamwomba mara nyingi na TAMISEMI nimewaomba, waisaidie Hospitali ya St. Joseph ili waweze kuwasaidia akina mama waweze kulala kwenye vitanda. Wanachohitaji kwa sasa hivi ni vitanda 50 tu.

Kwa hiyo, Serikali inaweza ikasaidia kupitia TAMISEMI, waweze kupata vitanda vile na akina mama waweze kuokoa maisha yao, maana kwa sasa hali ni mbaya, ukizingatia KCMC imejaa. Hospitali ya KCMC wagonjwa wanalala chini katika wodi ya kwanza na wodi ya upasuaji. Hospitali imeelemewa. Hospitali kama KCMC ni ya Rufaa, haina *CT-Scan* kwa sasa, tunaiomba Serikali iende ikaiangalie Hospitali ile; kwa mfano, sasa hivi kuna ajali

*[MHE. LUCY F. OWENYA]*

imetokea watu wamekimbizwa KCMC, lakini wanashindwa kuhudumiwa kwa sababu vifaa muhimu vidogo vidogo havipatikani. Hali siyo nzuri katika Hospitali yetu ya Rufaa kama watu wanavyofikiria.

Mheshimiwa Spika, pia ningeomba Serikali katika majibu yake watueleze ile wodi ya akina mama na *theatre* pale Mawenzi imefikia wapi, wapeleke pesa pale ili iweze kutusaidia, watu wengi wasiende kujazana sana *KCMC* na katika Hospitali Teule ya St. Joseph.

Vilevile naungana na Kamati kwamba, deni la *MSD* la bilioni 52 sasa Serikali ililipe; ni matatizo kwa sababu unakuta wagonjwa wengi wakienda kwenye Hospitali za Wilaya wanakosa madawa, inabidi waende wakanunue madawa kwenye maduka binafsi. Inakuwa ni ghali sana kwa watu. Unakuta dawa za malaria ambazo zinaweza kupatika katika Hospitali za Serikali saa nyingine hawazipati mpaka *MSD* ipeleke na *MSD* hawapeleki kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Kwa hiyo, Serikali walipe deni hili ili *MSD* nao waweze kupeleka dawa hizi.

Mheshimwa Spika, naomba nichangie kidogo kuhusu elimu. Elimu ni msingi wa kila kitu. Kwa siku za hivi karibuni tumeona elimu imezidi kuporomoka, watoto wanafeli, lakini hii inachangiwa zaidi na Wizara kwa kutopewa fedha za kutosha na pia kutokuwa na mazingira mazuri ya kufundishia na Walimu kutokuwa na motisha ya kutosha. Mfano, shule nyingi hasa za vijijini unakuta hazitimizi vigezo sijui kwa nini zinaruhusiwa kufunguliwa? *(Makofi)*

Unakuta kuna shule nyingine zina Mwalimu mmoja. Shule za Primary Mwalimu mmoja anafundisha darasa la kwanza mpaka la saba. Mwalimu huyo huyo afundishe masomo yote.

Shule nyingine wanakaa chini ya miti wanajifunza, shule nyingine hazina hata maji, watoto wanaishia kwa kusomba maji vijijini. Unakuta shule nyingine hazina matundu ya kutosha ya choo; hii kwa watoto wa kike inachangia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



wanakosa kwenda shuleni kwa sababu tu hamna maji na vyoo shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Kamati kabisa katika Ripoti yao, ukurasa wa 13, ambao wamesisitiza kwamba, Serikali iwawezeshe Idara ya Ukaguzi wa Elimu Nchini kuwa Wakala wa Kujitegemea ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzingatie kwamba, Walimu wanaoenda vijijini wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, wanapaswa walipwe posho ya mazingira magumu. Unakuta mwalimu anaishi mjini unampa *post* aende kijijini anafika kijijini hana nyumba ya kuishi, akitaka kufundisha hamna hata ubao wa kufundishia, wanaenda kufundishia watoto chini, hamna nyumba; unategemea mwalimu yule atakubali kuishi kule kweli? Kwa hiyo, nafikiri wakipewa hii motisha ya kulipwa posho wanaweza wakakubali wakaenda vijijini.

Mwisho kabisa, naomba niungane na Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu wanafunzi wa shule za awali kuanzia darasa la kwanza mpaka la tatu wafundishwe yale masomo ya KKK (Kusoma, Kuandika na Kuhesabu). Unakuta mtoto wa *primary* anapewa masomo 12. Nilimwona mtoto wa mdogo wangu anabeba vitabu vingi, sasa mtoto yule hawezi ku-*concetrate,* anachukia shule, hawezi kwenda kusoma masomo yote hayo mtoto mdogo, akili yake bado anatakiwa ajifunze kuunda herufi, kuhesabu na kuandika. Akifika darasa la nne ndiyo aendelee sasa kupewa masomo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni udhibiti wa vipodozi na vyakula. Watu wanaathirika sana na hivi vipodozi, wengine wanapata saratani. Sasa hivi tumeona Wachina wanaleta madawa wanasema ya kuondoa sumu mwilini. Serikali haijatueleza hivi hizi chai zinazoletwa na madawa yanayoletwa wanasema ni ya kuondoa sumu mwilini; mmefanya utafiti? Tunaona saratani inaongezeka; pengine ni sababu ya hizi dawa!

Tunaona magonjwa ya visukari yanaongezeka, maana wanasema inaondoka visukari, inaondoa presha. Je madawa haya yanachangia katika magonjwa haya? Serikali imeshafanya utafiti na kujua hizi dawa za Wachina, za Wakorea, zinazoletwa hapa nchini za kutoa sumu mwilini ni kweli zinatoa sumu mwilini au zinatuongezea magonjwa? Serikali iliangalie hili kwa umakini wake na wale wanaotumia mikorogo chonde chonde nawaomba, achaneni na hivyo vitu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Marombwa, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Mbassa badala ya Mheshimiwa Zitto.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipatia nafasi nichangie hoja zilizotolewa mbele yetu na Kamati ya Kudumu ya Bunge Huduma za Jamii pamoja na Maendeleo ya Jamii.

Nianzie kwa upande wa elimu. Naunga mkono maelezo yote ambayo yametolewa na Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nami nataka kuchangia maeneo machache. Ukiangalia kwenye ukurasa wa kumi, Wameelezea pale katika *bullets* ya kwanza, ya pili na ya tatu, ni kuwezesha mafunzo kazini kwa Walimu kuwa endelevu na kutolewa kupitia Mpango Maalum wa Mafunzo Kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sana Walimu wetu hawajapata mafunzo kazini. Miaka ya nyuma Walimu walikuwa wanakwenda mara kwa mara, lakini kwa zaidi ya miaka kumi sasa, Walimu hawa hawana *in-service course* yoyote inayotolewa. Ukishamaliza chuo unapelekwa shuleni, basi huko shuleni utaendelea kukaa mpaka muda wako wa kustaafu unapofika ndipo unaacha kazi, hakuna *in-service training*. Sasa Serikali imejiwekea lengo kwamba, ifikapo mwaka 2014, kwa mfano, kwa upande wa Elimu ya Msingi, tunataka wanafunzi wetu wanaomaliza Elimu ya Msingi, asilimia 80 wafaulu. Ukiangalia mwenendo wetu wa

matokeo ya mitihani, tunakwenda hapo kwenye asilimia 80 hatufiki. Hatujiulizi chanzo ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tupo asilimia 55, matokeo ya mwaka jana, ya mwaka huu ni asilimia 53 tu. Chanzo kikubwa mafunzo kwa Walimu hayapo. Walimu wapo, lakini ule uwezo wao wa kufundisha ndiyo unayumba hapo hapo asilimia 50 mpaka 60. Watavukaje wafike asilimia 80 mwaka 2014 wakati hatuna programu yoyote tuliyoiandaa ili kuwa-*empower* Walimu waweze kufanya kazi zao vizuri! Hatuna mafunzo kama hayo.

Tatizo tulilokuwa nalo Wizara ya Elimu ni kwamba, hakuna mpango wa kuwasaidia Walimu wa Shule za Msingi. Wanapotaka kujiendeleza Walimu hawa Sheria zetu za Ualimu ziko *very rigid,* kama wewe umemaliza darasa la kumi na mbili, basi huwezi kupata *diploma*, ukiwa na cheti chako cha ualimu huwezi kupata *diploma* mpaka uende ukafanye mtihani wa darasa la kumi na nne. Ukimaliza mtihani wa darasa la kumi na nne uende ukasome miaka miwili ya *diploma* ndipo utakapoweza kuipata hiyo *diploma.*

Kwa nini Walimu hawawezi kwenda kama wanavyokwenda Sekta zingine? Wenzetu Madaktari wamejiwekea utaratibu maalum, Madaktari wengi nchini ni wale ambao zamani walikuwa *RMA,* wamemaliza Elimu ya Msingi wakapelekwa kwenda kusoma Udaktari, *Rural Medical Aid (RMA)*, anakwenda kule anasoma kwa muda wa miaka miwili na cheti chake ni kilekile cha darasa la saba, akimaliza miaka yake miwili anarudi kufanya kazi miaka mitatu. Akitoka pale huyu *RMA* anaruhusiwa kwenda kusoma *Medical Assistant*. Hana cheti cha darasa la kumi na mbili, cheti chake ni cha darasa la saba, hatumii cheti cha darasa la kumi na mbili kwenda kusoma *Medical Assistant,* ambayo ni sawasawa na *Diploma*. Akimaliza pale anakuja kufanya kazi. Anakaa miaka yake mitatu huyu *Medical Assistant* anaruhusiwa kwenda kusoma *Assistant Medical Officer* kwa cheti cha darasa la saba. Kwetu sisi Walimu hicho kitu hakipo. Hivi tutaboreshaje Elimu ya Msingi bila ya kuwa na *Diploma* ya Elimu ya Msingi? *(Makofi)*

*[MHE. ABDUL J. MAROMBWA]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Walimu waliomaliza darasa la kumi na mbili tusiwalazimishe wamalize darasa la kumi na nne. Hawa Walimu waliomaliza Elimu ya Msingi wa darasa la kumi na mbili ambao wanafundisha Elimu ya Msingi, tunatakiwa tuwaendeleze ili wapate *Diploma in Primary Education*. Wakipata elimu hiyo, wakirudi kuja kufanya kazi huku mashuleni huku kwetu walikotoka, kwa vyovyote *performance* yao inakuwa kubwa. Asilimia 80 ambayo tunakusudia kwa Taifa letu itafikiwa. *(Makofi)*

Tukiwawekea vikwazo hivi Walimu wetu kwamba wewe huwezi kwenda *diploma* mpaka umalize darasa la kumi na nne, hatutaboresha elimu yetu, tutaididimiza tu elimu yetu hii ya msingi na hatutofikia hiyo asilimia 80. Kwa hiyo, ombi langu ni hilo kwa Wizara, iangalie, iweke utaratibu mpya sasa wa kumuwezesha huyu Mwalimu hata ukiwa na cheti chako tu cha darasa la kumi na mbili, cheti cha ualimu *Grade A*, basi uweze kwenda kusoma bila kufanya mtihani wa *form six* ili uweze kupata *Diploma in Primary Education* hata *Degree in Primary Education* ili akirudi aweze kufanya kazi yake vizuri. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika ukurasa wa 11 nakubaliana na Kamati kwamba, ni vizuri ule mfumo wa zamani ukatumika katika kutoa matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka huu. Mimi nakubaliana na hilo, isipokuwa niongeze; mwaka huu Wizara ya Elimu imefanya jambo jema sana, katika kutoa matokeo ya Elimu ya Msingi, waliweka madaraja pamoja na *marks* zake. Naiomba Wizara ya Elimu kwa mwaka huu tena watakapokuwa wanatoa matokeo ya kidato cha nne, matokeo yale yasiwe ya daraja peke yake, yawe na alama alizozipata ili mwanafunzi huyu anapotaka kwenda kusoma, akisema mimi nimemaliza darasa la kumi na mbili lakini cheti sikupata nimepata *division* yangu sifuri, ukienda kwenye mtandao utaona amepata *division zero*, lakini *point* zake alipata alama ngapi, pengine 28 au 29. Hii itamsaidia hata yule ambaye anataka kumpatia mafunzo kujua huyu ana uwezo kiasi gani. *(Makofi)*

[MHE. ABDUL J. MAROMBWA]

Kwa hiyo, haya matokeo ya mwaka huu kama mlivyoyatoa ya Elimu ya Msingi, basi na Elimu ya Sekondari napendekeza yatolewe hivyo ili kila mtu ajijue. Anapotaka kujiendeleza ajue mimi nitajiendeleza kweli nataka ku-*resit* mtihani wa darasa la kumi na mbili hivi ninaweza ku-*resit* kweli au sina uwezo huo nifanye kitu kingine chochote. Hilo la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kwamba, upande wa Wizara ya Afya kuna vitu vingi sana; kwa mfano, sasa hivi mtu anayesomea *CBG* kwa maana ya *Chemistry, Biology* na *Geography,* haruhusiwi kwenda kujiunga na Udaktari. Lengo letu ni kuongeza idadi ya Madaktari nchini. Sasa kama una lengo la kutaka kuendeleza idadi ya Madaktari, lakini hawa waliosomea kwa mfano, *CBG* hawaruhusiwi sababu zake ni nini? Hivi wale waliosomea *RMA* walisomea *PCB* au *PCM* ambao sasa hivi ni Madaktari wakubwa nchini?

Mimi naiomba Serikali kama kutakuwa na uwezekano waangalie upya, lengo ni kuongeza idadi ya Madaktari. Huyu anayesomea *CBG* ni lazima anasomea na *Mathematics*, ingawa ni *Basic Mathematics*, itamsaidia hii kuweza kufanya kazi yake ya Udaktari. Hebu tuangalie sheria zetu hizi zinasemaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, upande wa mawasiliano *TBC.* Amezungumza vizuri sana Mheshimiwa Mbunge wa Lindi Mjini. Kwa kweli ni aibu, *TBC* haisikiki kabisa, ukienda Wilaya ya Rufiji hakuna hata kijiji kimoja ambacho kinasikia *TBC.* Ukienda Mkoa wa Lindi utakuta ni Mkoa mzima hausikiki *TBC;* tatizo ni nini? Tunaiomba Serikali hii ndiyo redio yenye dhamana, ndiyo yenye kutoa maelekezo sahihi kwa Wananchi wake, iboreshwe ili Wananchi hawa waweze kusikia kinachotendeka katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Mbassa, ajiandae Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar na atamalizia mchana huu Mheshimiwa Makilagi.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika Taarifa zote mbili zilizoletwa mbele yetu leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono Hotuba zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala zima la Walimu. Katika hali iliyopo sasa hivi, niseme wazi sisi tuliotokea mikoa ya pembezoni, imefikia mahala watu wamekata tamaa. Inaonekana kuwa Mwalimu sasa ni adhabu katika maisha. Hii imetokana na sababu za msingi nyingi tu kwa mazingira waliyonayo katika utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu unapofanya kazi yako vizuri, ukatimiza wajibu wako, ni sharti ulipwe kile unachokihitaji au unachokidai kutoka upande wa pili. Suala la madeni imekuwa ni madeni, kila tukiishauri Wizara wanasema tumelipa, lakini ukifika huko migogoro kibao, watu wanadai madeni yao. Sasa hapa kinachoendelea ni nini? Ni wazi kabisa, deni haliwezi kuisha, lakini lipunguzwe, wale wanaodai wapatiwe haki yao waweze kuendelea na kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongelea masuala ya elimu, lakini kuna suala zima ambalo hatujaliongelea kwa ukaribu sana; ni jinsi gani wale ambao wapo nje ya mfumo rasmi wa elimu wanavyoweza kusaidiwa? Tuna hao Walimu ambao walikuwa wanafundisha MEMKWA, haya masuala ya MKEJA. Hawa ukiangalia wanalipwa kiasi kidogo sana sana kulingana na kazi wanayoifanya. Kimsingi, wanajitolea. Inasikitisha sana mtu anayejitolea kwa ujira mdogo anadai mpaka jasho linamtoka. *(Makofi)*

*[MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Biharamulo Magharibi imekuwa ni kero, watu hawa kila siku ni meseji bwana mbona hatulipwi. Inakuwaje, utaratibu ukoje? Hebu Wizara tuangalie kama kweli tulianzisha makundi haya ya elimu nje ya mfumo rasmi kama tunaweza kuyahudumia tuyahudumie kweli na hawa watu wapate stahili zao. Ukifuatilia takwimu, tunayo idadi kubwa ya Watanzania wasiojua kusoma na kuandika na huu ni ukweli. Wapo watu wenye nia ya kutaka angalau wajue tu kuandika na kusoma, lakini leo bado watu wanaojitahidi kuwasaidia hawahudumiwi; hivi tunaendesha Taifa lipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ukiangalia hata haya matokeo ya Darasa la Saba, wapo vijana wengi ambao walikuwa MEMKWA na wamefanya vizuri; lakini ni juhudi ambazo zimekuwa zikifanywa na haya makundi ya wanaosaidia. Hebu naomba turudi tuwasaidie Walimu hawa, tuwalipe posho zao japo kidogo waendelee na kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala zima la *VETA.* Kweli ni nia nzuri ya Serikali kuanzisha Vyuo vya *VETA,* kuweza kutoa stadi na mafunzo kwa Vijana waweze kujiajiri au kuajiriwa. Katika awamu hii, vyuo 25 vimeanzishwa, nashukuru ni hatua, lakini bado kuna makandokando na upungufu sana. Leo hii vyuo vingi ambavyo vimeanzishwa, Tume ilipita kwenda kukagua mazingira yale na kuyaona yakoje na ikahakiki ikatoa kibali kwamba vyuo hivi vianze, lakini bado mambo mengi hayajakamilishwa. Vyuo hivi vimeanza lakini bado unakuta karakana hazijajengwa. Vyuo hivi vimeanzishwa lakini unakuta wanafunzi au wanavyuo wana matatizo ya vitendea kazi na vitendewa kazi. Hebu Wizara ijaribu kukamilisha haya, hata tunakoenda kwenye hatua nyingine ya pili, lakini huku tulikotoka walau tumejenga msingi mzuri na wao wamepata vifaa vya kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine katika Vyuo hivyo vya *VETA* ni jinsi gani Wizara inavyoweza kuvisimamia kwa usimamizi sahihi. Tunajua kuna matatizo ya Walimu au

*[MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA]*

Wakufunzi. Pamoja na nia hiyo nzuri, mkakati ukoje walau wa kila mwaka kuhakikisha hawa waliopo kwanza wanapewa *on job training*. Vilevile kuandaa Walimu wapya kujaza *gap* ambayo ipo kwa ajili ya kukamilisha mitaala inayofundishwa pale. Upande mwingine, usimamizi wa kawaida wa Wakuu wa Vyuo hawa wanafuata kalenda ya vipindi jinsi ilivyo katika vyuo vyao? Sehemu nyingi tumeshuhudia hata Vikao vya Bodi havifanyiki. Inafika mahala chuo kinakwenda tu mwaka unapita. Mkibahatika mkakaa kikao kimoja cha Bodi basi. Sasa sijui kama huo ndiyo utaratibu kwamba, hakuna vikao muhimu na vya kimamlaka ambavyo vinapaswa kukaa? Sielewi, nitaomba nipate ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na uanzishaji wa vyuo mbalimbali mitaani. Unakuta wameweka bango zuri tu tunafundisha sijui Elimu ya Chekechea, Utalii, kusindika vyakula. Ukiangalia hawa watu wamesajiliwa wapi huwezi kupata mamlaka yoyote ya kisheria ambayo inapaswa kusajili walikosajiliwa. Hawa watu wanakwenda mitaani wanakodi nyumba ambazo ukiziangalia hazina kiwango cha kukidhi kuwa chuo. Mazingira ambayo ni hatarishi kwa watoto wetu. Wanawatoza fedha nyingi sana wazazi na inafika mahala wanasema sisi hapa mtoto akishahitimu tunamtafutia kazi. Sasa kazi ijulikane kwanza ni *level* ipi ya cheti inayotolewa pale. Mazingira magumu.

Mimi naomba tafadhali, Wananchi wamechoka kuibiwa na kutapeliwa. Leo hii wanashindwa kugharimia elimu hii ya kawaida ya msingi, mzazi amejitahidi amefika huko mtoto ndiyo hiyo bahati mbaya labda kapata alama ambazo haziridhishi afanyeje, basi ngoja ampeleke upande wa pili. Anampeleka kule nako kumbe ni majanga anaenda kuibiwa tena. Ninaomba usimamizi wa vyuo hivi uwe wa makini sana, vikaguliwe na kabla ya kuruhusu kuanza kuwe na mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende upande wa afya. Tumeongelea masuala mengi sana katika Wizara yetu ya Afya na Ustawi wa Jamii, lakini suala kubwa ni kutotimiza

*[MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA]*
lile Azimio la Abuja. Kama leo hii tungekuwa tunapata ile asilimia 15, nafikiri mambo yote yangekwenda vizuri. Tujifunze mazuri kutoka kwa wenzetu. Kenya wamefanya limekuwa suala la kisheria na la kikatiba, wanapata asilimia 15, leo hii wanakwenda vizuri, japo si kwa asilimia zote lakini walau wamepunguza haya matatizo.

Tumekuwa na mambo mengi sana lakini tunasahau kwamba, ili kila kitu kiende vizuri lazima uwe na afya njema. Bila afya njema haliendi lolote hapa. Naomba sasa tulifanye suala hili lirudi liwe la Kikatiba, tupate asilimia 15 tupunguze matatizo ya vifo vya akina mama na watoto na matatizo yote yaliyopo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala zima la wazee. Tuna kambi nyingi sana za kutunza wazee wasiojiweza. Ieleweke kabisa kwamba, kila mmoja wetu hapa Mwenyezi Mungu akimjalia lazima ataifikia hatua ya uzee na kuwa mzee siyo dhambi. Leo hii nitolee mfano mmoja tu hapa Sukamahela Manyoni, unakuta wale wazee wamekaa pale wanapigwa na jua, wameumia, wamechoka, hawajiwezi taabani. Ukiangalia makazi yao wanapoishi tabu. Ukiangalia chakula wanachopata shida. Leo hii tunashukuru sana labda Kambi ya Masista pale wanaowasaidia wale wazee. Serikali iko wapi? Hawa wazee wako wapi? Wanasaidiwaje? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isifike mahala sasa kuwa mzee ikawa ni laana au ikawa ni tabu ndani ya nchi hii. Hebu tuwajengee mazingira mazuri, tuwaone kana kwamba waliyoyatenda ndiyo yametusaidia sisi kufika hatua hii. Wametoa mchango mkubwa sana na mzuri sana ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na suala zima la usimamizi wa huduma ya afya. Kuna mambo mengi sana ambayo yanajitokeza kiutendaji, lakini naamini kabisa kukiwa na mfumo mzuri wa usimamizi wa shughuli za afya, mambo yote yatakwenda vizuri. Tunalalamikia upotevu wa dawa, ukosefu wa Watumishi, mazingira mabovu, lakini

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



kama kungekuwa na timu za usimamizi kutoka ngazi ya Wizara kuja ngazi ya Mkoa, Mkoa kwenda ngazi ya Wilaya, ninaamini hata huko kwenye vituo kungekuwa kumekaa vizuri. Hebu leo hii tuombe Wataalam hawa, Kamati hizi, wahusika wasikae ofisini, wateremke wakaangalie haya matatizo. Mengine ni matatizo madogo tu, ambayo kimsingi, Kamati ikifika ikaona, ikashauri na ikaelekeza, siku nyingine wakirudi wanaanza na tatizo lingine siyo hilo tena.

Kumekuwepo na matatizo ya hizi Kamati kutokufanya kazi na ndiyo maana tunaona utitiri wa vituo vinavyoanzishwa vya kutoa huduma ambavyo havina sifa. Tunasubiri Timu ya Wizara ndiyo iteremke na ile rangi yao nyekundu wakaandike kwenye zile kuta. Kamati za Usimamizi za Wilaya ziko wapi? Kamati za Usimamizi za Mikoa ziko wapi mpaka ifikie hatua hiyo ni Wananchi wangapi ambao wameshapata huduma ambayo ni mbovu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanafanyika kwa sababu Kamati hizi zimelala hazitaki kufanya kazi. Mimi naomba Kamati hizi hebu teremkeni mkatekeleze majukumu yenu. Msimamie inavyopasa kuwa na ninajua matatizo mengine haya yatakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa suala moja tu ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, ajiandae Mheshimiwa Makilagi.

**MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupata nafasi hii. Vilevile naunga mkono Hotuba zote mbili zilizotolewa leo asubuhi.

Nitakwenda moja kwa moja katika Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake. Mfuko huu unalenga kutoa mkopo wa masharti nafuu kwa akina mama. Vilevile

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



kuongeza ajira na kuwainua kimaisha. Katika Mfuko huu Halmashauri inatakiwa itoe asilimia tano ya mapato yake. Kwa bajeti ya mwaka 2013/2014, Serikali imekubali kutoa bilioni mbili. Kwa hiyo, sasa ni kazi yetu sisi Wabunge kuhakikisha Halmashauri zinatoa asilimia tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo hii imeanza kutoka toka mwaka 2002 na ilipofika mwaka 2013, jumla ya mikopo iliyotolewa kwa akina mama ni shilingi milioni 960. Kwa bahati mbaya mikopo hii hairejeshwi kwa wakati na rekodi ni mbaya. Mpaka kufikia mwaka huu, jumla ya pesa zilizorejeshwa ni shilingi 257,831,893. Hiyo ni sawasawa na asilimia 27. Zaidi ya shilingi milioni 700 bado mpaka leo hazijarejeshwa, sawa na asilimia tatu. Kwa hiyo, nafikiri juzi hapa Waheshimiwa Wabunge wengi tulikuwa tukiwaoneshea vidole Mawaziri. Leo nafikiri vidole vile vinarudi kwetu, kwa sababu sisi wengi hapa au sote ni Madiwani na sote tunatakiwa tusimamie Mfuko huu. Kwa bahati mbaya sana, kazi hiyo hatuifanyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo Ripoti hapa mkononi kwangu na nitasoma baadhi ya Mikoa na Halmashauri ambayo haikufanya vizuri kabisa. Nitaanza na mikoa ambayo imefanya vibaya. Mkoa wa kwanza ni Rukwa. Rukwa hawajarejesha hata senti moja mpaka sasa hivi, umepewa jumla ya shilingi milioni 24 na hakuna kilichorudi. Kwa maneno mengine, hakuna pesa zilizorudi wakapewa watu wengine zikazunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa mwingine ni Mkoa wa wa Manyara. Mkoa wa Manyara walipewa shilingi milioni 44 na mpaka sasa wamerejesha shilingi 2,200,000 basi, bado wanadaiwa shilingi milioni 41. Ina maana pesa nyingine zipo mikononi akina mama hawajarejesha, kwa hiyo, wengine hawapati. Hiyo ni baadhi tu ya Mikoa ambayo imefanya vibaya, lakini ni karibu yote imefanya vibaya ila imezidiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa ambao umefanya vizuri kuliko yote, ningependa kuutaja ni Mkoa wa Geita.

*[MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR]*
Mkoa wa Geita umelipa pesa zote na sasa hivi pesa zile zimeanza kurejea. Iliposomwa Taarifa hii kwenye Kamati, nikaahidi kwamba, nitakuja katika Bunge kulieleza ili na sisi tushughulikie katika Halmashauri zetu. Twende katika Halmashauri tusimamie, tuhakikishe pesa hizi zinarudi na wengine wanafaidika kupata mikopo. Kama hatukufanya hivyo, ina maana hizi shilingi bilioni mbili ambazo zitatolewa na Serikali, zitakuwa ndiyo hivyohivyo, mikopo itakwenda kule na baadaye pesa hazitarudi na wengine hawatapata. *(Makofi)*

Kadhalika, nilimwomba Mheshimiwa Waziri, Ripoti hii vilevile aisambaze kwa Waheshimiwa Wabunge, kila Mbunge awe nayo, aende katika Halmashauri zake na kuhakikisha pesa hizi zinarudi na zinazunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninalotaka kulizungumzia ni kuhusu *TBC. TBC* inamiliki Redio tatu na TV mbili. Ina miaka mingi sana ya matatizo, mitambo imeshazeeka sana na kwa hiyo, mara nyingi hatupati matangazo ya redio na TV kwa uhakika. Katika mwaka huu wa 2013/2014, Serikali imepanga kutoa shilingi bilioni sita ili kulipa Shirika hili liweze kuboresha mitambo na vifaa vinginevyo. Hivi sasa nafikiri wameshaanza kazi nzuri ya kununua Redio za FM tisa, kuubadilisha mtambo ule analojia ulioko Makao Makuu kuwa dijitali na vilevile mitambo mitano ya Redio FM ambayo ipo mabondeni sasa hivi itawekwa sehemu ya miinuko. Mategemeo ni kwamba, baadaye hali itaboreka na kwa kweli imeshaanza kuboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC* wana matatizo mengi sana. Moja ya tatizo lao ni kwamba, wanadaiwa sana. Wanadaiwa zaidi ya bilioni mbili na watoa huduma mbalimbali. Kuna watoa huduma wa ndani ya nchi na wengine nje ya nchi. Vilevile kuna watoa huduma wa *satelite* wa nje ambao mpaka sasa hivi deni lao halijalipwa. Kwa hiyo, wakati wowote pengine matangazo ya TV yanaweza yakakatwa kutokana na kutolipwa madeni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika, *TBC* inadai madeni mengi vilevile. Ina wadaiwa sugu wengi inawadai na mpaka sasa hivi pesa zile hazijalipwa. Serikali inadaiwa na kuna Taasisi za Serikali zinadaiwa na kadhalika Taasisi za Binafsi zinadaiwa. Katika Bajeti iliyopita, tulisema hapa kwamba, wale wote ambao wanadaiwa, basi Serikali ichukue hatua ya kuwakata katika bajeti zao ili Shirika hili liweze kwenda vizuri. Kwa nia kwamba, baadaye iweze kufanya biashara vizuri na kuboresha mzigo mkubwa huu wa Serikali wa kutoa kila mwaka pesa chungu nzima. Tunaiomba tena Serikali iliangalie suala hili, ifuatilie madeni ambayo inadaiwa ili iilipe *TBC* na iweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia mpaka hapo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Makilagi, ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kutoa machache ambayo nimejiandaa kuzungumza kwa siku ya leo. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu, muweza wa yote, kwa kunipa fursa kuweza kusimama kutoa mchango wangu katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na utangulizi kwa kusema kwamba, ninawashukuru sana Wanawake wa Tanzania kuendelea kuniamini kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa Tanzania kwa kipindi kingine cha miaka mitano kwa kura zote za Ndio na kwa kweli haikuwepo kura ya Hapana. Kitu ambacho ninaweza kuwathibitishia ni kuwaambia kwamba, imani huzaa imani, nitaendelea kufanya kazi zangu kwa ufanisi na kwa uadilifu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya utangulizi huo, naomba sasa na mimi niungane na wenzangu kuunga mkono hoja zote mbili zilizoletwa na Kamati zote mbili; ya

*[MHE. AMINA N. MAKILAGI]*
Kamati ya Huduma za Jamii na Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Nampongeza sana Mama Sitta na Mama Jenista Mhagama na Timu yake, waliofanya kazi nzuri sana ya kuchambua na kutoa maoni mazuri sana, ambayo nafikiri kama Serikali itayasikia, yatasaidia sana kuboresha huduma hizi za jamii na huduma ya maendeleo ya jamii, jinsia na watoto. *(Makofi)*

Yote yaliyopendekezwa humu naomba niungane nayo, lakini naiomba Serikali kupitia Wizara zote tatu, tena zote kwa asilimia zaidi ya 80 zinaongozwa na Wanawake; Dkt. Fenella, Mama Sophia Simba, Mama Kabaka na kaka yangu Shukuru Kawambwa; maoni yaliyoko kwenye hizi Taarifa myaangalie na myafanyie kazi kwa sababu ni maoni yenye tija, hongereni sana Wenyeviti Wanawake mnaweza na Mungu awatie nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya utangulizi huo, sasa naomba nianze na Sekta ya Afya. Naomba niungane na wote walioongea na hasa Mheshmiwa Mbassa, amemalizia kwa kusema kwamba, Azimio la Abuja litekelezwe. Azimio la Abuja likitekelezwa, changamoto zote tunazoziona katika Sekta ya Afya zitaondoka tena kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu Sekta ya Afya ndiyo roho ya nchi yetu. Bila afya hakuna kilimo, bila afya hakuna uzalishaji wa uchumi, bila afya hakuna chochote. Sekta hii siku hadi siku tumekuwa tukiona jinsi ambavyo fedha zake ni chache. Kitu ambacho kimepelekea tunashindwa sasa kujenga zahanati katika kila Kijiji kama tulivyokusudia, tunashindwa kujenga Kituo cha Afya kama tulivyopanga, tunashindwa kupeleka Wataalam katika vituo vyetu na zahanati zetu kama tulivyokusudia. Katika hospitali zetu, tunashindwa kuboresha masilahi ya Wafanyakazi, tunashindwa kuboresha huduma zote, madawa na kulipa hata deni la *MSD.*

*[MHE. AMINA N. MAKILAGI]*

Naomba sana hebu Serikali ithubutu katika bajeti inayokuja na siyo kusubiri bajeti peke yake, tuthubutu tufanye hata maarifa ya ziada. Kwa sababu hivi karibuni nilikuwa Igunga, nimetembelea Kijiji kinaitwa Miti Mitano, hivi karibuni nilikuwa Ruvuma kule Nakapanya, nimekwenda Njombe, nimekwenda Ludewa kwa Mheshimiwa Filikunjombe, nimeongea na Wananchi, nilikuwa nawauliza maswali hebu niambieni kero zenu; Wananchi wanatambua kazi nzuri sana inayofanywa na Serikali ya CCM. Wananchi wamenituma nije niseme ahsante kwa Chama cha Mapinduzi kwa kutekeleza Ilani kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya mengi, imejenga barabara kila pahala na hakuna ambaye anabisha. Serikali imeboresha huduma mbalimbali, lakini Wananchi wananiambia mambo mawili, Maji na Sekta ya Afya. Wanalalamikia vituo vya afya vipo mbali na watu wanakoishi. Naomba niishauri Serikali, suala la ujenzi wa zahanati katika kila Kijiji, suala la ujenzi wa kituo cha afya katika kila Kata, hatuwezi kuwaachia Halmashauri peke yao. Tukiwaachia Halmashauri waweke vipaumbele katika bajeti zao, hatutafika popote. Ninaomba uwekwe msukumo litolewe agizo suala la ujenzi wa Zahanati katika kila Kijiji na kila Kata liwe ni jambo la lazima. Hapo nilipokuwa napatolea mfano, Miti Mitano, nimekuta wanawake wanatembea kilometa 20 kwenda kufuata huduma ya kupima mtoto na mama mjamzito. Mwanamke anaumwa uchungu usiku anakwenda kutembea kilometa 20, wanafia njiani. Tusiachie Halmashauri. Naomba sana hapa Azimio la Abuja likitekelezwa zahanati zitajengwa, Vituo vya Afya vitajengwa na lengo letu litaweza kufikiwa kama ambavyo Ilani ya CCM imetamka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Wataalam katika vituo vya afya ni kero sugu. Katika kilio walichonipa Wananchi maana hapa nazungumza natokea Jimboni kwangu, Jimbo langu mimi ni Tanzania nzima ndiyo wananchi walionichagua. Nafasi yangu inatokana na idadi ya kura za Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na ninapigiwa kura na Watanzania wote. Kwa hiyo, Jimbo langu ni Tanzania

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



nzima, nimetembelea Majimbo yote kabla ya kuja hapa. Kero ya Wananchi waliyonituma nije nizungumze hapa ni suala la Wataalam katika Vituo vya Afya.

Serikali imefanya kazi nzuri, imejenga Zahanati kila pahala, mfano ni Jimbo la Igunga. Igunga wamejenga Vituo vya Afya vingi iwezekanavyo Urambo. Urambo wamejenga mpaka na Kituo cha Mama Ngojea chini ya Mama Sitta na wenzake. Nimekuta zahanati zaidi ya 54 hazijafunguliwa. Tatizo nini? Hakuna Wataalam, hakuna nyumba za Waganga. Shida ni nini? Tunasubiri Halmashauri ndiyo ijenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, hatuwezi kuwaachia Halmashauri ya Igunga na maeneo mengine wakatujengea nyumba za Waganga na wakatuletea Wataalam katika maeneo yetu. Ninaomba hebu tujielekeze sasa katika kutengeneza utaratibu mpya. Maana huu wa kusubiriana kutokea sijui vijana watoke katika vyuo vyao umeshindikana. Hebu tutafute, wakati ule tulikuwa na wakunga wa jadi wanapewa mafunzo ya muda mfupi. Tuwaandae vijana sasa. Sasa hivi Tanzania tuna wasomi wengi wamemaliza vyuo vikuu wamekaa. Tuwape mafunzo ya muda mfupi, tuwafundishe hata namna ya kupima malaria katika vituo vyetu, namna ya kupima akina mama wajawazito pale, kupima watoto, maana unakuta hata huduma ya kupima mtoto eti hakuna Mtaalam katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba huu utaratibu tukae chini na ikiwezekana tuunde *Task Force* ikae chini, tuangalie hivi huu utaratibu wa kukaa kusubiria hao Wataalam waliobobea hatutawapata. Igunga wanasema wapo pale, zahanati zimekamilika hawana Wataalam. Masharti yaliyowekwa katika uanzishaji wa hivi Vituo vya Afya na zahanati ni magumu pia. Wananchi wakati wanahamasishwa wameambiwa jengeni zahanati, jengeni kituo cha afya, wamekamilisha wanasubiri kituo kifunguliwe.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru.

**MHE. AMINA NASSOR MAKILAGI:** Hiyo ni ya kwanza Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunilinda, naona unataka kunipunja lakini nakupenda sana ahsante. Utanilinda na huu muda wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasisitiza hapa suala la huduma ya afya. Nazungumza kwa uchungu, kwa sababu waathirika wakubwa ni wanawake na watoto. Hata huyo baba anayeumwa anategemea apelekwe na mke wake hospitali. Mtoto anayeumwa anatakiwa apelekwe na mama. Kutembea masafa ni mwanamke ndiye anayejua. Adha wanaipata akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ndiyo ujumbe walionituma nije niwasemee hapa, naomba sana Serikali ithubutu na ninajua Serikali yetu ikiamua inaweza. Kama tumeweza kujenga barabara kilometa na kilometa, kama tunapeleka maji kila pahala, Miradi mikubwa mikubwa ikiwemo Kashuwasa, Dar es Salaam tunaboresha, tutashindwaje kupeleka vitu vidogovidogo katika maeneo yetu ndugu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kwa kweli naendelea kuipongeza Serikali, kwa kazi nzuri sana inayoifanya, kuwezesha Wanawake na Vijana kiuchumi. Naipongeza sana Serikali kwa kazi waliyoifanya nzuri ya kuimarisha huu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana. Kutenga shilingi bilioni 6.1 kwa ajili ya Vijana na shilingi bilioni mbili kwa ajili ya Wanawake. Ombi langu, ninataka niulize na swali hapahapa; hizi fedha ziko wapi? Ni ngapi zimeshatengwa? Zimeshapelekwa wapi? Zipo katika

Halmashauri ipi? Na utaratibu wa kuzipata ukoje? Maana nimekwenda huko, Wanawake hawajui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kubwa la huu Mfuko wa Wanawake, hii shilingi bilioni mbili mliyotutengea haitoshi. Nafurahi sana, Naibu Waziri wa Fedha mko hapa tena bahati nzuri Wanawake wawili, haitoshi bilioni mbili kwa vikundi nilivyoviona vya *VICOBA, HISA* na vikundi vya ujasiriamali, wanawake wameamua na ndiyo wanaolea Taifa. Ninaomba hebu jielekezeni kuongeza fedha. Kama za Vijana zimepatikana shilingi bilioni sita na Wanawake zifike mwaka huu shilingi bilioni sita na ikiwezekana bajeti ijayo zote tuzipaishe Vijana shilingi bilioni kumi, Wanawake shilingi bilioni kumi, watu waendelee; kwa sababu Vijana wamesoma, wapo tayari, nimeona mfano mdogo pale Igunga. Vijana wamewezeshwa wameingia kwenye Sekta ya Kilimo, ni wasomi wale wanafanya kazi vizuri na hakuna manung'uniko. Ninaomba huu Mfuko uongezwe.

Ombi langu kwenye hii Wizara ya Maendeleo ya Jamii; hivi kwa nini inakuwa Wizara yatima? Wizara Mtambuka, Wizara ambayo bila Wizara hii mambo hakuna, lakini ni Wizara maskini kuliko Wizara yoyote. Waziri mwenyewe anatembelea gari la Nissan, ndiyo Waziri pekee anayetembelea Nissan Patrol. Nimekwenda kwenye mikoa mbalimbali, nimeonana na Mabibi Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; hata fedha ya kumfikisha kwenye kijiji hana, mafuta kwenye pikipiki hana, gari lake hawampi. Pikipiki mbovu ndiyo wanampa Bibi Maendeleo ya Jamii. Kwa hiyo, matokeo yake, haya maelezo aliyoyatoa hapa Mjumbe kwamba, fedha za Mifuko ya Wanawake na Vijana hazirejeshwi ni kwa sababu hawa Wanawake na Vijana hawana hata elimu ya namna ya kuendesha ushirika. Hawajui hata huu mkopo unatakiwa urejeshwe. Ninaomba Wizara hii tuiangalie ili Mabibi Maendeleo wetu walioko kule waweze kufanya kazi kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niulize hii Sheria ya Ndoa inakuja lini maana tusije tukadanganyana hapa kwamba tunasubiri Katiba, haihusiani na Katiba? Hii Sheria

ilitungwa na Bunge tunaitaka hapa ije. Sheria inayoruhusu Mtoto kuolewa kabla ya miaka 18. Sheria ya Mirathi na sheria zingine zije hapa tupitishe. Msije mkazungumzia Katiba inakuja kumbe Katiba haihusiani, hii sheria ilitungwa hapa. Nataka kujua imefikia wapi maana kila wakati tunaahidiwa kwamba sheria inakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa elimu, naomba kwanza niwapongeze sana Walimu wetu Tanzania, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwalea watoto wetu. Ninaomba masilahi yao yaboreshwe kwa sababu Walimu wana madai ya uhamisho na wana madai ya malimbikizo ya madeni yao ya kupandishwa madaraka. Walimu wana changamoto za nyumba za kuishi, Walimu ndiyo kila kitu, naomba tuwaangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Makilagi, mchango wako umekuwa mzuri sana.

Waheshimiwa Wabunge, kipindi chetu cha asubuhi kimeishia sasa. Jioni tutakuwa na wachangiaji wanne tu, akianza Mheshimiwa Kibona na wale watatu watatangazwa baada ya Mheshimiwa Kibona kupata nafasi. Serikali itaanza kutoa mchango wake saa kumi na mbili kasorobo, itapata muda wa saa moja na wahusika wote wameshapewa taarifa za michango yao.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.57 mchana Bunge lilifungwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo tuna Taarifa mbili za Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii na Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, mjadala unaendelea. Nitapata wachangiaji wachache tu jioni hii. Mheshimiwa Aliko Kibona!

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja zilizopo mbele yetu; Hoja ya Maendeleo ya Jamii na Huduma za Jamii.

Kwanza, nachukua nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti na Wajumbe wote wa Kamati hizi, kwa kazi nzuri waliyoifanya Na kututayarishia Taarifa nzuri. Kwa kuwa muda ni mfupi, naomba niende moja kwa moja kuchangia baadhi ya maeneo niliyoyaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Hifadhi za Jamii; nizungumzie kidogo kuhusu nililoliona katika nchi hii kwa upande wa Jeshi letu la Polisi. Nimeambiwa Jeshi letu la Polisi, Mfanyakazi au Mtumishi wa Jeshi la Polisi anakuwa *pensionable* baada ya miaka 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni sheria zilizopitwa na wakati, ambazo Wabunge wamezisemea hapa Bungeni, wakilaani Watendaji katika kitengo hiki cha uandaaji na kuangalia sheria zilizopitwa na wakati; ni sheria kandamizi, ni sheria zinazokiuka haki za binadamu; kwa kweli ni sheria ambazo zimepitwa na wakati. Haiwezekani Mtumishi akae miaka 12 ndipo awe *pensionable*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wenzangu wa Kamati hizi ambazo zinaangalia jambo hili, zilichukue jambo hilo na pengine tusikie kidogo maelezo kutoka kwa Waziri anayehusika, ni kitu gani ambacho kinafanya wang'anga'nie sheria iliyopitwa na wakati?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Nadhani ni moja ya zile sheria za mwaka 42 ambazo tulikuwa tunajadili Sheria ya *GEPF* tumeibadilisha juzi, pengine na hii inaingia huko. Maana ni sheria ambazo wale wengine wenzangu wanaojua kusema, huwa wanaingiza na maneno ambayo yana ukakasi, lakini mimi naogopa kusema. Niseme tu kwamba, wahusika waliangalie hili, ndugu zetu wa Jeshi la Polisi wapate haki yao, wapate pensheni. Wanapoajiriwa waanze kukatwa na kuwa *pensionable* moja kwa moja kama Watumishi wengine wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pensheni ya Wazee; mimi nimeshangaa kidogo, hii imeonesha jinsi gani sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge pengine tusivyokuwa makini. Mwaka jana nimesikia sisi Wabunge tulipiga kelele sana tukizungumza habari za *withdraw* iendelee. Mimi niseme kwamba, naishukuru Kamati kwa utafiti iliyoufanya, kwa kutembelea nchi mbalimbali na kujua katika mfumo wa Hifadhi ya Jamii, hakuna kitu kinaitwa *withdraw*.

Leo tunazungumza kwamba, wazee wetu walipwe pensheni. Leo hii sisi tuliopo hapa ni wazee wa kesho, kama tutakuwa na pesa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii tukachukua, halafu baada ya kuzeeka tukataka tena tulipwe pensheni; hii haitawezekana.

Kwa hiyo, naishukuru Kamati imetengeneza utaratibu mzuri, naomba likae vizuri, tulijadili tuliweke vizuri. Kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, siyo kwamba kwa sababu haturuhusu *withdraw*, kwa hiyo, wanachama wateseke. Narudia tena kama nilivyosema, waangalie, wawe wabunifu, kama mtu amekosa ada ya mtoto wake kujisajili kusoma Chuo Kikuu, amekosa mkopo, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iingilie kati, *cheque* iandikwe iende kwenye chuo husika, mtoto wa mwanachama husika asome kama kawaida. Kwa njia hiyo, hakuna mtu atakayetamani kuji-*withdraw* katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze kidogo kuhusu Walimu. Mwenzangu mmoja asubuhi amechangia vizuri, mimi nimefurahi. Walimu waliopo sasa hivi na wengine

wanakaribia kustaafu, ndiyo waliotufikisha hapa, wengine walikuwa darasa la saba. Ninao wenzangu wengi niliosoma nao *Form I*, yuko Dkt. Mahenge hapa ni shahidi yangu, tumeanza naye *Form I.* Yuko mwenzangu Mheshimiwa Dkt. Tizeba pale, tumeanza naye *Form I,* lakini ni matunda ya Walimu waliokuwa *UPE* Darasa la Saba. Haiwezekani kwa sasa tuanze kuwabeza, tunawasumbua, mara ooh ukawe *Form IV,* ukasome. Ndugu zangu, kusoma ni kazi ngumu, hebu hawa wazee tuwaruhusu waendelee kujiendeleza wakiwa na vyeti vilevile vya darasa la saba. Kwanza, walio wengi ni wazuri kuliko hata wa *Form IV. (Makofi)*

Mimi najivunia Walimu hawa, wazee hawa wa zamani wamenifikisha hapa na wenzangu hawa ambao nimewataja na pengine wapo wengi hapa ndani. Kwa hiyo, hawa Walimu wasisumbuliwe, waenziwe. Kama mtu ana haja ya kujiendeleza, mfumo ule ule tena nasikia hata kwa Waganga wameanza kuleta chokochoko. Wale Waganga ambao wametuhudumia vizuri wakiwa darasa la saba ambao wamekwenda kusoma *RMA,* tusiwaingilie na kuwasumbua. Waendelee kupanda ngazi. Kama mtu anataka akajisomee, kwanza, wakifika vyuoni wanawashinda hata *Form VI. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuwe waangalifu, hawa wasomi wengine wanaingia huko maofisini, mambo wanayoanza kuyapanga ndiyo yanayoturudisha nyuma, ndiyo yanayotuletea matatizo katika utendaji Serikalini.

Wenzangu wengine tulikuwa na mjadala juzi hapa wa pesa za Serikali za Mitaa wakasema Waziri ajiuzulu, Waziri Mkuu ajiuzulu, Mawaziri wajiuzulu na kadhalika. Mimi nasema ndugu zangu tusikimbilie huko. Ukiwa na mtoto ameenda shuleni *Form I,* baada ya miezi sita akirudi amekonda, amedhoofu, fanya utafiti badala ya kumhamisha shule au kumwachisha.

Tatizo lililopo, pamoja na haya niliyoyasema hapa, ni mfumo katika Serikali yetu. Hivi wewe hapo unayesema Waziri Hawa Ghasia ajiuzulu, tukisema kwa mfumo huu huu

tukupe wewe tuendelee na mfumo huu huu utaweza? Ndugu zangu naomba wahusika waangalie sheria zilizopo, waangalie mfumo tulionao, huu ndiyo unatufanya tupige kelele hapa ndani, siku ya siku tutaanza kuparuana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa Watumishi wa Afya; wapo Watumishi waliosoma vyuo mbalimbali. Sijajua hivi vyuo nani alivisajili kule Mbeya vipo Vyuo vya Chimala na sehemu zingine? Watoto wanasoma pale miaka miwili au mitatu, wakirudi wakienda kuomba kazi wanaambiwa chuo hiki hakitambuliki, lakini mzazi amelipa ada miaka mitatu kama alivyosema mwenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitaka huu Mpango wa MMEM ukamilike, hebu twende na mpango wa hao watu ambao wamesoma hata vyeti vya chini, mradi wanajua kugawa asprin na kadhalika. Kwa sababu kuna maeneo mengine hatujafungua hospitali, lakini unaweza kushangaa wapo Vijana waliosoma miaka miwili au mitatu kwenye vyuo mbalimbali, wanaweza kufanya kazi hizi. Hebu tuangalie, tu-*screen*, kama ikiwezekana tuweze kuwaajiri hawa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye lugha. Hivi lugha yetu ni ipi mpaka sasa hivi? Wenzetu wa Huduma za Jamii mtuambie lugha yetu ni ipi ambayo watoto wetu sasa wanafundishia? Ukiwa Profesa, ukiwa Daktari, vyovyote vile ukiwa na *Master;* mimi nikikuuliza kwa lugha ya mama yangu, nikasema miguu ya kuku miwili ongeza miguu ya bata miwili jumla ni mingapi; hata ukiwa Profesa utajibu swali hilo. Hayo ndiyo maswali tunayowauliza Vijana wetu wa *Form IV* kwenye mitihani yao. Matokeo yake, kwa sababu hawana msingi wa lugha ile ya Kiingereza, wengi wana akili nzuri tu, tukiwauliza maswali yale kwa Kiswahili, wanaweza kufanya vizuri. Kwa kuwa msingi wa lugha sisi wenyewe tunajikanganya, hatuna msimamo thabiti, watoto wetu wanafeli mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, yalikuwepo mengi ya kuongea, lakini naunga mkono hoja. Ndugu zetu wa Jeshi

*[MHE. ALIKO N. KIBONA]*
la Polisi watazamwe kwa jicho la huruma na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Aliko Kibona. Anayefuata ni Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Lusinde ajiandae!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii. Nami pia nazipongeza Kamati zote mbili kwa kazi kubwa ambazo wamezifanya. Pamoja na michango mikubwa ambayo mlijaribu kuishauri Serikali, lakini nataka nitoe ushauri wangu kwa ujumla.

Taifa letu tuna changamoto nyingi ambazo zinatukabili kama Taifa. Kamati hizi mbili ni Kamati mtambuka ambazo zinatakiwa zipewe umuhimu wake, kwa sababu ndiyo zinali-*shape* Taifa. Kama Taifa tunajua tunataka twende wapi. Kamati zote mbili, kwa mawazo yangu naona kama zinashughulikia sana eneo la juu, hatuanzi na chini. Kwa hiyo, Taifa letu ili tupate Taifa zuri ambalo ni zalendo na lenye afya nzuri, ni lazima tuanzie huku chini kwenye ngazi ya familia.

Mimi ningeomba nishauri kwa ujumla kwamba, ili tuwe na *strong societies* ni lazima tuwe na *strong families*. Sasa katika mipango yote hii, naishauri Serikali, maana sijaona, mambo mengi yanazungumzwa, mambo ya shule ambayo tumeyazungumza mpaka hata kwenye Wizara ya Elimu yamezungumzwa, lakini tusipokuwa na *strong families* ambazo zinaanza nyumbani, hatuwezi kuwa na *society* yenye nguvu. Ukiwa na baba dhaifu, utakuwa na familia dhaifu na ukiwa na familia dhaifu, utakuwa na mtaa dhaifu. Mwisho wake Vijiji dhaifu, hatimaye Wilaya dhaifu, Mkoa dhaifu na Taifa dhaifu.

Kwa bahati mbaya sana, tunafundishana haya masomo ya darasani ambayo siyo mabaya, lakini hatufundishani huku chini ambako lazima tuwajenge

watoto wetu. Tumekuwa na wazazi wengi ambao hawawajibiki na familia zao, tumekuwa na akina mama wengi ambao hawawajibiki na familia zao. Unaweza ukawa na *Ph.D,* unaweza ukawa umesoma, lakini kama familia zetu hazijaanza ndani, hatuna *responsible fathers,* hatuna *responsible mothers,* hatuwezi kuwa na Taifa zuri. Mfano mzuri ambao tunaweza tukajiuliza wote kwa pamoja; *why do we build strong houses but we fail to build strong homes?*

Tunajenga majumba makubwa sana, lakini hatujengi makazi mazuri, ambapo watoto wetu tunaowaandaa lazima wakae kwenye makazi mazuri, ambapo akina baba na akina mama wanaandaa familia hizo. Taifa tunaloishi kwa sasa hivi, watu wana changamoto nyingi sana, watu wako *stressed,* kuna *domestic violets*, wengine wako *depressed* na wengine wana *trauma. Solution* gani ambayo Serikali au Wizara hizi inatoa kwa watu kama hao ambao wako *stressed*, wako *depressed*? Unaweza ukakuta hapa Bunge tumekaa tuna migandamizo mingi sana. Huduma kama hizi, kwa mfano, mtu ana *stress* anataka asaidiwe hata hapa hapa Bungeni anazipata wapi? Hii changamoto kubwa duniani kote, ili tuwe na familia nzuri ni lazima tuanzie nyumbani.

Sasa ningeomba hii, pamoja na kwamba, tunashughulikia na masomo makubwa ambayo ni vizuri wakasoma na Kamati zote zimeshauri, lakini huku mwanzo ambako watu kwenye familia moja moja hawapati hii misaada inakuwa ni tabu. Kwa mfano, kule Iringa Chuo cha Tumaini kina *Faculty* ya *Councelling,* lakini sijaona juhudi za makusudi ambazo Serikali inaandaa hao watu kama ambavyo tunaandaa Mabibi Shamba na Mabibi Maendeleo. Katika mitaa yetu, kuna watu wana shida nyingi sana, watu wanaugulia wengi, wengine wameumizwa, wamekuwa *abused.* Ili tuwe na familia nzuri tujenge Taifa letu, lazima hizi huduma zitolewe katika maeneo tunayotoka.

Wenzangu wamezungumza hizo *solution* walizo-*offer.*

*[MHE. MCH. PETER S. MSIGWA]*

Juzi nilipozungumza hapa kwamba ni lazima tutoe *solution* inayohusiana na tatizo tulilonalo. Kweli kuna watu wengine tunatakiwa tutoe *solution* za matatizo ya kielimu na kiufahamu, lakini kuna watu wengine wanahitaji *spiritual healing*, watu wengine wanahitaji *spiritual councelling*. Ni namna gani hizi Wizara zina maingiliano na watu wa Misikitini, watu wa Makanisani; watu ambao wanaweza wakasaidia kuhakikisha wanatoa migandamizo ambayo watu wanayo?

Nimeuliza swali moja hapa kwamba; *why do we build strong houses*? Watu wamejenga majumba makubwa, lakini kwao hakuna raha, wana ugomvi. Wanasiasa wengi wanaoongoza *they have nice houses, but they don't have nice homes.* Hawawezi kukaa na familia zao. Leo naongea Kichungaji kidogo, naomba mnisikilize. *(Kicheko/Makofi)*

Hebu tujiulize kama Wabunge ambao tunatakiwa tutoe mifano ambayo ni kielelezo vizuri kwamba tunapoongoza Taifa ili tuwe na Taifa zuri tusiwe na machokoraa mitaani, tusiwe na wezi, sisi wenyewe nyumba zetu ziko salama. Tunaishi vizuri na familia zetu, tunawatunza watoto wetu? Nimesema *we build strong houses, we fail to build strong homes. We preserve nature but we kill babies*. Tunatunza mazingira ambayo mwanadamu anatakiwa aishi, lakini utakuta watu bado wana-*abort.* Ni namna gani Wizara hii au hizi Kamati zinaishauri Serikali ili kuingiliana na watu ambao nimesema tunahitaji tuwasaidie kwa namna moja au nyingine kwa sababu watu wana changamoto mbalimbali?

Nirudie tena, ni namna gani Chuo kama cha Tumaini ambacho nadhani ni cha kwanza katika Tanzania, kime-*offer* hii *faculty* ya *councelling?* Mna-*connect* vipi na watu? Kweli watu wanalima?

Hatuwezi tukajiamini hapa kwamba, tutawafundisha watu wawe na elimu ya juu, lakini ndani ya familia zetu na ndani ya nyumba zetu ambako tunaanzia huko, ukiwa na baba ambaye anawajibika,

[MHE. MCH. PETER S. MSIGWA]

anayemfundisha mtoto wake kuwajibika, tunakuwa na Taifa lenye maana. Mara nyingi, lakini si mara zote, kwa sehemu kubwa sana watoto ambao wamekuwa familia ambazo zinawajibika ambazo baba na mama wanawajibika kuwatunza wale watoto, nao wameonesha mfano kwamba wanapokuwa na familia zao wanawajibika.

Kwa hiyo, ni wajibu, sijaziona programu za Serikali ambazo zinaandaa kwa kuhamasisha watu kwamba ni namna gani wawajibike kwenye familia zao, ni namna tuweke *values*. Ndiyo maana kuna watu wengine wamesoma hawana *values* katika maisha yao. Hawawezi kujua *wrong* na *right,* kwa sababu hatujawekeza kwenye msingi mkubwa wa nyumbani, ambapo mtoto anaanza kufundishwa nyumbani kabla hatujampeleka kwa mwalimu. Kwa hiyo, ningeomba kwa wale wanaohusika, ni vizuri tukatilia mkazo, maana hili tatizo ni kubwa sana.

Nilitoa mfano juzi hapa, kama tutakuwa na Taifa ambalo kimsingi, takwimu zinaonesha asilimia 42 ya watoto wanaozaliwa wanadumaa. Hebu *imagine*, baada ya miaka 15 au 50 tutakuwa na Taifa la namna gani? Asilimia 40 katika watu kumi, watu wanne wamedumaa; tutakuwa tunazalisha Taifa la namna gani? Mwisho wa siku, tuna wajibu sisi kuliacha hili Taifa bora kuliko tulivyolikuta. Wajibu wetu ni kutengeneza mazingira mazuri. Ukiangalia *life-span* yetu huku Kusini mwa Jangwa la Sahara ni miaka 58 *almost.* Kwa hiyo, ukiangalia Wabunge humu ndani tumebakiza muda kidogo sana.

Sasa swali ni kwamba, tunaachaje Taifa letu kama tukiwa na familia ambazo haziko *responsible*, tukiwa na familia ambazo haziwajibiki? Inawezekana sisi tuliokuwa watu wazima labda hatukujipanga vizuri, hatukuwaandaa watoto wetu vizuri. Je, Serikali na Wizara zinazohusika ni namna gani katika mifumo ya shule zinaandaa hawa watu ambao wana-*deal* na hizo changamoto nilizozisema, watu wengine wanakuwa *abused* hawaonekani mitaani, huko vijijini kuna wengine wana *trauma*, wanapigwa, wako *depressed*?

*[MHE. MCH. PETER MSIGWA]*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengine wako *abused,* hawaonekani Mitaani, huko vijijini. Kuna wengine wana Trauma, wanapigwa, wako *depressed*. Ni *solution* gani ambayo hizi Kamati au hii Wizara na wale wanaohusika wanazitoa?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na michango mizuri ya elimu, lakini nirudie tena kusema tena kwamba mfumo wetu wa elimu huu ambao tumeupigia kelele ni mfumo ambao hautoa majibu ya changamoto tulizonazo. Naomba Serikali vilevile ichukue majukumu haraka kuokoa kwa sababu tuna watu ambao tunawaandaa kuajiriwa, hatuandai watu kuajiri. Kwa hiyo, matokeo yake tumeacha kuwa na somo la kufundisha watu na kikubwa zaidi tumeacha kuwafundisha watu namna ya kujitegemea kwa sababu mfumo tulionao ni kuwalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri tena Wizara zinazohusika kwamba hebu tujitahidi tubadilishe *mind set* ya Watanzania kwamba ukisoma ili uajiriwe ni *mind set change*. Ukienda nchi nyingine huwa wanawaalika hata *motivational Speakers*. Kwa mfano, katika nchi yetu ni nani hawa *Motivation Speakers, inspirational Speakers,* watu ambao wanaweza wakaeleza maisha yao walikotoka, walivyoshindwa, walitoka labda katika *family* duni lakini baadaye kwa kuwa walikuwa wanawaza *positive*, wakafanikiwa. Kwa nchi yetu haya mambo ni kama vile ni mageni.

Ningeishauri hata Wizara, hebu jaribuni ku-*contact* na watu wengine duniani, nimeona nchi nyingine huwa wanawaita watu wakubwa wanaenda kukaa hata na Baraza la Mawaziri, wakawashauri. Kuna mambo mengine ni *mind set change.* Ukiwa una *spiritual problem you need to get a spiritual solution*. Ukiwa na matatizo ya kielimu, unahitaji jawabu la kielimu. Kwa hiyo, mtu akiwa na mapepo hata ukimwambiaje hawezi kukubali inabidi yakemewe; hiyo ni *spiritual solution*. Kwa hiyo, ningeomba haya mambo Wizara iyaangalie tushauriane wote kwa pamoja tuliandae Taifa letu. Lakini kuhusu *mind set* tutafute watu ambao

wanaweza wakahamasisha watu, wakawabadilisha namna ya kufikiri kusudi kwa pamoja tuweze kulijenga Taifa letu, vinginevyo tunaweza tukaliacha Taifa baya kuliko tulivyolikuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mchungaji Msigwa. Nimekuona Mheshimiwa *Engineer* Mnyaa. Kuna nini?

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza Mchangiaji wa hivi sasa aliyepita; na asubuhi ya leo pia kulitokea mambo katika Bunge lako Tukufu, ambapo kwa kutumia Kanuni ya 68 (7) naomba mwongozo uende sambamba na Kanuni ya 64 (1) (g) kuhusu mambo yanayoudhi au lugha zinazoudhi, kwamba hivi sasa hivi tunaendelea mjadala wa Taarifa ya shughuli za Kamati za Maendeleo ya Jamii; na kwa kiasi kikubwa hiyo jamii huko nje wanatusikiliza. Wakitusikiliza Bunge lako Tukufu kuna baadhi ya maneno mengi sana aliyotumia Msemaji wa hivi sasa sijui kama jamii wataelewa. Imetumika sana *SwanEngl* Kiasi ambacho sijui wataweza kuwa na ufahamu, na ndio maana mjadala huu unasikilizwa kwenye *Television* ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini asubuhi pia katika swali Na. 96 la Mheshimiwa Mturano, alitumia lugha ambayo kwa kweli kwa mujibu wa Kanuni inaudhi; pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Michezo na Vijana. Wote wawili walitumia lugha ambayo inaudhi. Lugha hiyo ambayo bahati nzuri na hasa sisi wa Pwani Kiswahili kimejengeka vizuri sana kwamba neno moja unaweza ukalizungumza kwa *terminology* mbili tofauti likawa lina maana ile ile moja. Kwa mfano asubuhi lugha aliyotumia Mheshimiwa Waziri mimi siwezi kuitumia hapa, lakini kamaanisha kujisaidia haja

ndogo kule Uwanja wa Taifa. Mwenzake vilevile, lakini akatumia neno ambalo katika jamii hatulitumii. Hatuwezi kutumia katika Bunge lako Tukufu na walio nje, jamii inayotusikiliza, kutumia neno lile haiwezekani katika jamii yetu. Mimi siwezi kulitamka hapa.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, hebu tupe mwongozo wako kuhusu yale maneno ambayo tunayaharibu lugha yetu ya Kiswahili, jamii inatuelewa vibaya, Waheshimiwa Wabunge kwa heshima zetu tunatamka maneno ambayo hayapaswi katika jamii yetu kuyatamka. Naomba mwongozo wako.

**MHE. NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyaa, bahati mbaya sana hayo maneno mimi wala sikuyasikia. Kwa hiyo, nabaki hapa hata sielewi ni neno gani hasa lililozungumzwa ambalo haliko katika Kamusi ya kawaida ya Kiswahili. Kwa hiyo, ni vigumu sana kutoa mwongozo katika jambo hilo. Lakini kwa vile tuna muda tuendelee kuwasiliana.

Sasa namwita Mheshimiwa Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Zabein Mhita.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kusema machache. Nianze kwa kumshukuru Mungu, nimshukuru vilevile Mchangiaji Baba Mchungaji aliyemaliza muda wake, hakuamsha mihemko, amechangia vizuri kama alivyosema yeye mwenyewe. Hii imeonesha kuna utofauti mkubwa sana kumbe kati ya Wachungaji na Wawekezaji kwenye dini. Maana yake kuna Wachungaji na kuna Wawekezaji kwenye dini siku hizi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka niseme, kama kuna mambo hata sisi Waheshimiwa Wabunge hatutendi haki, ni kusema kwamba tunapongeza Wizara hizi na Kamati hizi. Hatutendi haki. Hizi Kamati zimedharauliwa, hizi Wizara zimedharauliwa na ndiyo maana zimepewa siku moja tu yenye masaa machache ya kuchangia. Hazina umuhimu wowote! Bunge linajua hivyo na Serikali inajua hivyo! Tusianze

kupakana mafuta hapa kwamba Wizara hizi ndiyo uti wa mgongo. Uti wa mgongo gani unachangiwa siku moja na Wabunge gani? Haya ndio mambo ya uongo Waheshimiwa Wabunge tusiyalete hapa Bungeni. Kama tunataka kuambizana ukweli, hizi Wizara ni muhimu lakini hazipewi umuhimu unaostahili. Ndiyo maana mpaka jioni hii wachangiaji wanne, asubuhi wachangiaji wanne biashara imekwisha. Wizara hizi kama hazitakiwi, zifutwe, hela zake zikatumike kwenye Wizara nyingine. Kuliko tunakuja tunapeana sifa hapa, bajeti zao hazieleweki, halafu tunasema Wizara muhimu sana, Wizara mtambuka. Mtambuka gani ambayo inachangiwa siku moja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka nazungumza hapa, Hospitali Teule ya *Mvumi Mission* ambayo imeingia kwenye mpango wa *DDH*, watumishi wake hawajapata mishahara. Leo ni tarehe 13, sasa tunaposimama hapa tunasema Wizara ya Afya inakusudia kujenga sijui watu waimarike kiafya, wale watafanyaje kazi katika mazingira magumu kama haya waliyonayo? Wanaandaa Sikukuu ya *Christmas,* hawajui mbele wala nyuma. Kweli hizi methali zinazosema aliyeshiba hamjui mwenye njaa, ni za kweli. Ndiyo maana mnaona hata tukiingia humu wakati mwingine tunasahau tulikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa napenda kutumia neno hili. Baadhi yetu sisi tumetoka kwenye familia masikini sana, nikiwepo mimi ninayezungumza hapa. Hata mnapozungumza malezi, alipokuwa anazungumza Mchungaji Msigwa amenigusa sana. Mimi ni miongoni mwa Watanzania wachache waliolelewa na mama tu. Baba yangu mimi sikuwahi kumwona. Kwa hiyo, wakati mwingine hata mnapolaumu, mnamlaumu mtu ambaye hamumjui vizuri historia yake. Nimekua katika maisha magumu mno. Ni kwa sababu watu hatujapata muda wa kutosha kusema. Hata hapa nasimama kwa heshima kumshukuru mama yangu Mdala Jane kwa sababu ameweza kunilea mpaka nimefikia hatua hii nakuwa Mbunge. Namshukuru sana.

*[MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE]*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanaishi katika mazingira magumu sana. Tusizungumze hapa kama tunataka kuwafariji watu. Hii Wizara ya Afya kukosekana tu hata katika mpango wa matokeo makubwa sasa, ni kichekesho. Hivi utatengenezaje matokeo makubwa sasa bila afya? Inawezekanaje? Kama afya siyo kipaumbele katika Taifa hilo, mnakuwaje na matokeo makubwa? Ni vichekesho vikubwa. Nenda Muhimbili uone watu wanavyokufa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madaktari sasa hivi wameacha ule mgomo wa kuonekana, wanagoma kimya kimya. Hakuna dawa, mgonjwa anaondoka. Hakuna kipimo, anaondoka. Kwa hiyo, kuna Watanzania chungu mzima wanateseka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nishauri, kama tunataka kujua kwamba Watanzania wanaumia sana kwa Wizara ya Afya kutokupewa bajeti, Waheshimiwa Wabunge tupige marufuku Mbunge kwenda kutibiwa India ili Wabunge wote tutibiwe hapa ndiyo tutakapoelewa ni kwanini Watanzania wanapata taabu. Lakini kwa sababu sisi tukiugua tu hata jipu hapa mtu anasema uongo anakimbizwa India. Hatuoni shida wanazozipata Watanzania. Jamani Watanzania wanateseka kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengine hapa tunayazungumza tu kama ngonjera. Tuzungumze mgawanyo, hata Wizara zenyewe zinavyoingiliana. Ukiangalia namna Wizara inavyoingiliana na Wizara ya Elimu na Wizara ya TAMISEMI, Unaenda kule unamkuta mtu yuko Halmashauri anasema yeye yuko upande wa TAMISEMI. Hawezi kumsikiliza Waziri wa Elimu wala Naibu wake. Hivi kwanini hata Wataalam wetu wameshindwa kutofautisha kazi? Wizara ya Elimu ibaki kuwa Wizara ya Elimu. TAMISEMI ibaki kuwa TAMISEMI. Kuna shida gani? Kuna mwingiliano mkubwa sana.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE]*

Nenda kaangalie mwingiliano kati ya Wizara ya Afya na Wizara ya Mheshimiwa Sophia Simba. Mheshimiwa Mama Sophia Simba Wizara yake inaitwa Wizara ya Jinsia na Maendeleo ya Jamii, lakini Vyuo vya Maendeleo ya Jamii viko Wizara ya Afya. Yaani vichekesho. Kinachozungumzwa kingine, kinachofanywa kingine! Kiasi ambacho hawezi kufoka, hawezi kumwambia mtu mwingine yeyote! Tumelundika vyeo viko zigizaga. Hakuna Waziri anaweza kukemea ukajua huyu anakemea Wizara yake moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda kaangalie Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana. Mwanzoni kabla sijawa Mbunge nilikuwa nafikiri ndiyo inatafutia watu kazi. Kumbe haitafuti kazi, inaitwa Wizara ya Kazi lakini haina kazi. Ukienda mifuko wanayoshughulikia Mheshimiwa Mama Kabaka, ni mfuko mmoja tu *NSSF*. Mifuko mingine iko Wizara nyingine. Hivi tunafanyaje kazi kwa namna hii? Hata nyie Wataalam hamwoni vichekesho?

Nenda huko kwenye Majimbo yetu, utaona vitu vya ajabu sana! Nyumba ya Mganga haijaisha, wanakuja kujenga nyumba ya Mwalimu nayo haijaisha, wanajenga Ofisi ya Mbunge nayo haijaisha; imekuwa Majimbo yote yana magofu matupu. Ni vichekesho! Kwa hiyo hata anaposimama Mbunge hapa anasema suala la kujiuzulu Waziri siyo dawa, hapana. Timu ya Mpira ikifungwa, anajiuzulu Kocha ambaye yeye hachezi. Ni kitu cha kawaida kabisa! Ustaarabu kama huo tujifundishe duniani, wala siyo lazima tuwe tunasukwasukwa, mpaka wasimame sijui Wapinzani waseme na sisi ndiyo tunatekeleza, hapana. Ikionekana watu wamesema huwezi, utoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana tukasema kila zinapokuja taarifa za Kamati, tungetaka Waheshimiwa Mawaziri; jamani bahati nzuri mmenisafirisha nyie wenyewe, nimekwenda China, nimekaa siku 15. *Seriousness* tuliyoiona China, China hakuna wakati Waziri anapungua uzito kama wakati wa Bunge. Sisi hapa ndio wanazidi kunenepa, kila Waziri unaona anaingia *Facebook*. Unapata nafasi ya

kuingia *Facebook* wakati Bunge linakutana? Ni vichekesho vikubwa sana! Kwa hiyo, kuna vitu vya ajabu sana. Tumekwenda pale China, tumekuta hakuna kitu kinachoogopwa na Serikali kama Bunge linapokutana. Waziri anasimamisha ziara zake zote siku kumi kabla ya Bunge kukutana ili kulipa nafasi Bunge. Lakini hapa Bunge linaendelea unaambiwa Waziri yuko ziara. Aah! Ziara ya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikwambie pamoja na ukubwa wa Baraza letu la Mawaziri, bado kuna vijiji chungu mzima katika nchi yetu havijafikiwa na Waziri. Ni vichekesho vikubwa sana! Tangu uhuru kuna Mawaziri hawajakanyaga kwenye baadhi ya Vijiji vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunamsifu leo Hayati Baba wa Taifa, kwa sababu ya kulala vijijini.

Leo kuna Waziri gani anatamani kulala kijijini? Mtu amepewa V8 nzuri, amejaziwa mafuta, ana dereva, lakini kwenda kwenye kijiji tu kwake shida. Unawaona tu siku zote wako Dar es Salaam; sijui Waziri yuko Iringa Mjini; sijui yuko wapi!

Nendeni Vijijini mkaone shida za watu. Mkitembea nyie wenyewe mtalia! Mtatuonea huruma hata Wabunge tunaposimama hapa. Kuna umbali wa kilometa 15 kati ya Shule ya Sekondari mpaka Sekondari nyingine au kutoka Shule ya Msingi mpaka Sekondari! Watu wanashindwa! Kuna Kijiji kimoja kinaitwa Manda katika Jimbola Mtera, mtoto anatembea kilometa 20 katika Jimbo la Mtera kufuata Shule ya Sekondari. Ataacha kupata mimba? Lazima hapo katikati atakutana na mtu amnunulie *chips* ampe mimba. Shule hazina Maabara!

Mheshimiwa Naibu Spika. Halafu mgawanyo, hebu tuangalie wataalam wetu, tuangalie hivi katika mikoa yetu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Hiyo ni kengele ya kwanza. Naifuata!

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu, Mikoa ipi ilianza kupata elimu mapema na Mikoa ipi ilichelewa, na sababu zake. Halafu tuipe upendeleo wa kutosha. Mnatujengea Chuo *UDOM* hapo. Hivi nyie mnafikiri Wagogo watakwenda *UDOM* kwa kucheza ngoma? *UDOM* inaenda kwa kusoma. Kama hamtupi Sekondari zenye Maabara, zenye umeme, zenye majengo ya kuhifadhi watoto wakalala pale, *UDOM* pale wataenda watoto wenu hao hao, nasi mtakuwa mmetuwekea kama *label* tu hapa!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili jambo haliwezekani. Hatuendi Chuo Kikuu kwa kucheza ngoma, kuchezea viongozi, hapana. Tunakwenda Chuo Kikuu kwa kusoma. Lifikirieni jambo hilo. Siyo tunakuja tunapiga porojo tu hapa.

Sekondari zetu hazina Maabara, Sekondari zetu hazina Mabweni, hazina umeme, halafu mnakuja mnatuambia Chuo Kikuu tumejenga Dodoma. Mnatujengea kwa ajili ya kutusanifu? Haiwezekani! Lazima mboreshe! Kama mnataka kutusaidia, boresheni Sekondari zetu, boresheni mazingira yetu ili na sisi tuweze kusoma, tuweze kupiga hatua kubwa. Ni masikini wachache sana wa Tanzania wanaweza wakafikia ujasiri nilionao mimi katika mazingira niliyokulia. Msifikiri ni jambo rahisi kwa mtoto aliyekua katika mazingira magumu kama ya kwangu mimi, awe Mbunge katika nchi hii. Siyo jambo rahisi!

Kwa hiyo, tutengeneze mazingira ya kuwafanya Watanzania wote popote walipo wapate fursa. *(Makofi)*

Ndugu zangu kuna vitu vinaumiza sana. Mimi wakati nikikua nimeshaoa mke wangu; mimi ni miongoni mwa watu wenye uzoefu wa ndoa. Nataka nikwambie Mchungaji Msigwa. Nimeoa nikiwa na miaka 23 na nimeoa nikiwa sina Mshenga. Nilikosa nauli ya kumsafirisha Mshenga. Nilikwenda mimi mwenyewe na nikamwoa Edina mimi

*[MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE]*

mwenyewe, sina Mshenga. Kwa hiyo, kwenye ndoa yangu hakuna ugomvi, kwa sababu hatuna mtu wa kwenda kumlilia. Kwa hiyo, kila siku namwambia, tukigombana, lazima tuelewane! Tukiwa tumepanga, tumeshindwa kulipa kodi, wenye nyumba wamekuja kung'oa bati juu, na mvua ikatunyeshea. Ni Watanzania wangapi wanateseka hivi? Halafu sisi tunakaa hapa tunapiga porojo!

Serikali kuweni *serious*! Tusione aibu, Waziri hata akiwa rafiki yetu, kama hatoshi tumwambie tupishe! Huu uwe ni utaratibu! Kila Bunge likija, lazima liondoke na Waziri mchovu, ndio Bunge hili litaheshimika. Lakini tukianza kutafuta ushahidi, sijui nani alete majina; hivi kweli nchi hii haijui kwamba kuna watu wameiba hela na wameweka nje, mpaka tuseme lete majina, lete majina. Tunaleta mambo ya mbwembwe hapa! Tunafahamu wote nchi hii imetoka wapi, iko wapi na inakwenda wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nisema kwa uchungu sana na sijapata kuzungumza maneno makali kwa Serikali yangu. Kuna baadhi ya vitu lazima tuvitekeleze. Hatuwezi kukubali kuwa na Mawaziri ambao muda wote wana-*chat* kwenye *Facebook*, Mwanajamii, wanaacha kufanya kazi za kujenga nchi hii, nchi ambayo iko nyuma kwa kila aina. Tumetembea nje tumeona.

Tumeona Bunge la Japan namna ambavyo wako *serious*. Huwezi kukuta mapengo! Hata Waheshimiwa Wabunge tujitendee haki. Juzi Mheshimiwa Ally Keissy alisema, kuna Wabunge wanasaini posho, lakini hawafiki. Hata humu kwenye kikao kuna Wabunge tunasaini, lakini hatuji vile vile. Kwa hiyo, tusiangalie tu zile safari za nje, tuangalie hata Bunge lenyewe na hoja tunazozingumza ni zipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, lakini naiomba Serikali, kila mwaka Kamati zinapoleta taarifa, tuwaambie *serious* na tule vichwa vya Mawaziri hata wawili watatu, watachangamka hawa! Watakuja kufanya kazi kwa heshima. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana mdogo wangu Mheshimiwa Livingstone Lusinde. Tunakushukuru sana kwa hotuba yako nzuri. Alichosema ni kweli. Ukikulia mazingira magumu kama ya Vijijini ya Mkoa wa Dodoma, ukafika mahali pakuwa Mbunge, hata Naibu Spika ujue ni shughuli kubwa. *(Makofi)*

Ni kweli kabisa, ukitaka kujua umasikini tembelea Mkoa wa Dodoma Vijijini uweze kujua. Hali ni ngumu sana! Tumepitia mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Zabein Mhita.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa jicho lako kuweza kuniona. Nami naomba nichangie hoja zilizo mbele yetu.

Naomba nikiri kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, lakini pia nikiri kwamba mimi ni Mwalimu. Nimeona hapa ndiyo nafasi yangu ya kuzungumzia Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ushahidi katika jengo hili kuna mwanafunzi wangu hapa ambaye ni Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie hasa kuhusu matatizo ya Walimu. Waswahili wanasema, aliyevaa kiatu ndiye anayejua wapi kiatu kile kinamfinya. Kama hujavaa kiatu, hujui wapi kinamfinya mtu. Kwa kutembea tu huwezi ukajua. Naomba nieleze matatizo ya Walimu nchini hapa.

Humu ndani ya hili jengo, Waheshimiwa Wabunge, nani ambaye hakupita kwa Mwalimu hapa? Walimu wetu hawa wamekuwa ni kama daraja la watu kupanda na kufika juu. Watu wanapanda daraja wanafika juu Walimu wako pale pale. Waheshimiwa Mawaziri wote mmepita kwa hawa Walimu. Mheshimiwa Naibu Spika, wewe pia umepita kwa Walimu. Kila aina ya taaluma wamepita kwa

Walimu, lakini Walimu hawa kwa kusema kweli wana shida kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kueleza kwamba pamoja na majukumu makubwa ya Walimu ya kufundisha, lakini Walimu hawa utawakuta wakishiriki mambo ya Sensa wapo, Walimu hawa utawakuta wanashiriki kwenye chaguzi mbalimbali, wapo. Wapo kila mahali, lakini pamoja na majukumu yote, Walimu hawa wana matatizo mengi. Walimu hawa naomba nizungumzie kuhusu madeni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wana madeni makubwa ambayo wanaidai Serikali, lakini kuna baadhi ya Walimu bado mpaka sasa ninavyoongea hawajalipwa. Pamoja na Serikali kwamba iliweza kutenga kiasi cha Shilingi bilioni 52 mwaka 2009 mpaka 2012, lakini bado wapo Walimu wanadai.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme moja. Ukiihoji Serikali kuhusu madeni ya Walimu, wanasema kwamba kuna baadhi ya Walimu ambao hawajalipwa kwa sababu kuna vigezo ambavyo hawajatimiza. Ukiongea na Walimu wanakwambia tumetimiza vigezo vyote. Sasa unashangaa hivi inakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano mmoja tu kutoka katika Wilaya yangu ya Kondoa, Jimbo langu la Kondoa Kaskazini. Kuna Walimu 179 ambao wanadai *arrears* za mishahara yao baada ya kupandishwa daraja tangu mwaka 2011. Sasa ni kithibitisho gani Serikali inakitaka kwa Mwalimu huyu? Wakati ni Serikali yenyewe ambayo imempandisha Mwalimu? Halafu unasema, hajatimiza vigezo. Vigezo gani hivyo? Walimu wanapeleka taarifa zao vizuri na vigezo vyote wanavitimiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali yetu iwafahamishe basi wale Walimu ambao hawajaweza kulipwa waelezwe kabisa ni vigezo gani ambavyo vimekosekana badala ya kuwaacha tu hewani hawajui,

waambiwe mwalimu fulani kuna hiki na hiki hujakamisha; mwalimu fulani unadaiwa hiki na hiki ili wale waweze sasa kuvikamilisha na waweze kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niiulize Serikali pia, eti ni kwa nini Serikali haina mpango endelevu wa kuwalipa Walimu badala ya kulimbikiza madai yao? Kwa nini kila wakati madai haya huwa hayalipwi mpaka yafike mabilioni ambapo inakuwa ni mzigo mkubwa kwa Serikali? Kwa nini?

Tunaiomba Serikali iwe na mpango basi madhubuti wa kuweza kuwalipa hawa Walimu wetu ambao kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana na ni wavumilivu sana Walimu hawa, lakini na uvumilivu nao unafika mahali una kikomo chake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matatizo yote ya hawa Walimu. Kuna Walimu wengi, tena ni wengi sana ambao wanapangwa katika maeneo yenye mazingira magumu. Mfano, maeneo ambayo hayana huduma za afya utawakuta Walimu; maeneo ambayo hayana maji, utawakuta Walimu; maeneo ambayo hayana huduma ya usafiri, utawakuta Walimu. Sasa kwa upungufu huo wa maeneo hayo utakuta kuna upungufu mkubwa sana wa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano katika Jimbo langu. Hivi katika Wilaya yangu ya Kondoa, mfano Mmwalimu anayefundisha Shule ya Matangalimo, kweli utamfananisha na Mwalimu ambaye yupo katika Jiji kubwa? Mazingira yao yanafanana? Mwalimu anayefundisha Gara, Chubi, Mwalimu anayefundisha Kijiji cha Mauno, ama Mwalimu anayefundisha Kijiji cha Kalamba Juu ama Kalamba Chini... *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyaa, upo hapo? Mheshimiwa Zabein endelea kuchangia. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kweli Mwalimu wa Kalamba Chini ama wa Kalamba Juu kweli umfananishe na Mwalimu ambaye yupo Mjini, kweli inawezekana? Haiwezekani! Basi Walimu wanaopangwa katika maeneo hayo, tumeiomba Serikali kwa muda mrefu sana angalau basi walipwe posho ya mazingira magumu. Wakilipwa posho ya mazingira magumu, angalau watapata imani na wataweza kuendelea katika maeneo ambayo wamepangwa. Hivi tatizo ni nini kuwalipa hawa Walimu posho ya mazingira magumu, wakati mazingira magumu yapo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeongelea kuhusu Walimu ambapo nimesema na mimi mwenyewe ni Mwalimu na ninaelewa adha ya Walimu. Sasa naomba nielezee kidogo kuhusu mambo ya afya. Ili Taifa liweze kuwajibika na kuleta maendeleo afya bora ni muhimu. Lakini hali hii itafikiwa vipi? Kuna kilio kikubwa cha upungufu wa madawa, vifaa vya tiba, vitendanishi hakuna katika hospitali zetu, Vituo vya Afya na katika Zahanati. Hakuna!

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili la ukosefu wa vifaa hivi linasukumwa kwa *MSD* ambao wana jukumu la kununua, kuhifadhi na kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Sasa tunawalaumu hawa *MSD*, lakini *MSD* inadai Serikali Shilingi bilioni 52. Taasisi hii inaidai Serikali Shilingi bilioni 52 ambazo hazijalipwa. Kiasi hiki ni kikubwa sana kwa Taasisi kama ya *MSD*. Je, *MSD* inatekeleza vipi jukumu lake sasa la kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi wakati lenyewe lipo hoi bin taabani halina fedha? Serikali imekopa. Serikali haioneshi dhamira thabiti ya kulipa deni hili. Hatujaona mpango ambao Serikali inasema itakuwa inalipa kiasi hiki kila mwaka ikipata fedha, hakuna!

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba tunafahamu kwamba Serikali yetu ina uwezo mdogo wa fedha, lakini basi ioneshe jinsi ambavyo italipa deni hili ili angalau kupunguza deni na kuiwezesha *MSD* iweze kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wamechangia huu Mpango wa *CHF,* wamelipia, wanakwenda hospitali, wanakwenda kwenye Zahanati, wanakwenda kwenye Vituo vya Afya, dawa hakuna, wanaandikiwa karatasi waende madukani wakanunue.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kweli kuna maeneo mtu akiandikiwa karatasi ama cheti kununua hizo dawa anapata. Kwetu katika Wilaya ya Kondoa akanunue wapi mgonjwa? Akanunue katika duka gani? Hali ya Kondoa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Ni kengele ya pili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zabein, dakika kumi ni chache sana.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali basi ilipe hilo deni ili wananchi waweze kupata dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zabein Mhita, nakushukuru sana. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge, atakuwa Mheshimiwa Zitto Kabwe. Baada ya hapo Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa ajiandae.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia Taarifa za Kamati hizi mbili; Kamati ya Huduma za Jamii na Kamati ya Maendeleo ya Jamii ambazo zinahusika na masuala nyeti sana katika Ustawi wa Taifa letu; masuala ya Afya, Elimu na Hifadhi ya Jamii na Maendeleo ya Jamii yenyewe kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inavyoitwa.

*[MHE. KABWE Z. ZITTO]*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la elimu ambalo Wabunge wengi sana wamelizungumzia. Ni dhahiri kwamba tuna *crisis* katika elimu. Ukiiangalia Taarifa ya Kamati, inapendekeza kwamba tuongeze bajeti katika Wizara ya Elimu, lakini ukienda kuangalia nyuma, Bajeti ya Wizara ya Elimu kuanzia 2007/2008 mpaka 2012/2013 utaona kwamba tumepeleka fedha nyingi sana katika Wizara ya Elimu. Lakini ukienda kupima matokeo yanayotokana na fedha hizo kwa kuangalia matokeo ya wanafunzi hasa matokeo ya Kidato cha Nne, huoni kabisa mahusiano kati ya fedha nyingi ambazo tunaziingiza katika Elimu na matokeo ambayo yanapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni dhahiri kuna eneo ambalo ni tatizo la msingi. Tatizo la msingi linaweza lisiwe fedha. Tatizo la msingi inawezekana ni namna gani fedha hizo zinatumika. Kwa mfano, ni kwa nini mpaka leo tuendelee kuwa tunalalamika kuhusu maslahi ya Walimu. Kwa sababu jambo hili lingeweza kumalizwa na kuweza kutoa *motivation* kwa Walimu na kuwafanya Walimu waingie darasani. Kwa sababu tuna tatizo kubwa sana la Walimu kutoingia darasani kutokana na masuala mbalimbali.

Kule katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kulikuwa na mjadala siku moja kuhusiana na mikopo ambayo Walimu wanachukua kwenye Makampuni ya ukopeshaji ambayo yana-*charge* riba kubwa sana. Kwa hiyo, yanamfanya Mwalimu asiweze kabisa *concentrate* darasani, kwa sababu hana mshahara. Mwisho wa mwezi ukifika hapati chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kutoa mfano, siku moja kwamba kuna Walimu ambao wakikopa, wanaacha kadi za Benki (*ATM card)* kwa ile Kampuni inayokopesha, yenyewe ndiyo inaenda kuchukua zile pesa. Yanatokea haya katika Halmashauri zetu. Katika hali kama hii inaonesha dhahiri kwamba kuna kazi ya ziada ambayo inabidi kuifanya kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunalinda heshima na maslahi ya Walimu wetu. Hata tufanye nini,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



hata tupeleke fedha nyingi kiasi gani Wizara ya Elimu, kama hatutafafanua na kuboresha maslahi ya Walimu, tutakuwa tunacheza tu. Tutakuwa tunacheza tu! Hili ni jambo ambalo ni lazima liangaliwe kwa makini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuweze kuhakikisha kwamba tunamfanya mwalimu aone raha kufundisha, aifurahie kazi yake. Walimu ambao wanafundisha maeneo ambayo hayafikiki, maeneo ambayo hali ya maisha ni ngumu, maeneo ambayo hayana umeme, maeneo ambayo hayana maji, maeneo ambayo usafiri ni mgumu, lazima wapewe fedha zaidi ya Walimu ambao wanafundisha maeneo ya kawaida kama jinsi ambavyo Taarifa ya Kamati ilivyoeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna tatizo kubwa zaidi. Tunafanya nini kwa watoto ambao wanashindwa kuendelea Kidato cha Tano na Sita. Tunafanya nini kwa watoto ambao wanapata *zero* au daraja la Nne ambao hawawezi kuendelea zaidi kusoma? *Solution* ni moja, ni *VETA*. Kasi yetu ya ujenzi wa *VETA* iko namna gani? Tumesema kwamba tutaendelea kujenga *VETA* kila Wilaya ifikapo mwaka 2015. Kasi ya ujenzi wa *VETA* hivi iko namna gani? Toka tumeingia mwaka 2010 mpaka sasa, Waziri wa Elimu amezindua *VETA* ngapi katika Wilaya zetu? Haya ndiyo maswali ambayo tunapaswa kujiuliza. Vinginevyo tutakuwa tunapiga siasa tu! Tutakuwa tunapiga porojo tu! Kila mwaka yatatoka matokea mabaya, tutalalamika, tutalia, tutarudi tutakaa, mambo yanaendelea kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima sasa ufanyike uamuzi mahsusi wa kuunganisha *VETA* na Jeshi la Kujenga Taifa. Tuhakikishie kila Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa ina Chuo cha Ufundi. Siyo hivyo tu, tuhakikishie kwamba mtoto anayemaliza *VETA,* kama amesoma uashi, uselemara, Umekenika na kadhalika aondoke na vifaa vya kwenda kumfanya aweze kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo kubwa sana la demografia katika nchi yetu. Tunavyozungumza sasa

nusu ya Watanzanipa wapo chini ya umri wa miaka 17. Tuna watoto wengi zaidi kuliko watu wazima. Tukikaa vibaya, hili ni bomu. Wengi hawapendi kuliita hivyo bomu, lakini hili ni bomu. Tunaenda kwenye *demographic bomb* iwapo hatutaweza kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapata *skills* za kuweza kujiajiri, wapate kazi waonde umasikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuwe na Mpango Maalum. Tunahitaji siyo chini Shilingi bilioni sita kujenga *VETA* moja ambayo ina vifaa vyote. Kwa ujumla, Wilaya ambazo zimebakia nchini, tunahitaji Shilingi bilioni 720. Lazima tuone fedha hizi tunazitoa wapi? Programu ionekane; na tumwekee malengo Waziri kwamba kila Taarifa ya Kamati inayokuja kusomwa hapa atuambie amefungua *VETA* ngapi mwaka huo? Vinginevyo, bila kuweka hizo *indicators* tutakuwa tunacheza. Hilo ni la pili ambalo nilikuwa napenda kulizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, nadhani bado Taarifa ya Kamati ukurasa 10 imezungumzia tatizo la viwango vya ufaulu, zile alama wanaita madaraja ya ufaulu na Wizara ya Elimu ilivyotangaza na bila kushirikisha Baraza la Mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni kosa la Kisheria. Baraza la Mitihani ndiyo chombo pekee ambacho kinasimamia masuala ya ufaulu. Wizara inawezaje kutangaza madaraja mapya ya ufaulu bila kushirikisha Baraza la Mitihani? Halafu Wabunge tukasema, ipite tu! Watumie madaraja mapya; ipite tu. Hapana! Tunahitaji suala la uwajibikaji hapa. Lazima watu waeleze. Maamuzi haya siyo ya bahati mbaya, ni maamuzi ya makusudi. Ni maamuzi ambayo yanaingiza siasa kwenye Elimu. Tusipokasirika na kuyakataa, haitatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nataka kulizungumzia ni katika Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Suala la Hifadhi ya Jamii. Wabunge wamezungumza sana kuhusiana na pesheni kwa wazee. Pia hata Kamati ya Huduma za Jamii imezungumzia suala la *University Coverage*

*[MHE. KABWE Z. ZITTO]*

kwenye Afya. Asilimia sita tu ya Watanzania ndio wapo kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuanze Mpango Maalum wa kuhakikisha Watanzania wengi zaidi wanaandikishwa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ya kuhakikisha tunaondoa ile dhana ya kwamba mkulima hana pensheni. Kwa kuhakikisha wakulima kupitia Vyama vyao vya Ushirika, wanajiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ukiamua kuwa na pensheni kwa wazee, wakati una watu wengi sana ambao hawaingii kwenye kujiwekea akiba, huko mbele mtagonga mwamba tu. Mtagonga mwamba! Mta-*solve* tatizo la leo, lakini baada ya miaka 10 mbele hamtakuwa na Taifa. Taifa lenyewe hili lenye *demography* hii, hatutaweza kufika!

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupendekeza Serikali ijaribu kuangalia, Mheshimiwa Waziri wa Kazi ajaribu kuangalia kama tunaweza; kwa mfano, nchi nyingine zinavyofanya, mkulima akijiwekea akiba ya Sh. 10,000/= kwa ajili ya pensheni, Serikali inaweka Sh. 10,000/= nyingine pale. Kwa hiyo, mnajikuta mna watu wengi sana ambao wapo kwenye mfumo wa pensheni na hivyo huko mbele hamtapata taabu kuweza kuwa na pensheni ya wazee wachache ambao hawakuweza kuchangia.

Kwa hiyo, nilikuwa napenda nipendekeze katika Kamati ya Maendeleo ya Jamii jambo hili waweze kuliangalia, ili tuweze kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa na watu wengi zaidi ambao wapo kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili waweze kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naomba tu nim-*quote* Mahatima *Gandhi* alisema "*first they ignore you, then they laugh at you, then they fight you, then you win.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto Kabwe ahsante sana na hasa ulivyomalizia.

Sasa namwita Mheshimiwa Shukuru Kawambwa - Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja hizi mbili za Kamati za Kudumu za Bunge. Nitajaribu kufanya mapitio katika maeneo yale ambayo yameongelewa na Kamati kwa msisitizo na pia yale ambayo yameongelewa na Waheshimiwa Wabunge kwa msisitizo kwa kadri ambavyo muda utakuwa umeniruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme pia katika yale ambayo nitakosa kuyatolea majibu, Waheshimiwa Mawaziri watakaofuatia wataweza kuyatolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la madeni ya Walimu. Nakiri kwamba suala hili ni zito, ni suala ambalo limeleta madhila sana kwa Walimu wetu, lakini siyo kwamba wamenyongeka Walimu katika hili na Serikali pia siku zote ilikuwa imenyongeka katika jambo hili. Tumejitahidi kwa kila namna kulitafutia dawa ili liweze kuondoa kabisa katika historia ya maendeleo ya Elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo ya kimfumo ambayo tumeanza kuyafanyia kazi kwa nguvu zote ili tuweze kuyaondoa haya matatizo ya kimfumo ambayo yanasababisha tuwe na madeni na kuendelea kuirudisha nyuma Sekta yetu ya Elimu. Kwa sababu madeni haya yanahusisha Wizara kadhaa; Wizara ya Elimu, TAMISEMI, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, na Hazina.

Kwa hiyo, ukishajumlisha milolongo hiyo unajikuta kwamba umefika mahali ambapo siyo pazuri sana. Kwa hiyo, ni wakati ambapo tunahitaji kujitoa katika mifumo ile ambayo inaturudisha nyuma badala ya kutusukuma mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya juhudi mwaka wa fedha 2011/2012 kukusanya madeni yote; jumla yalikuwa Shilingi bilioni 52 na ushee na tukaanza kuyalipa madeni hayo. Ni madeni ambayo tuliyakusanya na kuyahakiki kwa kushirikiana na Chama cha Walimu chenyewe ili tuwe na uhakika kwamba madeni hayo ndiyo yale. Chama kikisema ni hayo, na Serikali iseme ni hayo bila kuvutavuta kwamba huyu anasema ni deni, na huyu anasema siyo deni.

Sasa yale ni madeni ambayo yamekusanywa na kuhakikiwa mpaka Juni, 2011. Ndani ya mwaka 2012 tukayalipa. Lakini kipindi cha mwaka mzima wa 2012 na mwaka huu mwaka wa 2013 kwa sababu mfumo haujabadilika, madeni yanatengenezwa na yanajilimbikiza. Kwa hiyo, baada ya kuyalipa yale madeni, tumeingia kwenye *circle* ya kuhakiki sasa, kuanza kuanza kukusanya na kuhakiki madeni haya mapya ambayo sasa hivi tunaenda nayo kwa juhudi kubwa ili tuweze kuyalipa. Tumeweka azma maalum ya kuhakikisha kwamba haya madeni tunayalipa haraka iwezekanavyo ndani mwaka huu wa fedha. Kwa sababu tunataka tuondokane na madeni kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishaondokana nayo, siyo kuondokana nayo tu, jambo kubwa zaidi ni la kuhakikisha kwamba tunaondokana na kadhia ya kulimbikiza madeni. Kwa hiyo, tumeweka mkakati kwamba lazima tuondokane na kadhia yenyewe ya kulimbikiza madeni. Kwa sababu tulilipa madeni, lakini mpaka sasa hivi kama Waheshimiwa Wabunge wanavyosema, Walimu bado wanalalamika hawajalipwa madeni yao. Kwa sababu tuliyoyalipa ni yale tuliyoyakusanya, tukayahakiki na kuyalipa ni mpaka June, 2011. Lakini mwaka 2012 tulikusanya madeni mengine; na mradi mfumo bado upo huo huo, tutaendelea hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jambo kubwa kabisa ambalo tumelifanya ni kuweka mkakati wakuondokana na kadhia ya kulimbikiza madeni haya. Mikakati hiyo: moja, ni kwa wajiri wapya. Waajiriwa wapya waweze kuingia

kwenye orodha malipo mara moja tu wanapoingia kwenye ajira yao bila ya kupoteza muda na waanze kulipwa moja kwa moja.

Pili, ni kurekebisha mishahara ya Walimu mara tu wanapopanda madaraja. Akipanda daraja anarekebishiwa mshahara papo kwa papo, kwa utaratibu ambao umetengenezwa sasa hivi na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwamba hilo litakuwa linawezekana.

Tatu, kudhibiti uhamisho usiokuwa na tija kwamba kusiwe na uhamisho. Pia kutenga bajeti kwa ajili ya malipo stahili mbalimbali ya Walimu ili kuhakikisha kwamba fedha ipo wakati tunapofanya upandishwaji wa madaraja. Hili ndilo ambalo tunalifanya sasa hivi. Kama tulikuwa tuna matatizo hayo, tumeyaangalia kwa karibu mno. Tumeangalia pia kwa sababu tuna mpango mpya wa Matokeo Makubwa Sasa; tumeweka azma kule kwamba itakapofika Desemba tusiwe na madeni yanayozidi miezi mitatu kwa Mwalimu yeyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tupo nyuma katika kulitekeleza hili, lakini hili lazima litekelezeke kwa sababu tumeliahidi ndani ya mpango huu ambao siyo wa mzaha wala siyo wa kubabaisha. Kwa hiyo, hili tutalitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza kwa kauli, lakini tutaomba tu Waheshimiwa Wabunge, wananchi na Walimu kwa ujumla tuangalie zile hatua ambazo tunazichukua ili waone kama zinafanana na yale ambayo tunayasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la ujenzi wa Vyuo vya *VETA*, limezungumzwa kwa hisia kali. Niseme tu kwamba tunalitambua kwasababu kuna vijana wetu ambao wanamaliza Shule za Msingi na Sekondari kila mwaka kwa idadi kubwa, ambao hawapati nafasi ya kwenda katika ngazi inayofuatia. Kuna ambao hawapati nafasi ya kwenda Sekondari na wale ambao hawapati

nafasi ya kwenda katika Sekondari ya Juu. Wako kwa malaki! Kuna kipindi walikuwa wanakimbilia hesabu ya milioni.

Sasa kama Wizara tumeandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundi mahususi kwa ajili ya sekta hiyo. Mpango huo umekamilika, tumewasilisha kwenye Kamisheni ya Mipango, ili uweze kuhakikiwa na kupewa *priority* kwamba ni moja katika vipaumbele katika mipango ya Serikali. Ndani ya mpango huu, tutatekeleza ujenzi wa Vyuo vya *VETA* ndani ya nchi yetu kila Wilaya kuhakikisha kwamba tunafanikiwa kutimiza ile ahadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeanza sasa hivi kabla hata huo mpango kutengewa pesa nyingi, lakini tumeshirikisha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ambapo mwaka huu peke yake tumeshachukua Vyuo 25 na sasa hivi wameshadahiliwa wanafunzi 1,250 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili waweze kupata mafunzo ya ufundi stadi. Tutaendelea kuhakikisha tunaviboresha viwe Vyuo ambavyo vinaweza vikatoa taaluma hizi zote mbili kwa kipindi kimoja. Kwa hiyo, hili jambo lina mkakati maalumu pale tulipoambiwa kwamba na Waheshimiwa Wabunge tengenezeni mpango; wala hatusubiri kuambiwa tutengeneze mpango. Tayari tumeutengeneza na sasa hivi uko katika hatua za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la Baraza la Mitihani Tanzania kutohusishwa katika upangaji wa madaraja. Naomba niseme kwamba suala la madaraja lina historia ndefu. Lilihusishwa na Kamati kadhaa ambazo zilifanya udadisi baada ya matatizo chungu nzima ambayo yametokea, Kamati ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka 2010; mwaka 2011 mimi nilitengeneza Kamati kwa ajili ya *Islamic knowledge* na kadhalika.

Ushauri tuliopewa umeanza kutekelezwa mwaka 2012, niliwakabidhi Baraza lenyewe wakaleta mapendekezo ambayo tuliyatekeleza na yakaleta mtikisiko.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Sasa hivi ili tuendelee kuondoa kadhia zile zilizokuwa zinatokea tumeichukua *NECTA* yenyewe na Taasisi kadhaa nchi nzima zinazohusika na elimu ikitanguliwa na Kamati Maalum ambayo ilifanya mchanganuo kuandaa kazi hii ambayo imetangazwa na Serikali hivi karibuni.

*NECTA* imehusishwa na Taasisi chungu nzima zimehusishwa. Wadau kadhaa nchini, kila anayejulikana ni mdau, amehusishwa katika zoezi hili. Kama kuna mtu ambaye hakuweza kulifanyia kazi hili ni Bodi ya *NECTA* ambayo ni kazi ya Menejimenti ya *NECTA* kufikiza kazi hii kwenye Bodi yake.

Shirika lolote, Taasisi yoyote kupeleka kazi kwenye Bodi ni ya Menejimenti, haambiwi na mtu mwingine kwamba kazi hii ipelekwe kwenye Bodi.

Kazi imefanywa kwa umakini, lakini nikiri kwamba pale palipotokea tatizo, baada ya kulibaini tatizo, Serikali imeanza kulifanyia kazi ili tatizo hilo liondoke ili tusonge mbele, tuhakikishe kwamba vijana wetu; yale katika ripoti zilizopita nilisema kwamba hiki kinachofanywa sasa hivi mpaka hapo tulipoanza kufanyia kazi kinasababisha kufeli kwa wanafunzi, tukiondoe na ndicho hicho ambacho tumeanza kukifanya hivi sasa tuhakikishe kwamba watoto hawa hawatendewi dhuluma tena. Kila mwaka wapate kile ambacho wanastahili kukipata kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya wao, na kwa kazi kubwa ambayo Walimu wao wanaifanya na wazazi wanawategemea sana kuhakikisha kwamba wanafanikiwa katika kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kukosa muda, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Kawamba. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Dkt. Seif Rashid, atafuatiwa na Mheshimiwa Celina Kombani.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja ya Kamati ya Bunge. Nitajaribu kupitia vipengele kadhaa ambavyo Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge mmoja mmoja wameweza kutoa maelezo yao katika Wizara hii ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza ambayo ni ya muhimu imezungumziwa katika suala zima la Bajeti na hasa kusudio la kutekekleza makubaliano ya Abuja, kiukweli Azimio la Abuja ni zuri na kama tungeweza kulifanikisha, maana yake sehemu kubwa katika utekelezaji wa masuala ambayo yanahitajika katika utekeleza na kukamilisha utekelezaji wa Afua mbalimbali zinazohusu mambo ya Afya, ungeweza kufanyika. Lakini nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba huduma za Afya na Ustawi wa Jamii zinatolewa kwa kiwango kinachowezekana kutokana na mapato yake ya Serikali katika mwaka husika.

Nitoe tu Taarifa kwa ufupi sana kwamba kwenye miaka ya karibuni Serikali imeongeza pesa au Bajeti ambazo zimetengwa kwenye Wizara hii ya Afya na Ustawi wa Jamii kutoka Shilingi bilioni 925 mwaka 2009/2010, na 2010/2011 kuwa Shilingi bilioni 1,205 sawasawa na asilimia 12, na baadaye mwaka 2013/2014 mwaka huu kiwango cha Bajeti ya Shilingi bilioni 1,497 ambayo pamoja na kwamba kwa mujibu wa kiasilimia ni asilimia 10, lakini ongezeko ni zaidi ya Shilingi bilioni 200 katika Bajeti ya mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha msingi hapa ni kuangalia namna gani ambavyo Wizara hii itakuwa na pato la ziada, ama mapato mbadala ili kuhakikisha inatekeleza majukumu yake.

Sehemu ya kwanza tunazungumzia utoaji au michango ambayo wananchi wanatakiwa kutoa hasa kwakuwa wanachama wa Bima. Mifuko ya Bima ni sehemu mojawapo ya kuziwezesha hospitali zetu na Vituo vyetu vya Tiba kupata mapato ya kuweza kufanikisha uwepo wa dawa, uwepo wa vitendea kazi, lakini vile vile majengo

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*


kuboreshwa na Watumishi wakirudi nyumbani wawe katika mapato mazuri. Sasa katika hili kuna hatua mbili za msingi ambazo Serikali inakusudia kuzifanya.

Cha kwanza ni kuunganisha kwa mujibu wa Sheria, kufanya mabadiliko katika Sheria, kuunganisha ule Mfuko wa Afya ya Jamii pamoja na Mfuko wa Bima ya Taifa ili ukiunganisha Mifuko hii miwili, tutaweza kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanahamasishwa na wanakuwa wanachama wa Bima. Katika kulifikia hilo, maana yake Vituo vyote vya Tiba vitakuwa vinatoa huduma kwa watu wenye Bima wengi zaidi, kwa hiyo, mapato yake yatakuwa makubwa zaidi na kuwezesha kuziba mapengo ya kibajeti ambayo yanatokea mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima nitoe angalizo katika yote haya. Pamoja na nia nzuri ya Serikali kuhakikisha kwamba Bajeti inaongezeka, lakini vile vile tusisahau wakati tunajadili hili kwamba Watanzania takriban milioni moja wanaongezeka kila mwaka. Katika hili maana yake ni kwamba mahitaji yanaongezeka. Wanahitaji Hospitali ya Mkoa, Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati kila mwaka. Hizi ni mpya zinazotakiwa kujengwa kila mwaka.

Pamoja na hilo, tumeona kwamba mali bila daftari hupotea bila habari. Kwa hiyo, tumeandaa mkakati wa kuboresha mifumo wa takwimu, upatikanaji wa takwimu kwa kutumia njia za ki-*electronic.* Katika hili, mfano mmojawapo ni Hospitali ya Muhimbili na Hospitali ya Mbeya kama Kamati ilivyokuwa imeelezea, namna ambavyo wameongeza mapato yao kwa kubadilisha na kuweka mfumo wa kielectroniki.

Wizara sasa inakusudia kuhakikisha kwamba mifumo hii inafanyika na inatekelezeka karibu katika Vituo vyote vya kutolea huduma hapa nchini tukianza na vituo vikubwa vile katika ngazi ya Taifa, ngazi ya Kanda na ngazi ile ya Mikoa. Kwenye hili, litatuwezesha kusimamia mapato, kusimamia rasilimali watu, kusimamia matumizi ya dawa pamoja na vitendea kazi vyote ambavyo vinafika kwenye

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Vituo vyetu visiwe vinavuja kwenda nje ya Vituo. Hivyo, kuweza kufahamu kabisa uhalisia wa mahitaji yetu na namna ambavyo tunatumia hayo mahitaji ambayo tunayapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie eneo la uboreshaji wa huduma za Afya ya msingi katika mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi. Kwa hakika juhudi za Serikali ni kubwa na kwamba eneo kubwa ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia ni kwamba Zahanati na Vituo vya Afya vinajengwa lakini hazifunguliwi kwasababu zinakosa Watumishi.

Juhudi za Serikali katika kuongeza eneo hili la Watumishi; kwanza, ni kuwapa fursa watu kwenda kuingia katika Vyuo kujifunza ili wawe Wataalamu. Katika eneo hili, idadi ya wanafunzi ambao wanaingia Vyuoni mwaka hadi mwaka imekuwa imeongezeka. Hata nikitolea tu mfano wa mwaka jana 2012, ambapo wanafunzi 7,458 ambao waliingia Vyuoni mwaka huu ambao watakuwa wameingia Vyuoni ni 7,956. Hii ni karibu wanafuzi zaidi ya 500. Lengo ni idadi ya wanafunzi ambao wanaingia Vyuoni kufikia 10,000 ifikapo mwaka 2017.

Hilo ni eneo moja. Eneo la pili ni kwamba Serikali imekuwa ikiongeza idadi ya watu ambao wanapata fursa ya kuajiriwa baada ya kumaliza masomo yao. Katika miaka hii kuanzia mwaka 2009/2010 hadi 2012/2013 jumla ya nafasi 29,589 ya ajira kwa watumishi wapya imefanyika.

Vile vile Vituo vya kutolea huduma vya Afya na vyenyewe vimeongezeka kama nilivyosema awali. Vituo vya Afya vimeongezeka kutoka karibu 5,400 na hadi kufikia 6,600 mwaka jana 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapoongeza Vituo vipya maana yake unaongeza uhaba. Katika tafsiri hiyo, maana yake bado tuna uhaba mkubwa, ingawa kuna unafuu mkubwa. Tulikuwa na uhaba mkubwa mwaka 2006/2007 wa kiwango cha 67% leo tunazungumzia uhaba wa

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



watumishi katika Vituo hivyo kwa kiwango cha 50%. Ni hatua kubwa ambayo imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikutoa nafasi moja tu ya Wauguzi, Wauguzi idadi yao, wafanyakazi wameongezeka kutoka 10,000 mwaka 2005 hadi kufikia 20,000 mwaka 2010. Ni mara mbili ya ile ambayo ilikuwepo miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipate fursa ya kwanza kuzungumzia eneo la deni la *MSD* kabla muda wangu haujaisha.

Deni la *MSD* ni kweli Serikali ipo pamoja, Wizara yangu pamoja na Wizara ya Fedha, tumekaa kwa pamoja mwezi Novemba, 2013, baada ya kufanyiwa uhakiki wa deni lenyewe na Wizara ya Fedha imekubali kulipa deni hili kwa awamu kuanzia mwezi januari mwaka 2014. Kwa hiyo, tunaamini deni hili litakapokuwa limeanza kulipwa mwezi ujao, yaani Januari, 2014 basi hatua na uwepo wa dawa katika Vituo vyetu utaanza kuwa mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie eneo la huduma za afya ya akina mama na watoto, eneo ambalo wenzangu Waheshimiwa Wabunge wamechangia wakionyesha uhitaji, umuhimu wa uwepo wa Bajeti maalum kwa ajili ya vifaa vya kujifungulia na dawa za uzazi wa mpango. Nitoe tu taarifa kwamba kwenye Bajeti ya mwaka 2012/2013 tulikuwa na kiwango cha karibu Shilingi bilioni 15 zilitengwa kwenye eneo la Bajeti ya Chanjo, vifurushi vya vifaa vya vifaa vya kujifungulia na dawa za uzazi wa mpango. Mwaka 2013/2014 imeongezeka hadi kufikia Shilingi bilioni 36.9. Lakini tukijumisha na mradi unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika unaotekelezwa kwenye Mkoa wa Tabora, Mara na Mtwara, katika Mikoa hiyo, Serikali imejenga vyumba vya upasuaji na kununua vifaa, mashine katika Hospitali za Mikoa, Wilaya katika Vituo vya Afya kwa ajili ya huduma ya mama wajawazito.

Kwenye eneo hili maana yake ni kwamba tutaendelea kuboresha Mikoa mingine kadiri pale pesa

zitakapokuwa zinapatikana ili kuhakikisha huduma za mama mjamzito zinaboreshwa na zinakuwa nzuri katika maeneo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie sasa umuhimu wa kuwa na huduma za Bima ya Afya kwa wananchi wote, yaani *universe coverage.* Kwa bahati nzuri Mfuko wetu wa Bima ya Afya pamoja na Wizara yangu wamefanya tafiti mbalimbali ili kuweza kupata majibu yatakayoweza kutusaidia katika kuhakikisha kwamba tunaandaa mkakati wa kuboresha eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashid. Sasa namitwa Mheshimiwa Celina Kombani, atafuatiwa na Mheshimiwa Gaudentia Kabaka.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI)**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu masuala ya Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la Mheshimiwa Barwany ambaye amesema kwamba Walimu wana chuki sana na Serikali yao. Mimi napenda kumwarifu Mheshimiwa Burhani kwamba Serikali ina mahusiano mazuri sana na Walimu, na kupitia Vyama vyao tunashirikiana nao kwa karibu sana katika kuhakiki madeni yao hasa yale madeni yanayohusiana na mishahara.

Kwa mfano, tarehe 30 Agosti, 2013 tumekaa na Chama cha Walimu kuchambua madeni yao. Tukakubaliana tukae tena tarehe 18 Septemba, 2013. Tumekaa nao, tumehakiki nao madeni na tunaendelea kuhakiki nao.

Kwa bahati nzuri, wakati wa uhakiki wa madeni Chama cha Walimu katika Wilaya husika wanashirikishwa katika kuhakiki madeni hayo. Tumekaa tena na Chama

cha Walimu tarehe 8 Novemba, 2013 kwa ajili ya suala hilo hilo la kuhakiki madeni na tutakaa tena tarehe 30 Desemba, 2013.

Kwa hiyo, wazungumzao hawagombani. Sisi tunazungumza nao, tunahakiki madeni kwa pamoja, uhakiki wetu sasa hivi ni shirikishi. Kama Mheshimiwa Burhani katika Wilaya yako Chama cha Walimu hakikushirikishwa katika uhakiki wa madeni, mimi naomba utupe taarifa ili tuiambie hiyo Halmashauri iwashirikishe katika uhakiki wa madeni.

Suala la pili ni kuhusu mazingira magumu, Mheshimiwa Lucy Owenya; dada yangu Mheshimiwa Zabeni Mhita ameliongelea sana na Kamati imeongelea sana kuhusu posho ya mazingira magumu kwa Walimu. Lakini tujiulize, hivi wafanyakazi wa vijijini ni Walimu peke yao? Wako Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata, watu wa Kilimo na Kada mbalimbali. Kwa hiyo, tuwasemee wote kwa ujumla wao. Tusisemee kada moja tu kwasababu wote wanaishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira magumu tunayaangalia katika *parameters* zipi? Ni zile sehemu ambazo hazina huduma muhimu kama maji, huduma za afya, barabara, mawasiliano na nyumba za kuishi. Kwa hiyo, tunaliangalia lote kwa ujumla wake. Kwa hiyo, Wizara yangu mwaka 2010 ilipitisha ile Sera ya Motisha na Mishahara na tumeanzisha Bodi mwaka 2012, imefanya kazi nzuri; imesha-*identify* Wilaya 33 ambazo zina mazingira magumu. Sehemu hizo tunaziangalia kwa upana wake kwamba mazingira magumu ni yapi. Hatuangalii motisha kwa fedha tu, tunaangalia na *parameters;* kuna mawasiliano? kuna nyumba za kuishi? Yaani ni vitu vingi. Unaweza ukampa mtu hela, lakini nyumba ya kupanga hamna.

Kwa hiyo, tunachofanya ni kujenga nyumba. Sehemu zile ambazo zina visiwa, tumenunua boti kwa ajili ya kusafirisha wafanyakazi kwenda kuchukua mishahara. Tumefanya hivyo kwa muda mrefu. Kwa hiyo, hilo la mazingira magumu tuliangalie kwa watumishi wote

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI)]*
tunapotetea na sio kwa Walimu peke yake. Kuhusu ulipaji wa madeni; mimi nitaangalia tu upande wa madeni yanayohusiana na mishahara. Ni malimbikizo ya mishahara, *increment* pamoja na *promotion.*

Kwa upande wa Serikali kwa kweli tumefanya kazi kubwa sana kulipa madeni ya watumishi wote. Sasa hivi hatubagui, hatuangalii Walimu peke yake. Kwa hiyo, Serikali naomba nisahihishe *figure* ya Kamati. Zile Shilingi bilioni 52 ni fedha zilizolipwa na Serikali kwa watumishi kuanzia mwezi Julai, 2012 mpaka mwezi Oktoba, 2013 na siyo za miaka iliyopita. Hizi ni za mwaka mmoja tu mpaka leo hii. Kwa hiyo, kwa upande wa Walimu, kuanzia Julai, 2012 mpaka Oktoba, 2013 fedha za malimbikizo ya Walimu zinazohusu mishahara, zimelipwa kiasi cha Shilingi bilioni 33. Tumefanya kazi kubwa sana, na zilizobakia kidogo kwa watumishi wengine.

Fedha ambazo ziko kwenye *queue,* kwenye uhakiki, ambazo zimeshahakikiwa ni Shilingi bilioni 4.4 za Walimu, huenda zikalipwa mwisho wa mwezi huu wa Desemba, 2013. Fedha ambazo hazijahakikiwa kwa upande wa Walimu ni Shilingi bilioni 7.8 tu. Sasa angalieni tulikotoka, tumelipa Shilingi bilioni 33, ambazo ziko kwenye *queue* ni Shilingi bilioni nne, ambazo hazijahakikiwa ni Shilingi bilioni saba tu. Mwangalie huo mzigo. Tulikotoka ni kugumu zaidi kuliko huku tunakwenda. Nasema kwamba tunaangalia kwa watumishi wote, hatuangalii kwa Walimu peke yao. Kwa hiyo, nina *data* hapa za madeni yaliyolipwa kwa watumishi wote yaliyohakikiwa na yale ambayo yanahakikiwa kwa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mfumo madhubuti sana kwa upande wa *personal emolument* kwa sasa kwa sababu Mwalimu anapoajiriwa tu, akiingizwa kwenye Mfumo na taarifa zikikamilika mwezi huo huo anapata mshahara. Kwa hiyo, malimbikizo yameanza kupungua. Akipata *promotion,* mwezi huo huo kama barua zake zikikamilika, tunamwingiza kwenye mfumo. Kwa hiyo, niwatoe wasiwasi kwamba madeni yanayohusiana na *personal*

*emoluments* yenyewe yana mfumo mzuri na tunalipa na baada ya muda madeni hayo yatakuwa yamepungua kwa kiasi kikubwa.

Kamati imeongelea kuhusu chombo kimoja cha ajira kwa Walimu. Suala hili kama Serikali tunaliangalia kwa upana wake, kwamba hatuwezi tukaangalia chombo kimoja tu kwa upande wa Walimu, lazima maamuzi yetu tuwe waangalifu sana. Kwa hiyo, tunalifanyia kazi. Kwa sababu tukisema Walimu wawe na chombo cha ajira, na Madakari watadai na wengine watadai. Kwa hiyo, ni kama tutafungua *pandora's box.* Lakini ninachosema, mwajiri wa watumishi wote ni Serikali na siyo vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kaka yangu Mheshimiwa Lusinde alizungumzia kuhusu *DDH* Mvumi kwamba hawajalipwa mshahara wao. Inawezekana hawajafanya *data cleaning*. Kwa kweli zile sehemu zote ambazo hawakuingiza majina kwenye mfumo wetu wa Serikali, wanalipwa *separate* kwa kutumia vocha. Kwa kweli ule mfumo hatuutaki kwa sababu kuna udanganyifu wa aina fulani. Kwa hiyo, baada ya kutoka hapa nitaangalia kwamba: Je, Mvumi iko kwenye kundi hilo ambalo halijafanya *data cleaning?* Ili tuweze kuangalia kwamba kuna tatizo gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, dada yangu Mheshimiwa Zabein Mhita pia ameongelea hilo la mazingira magumu. Nafikiri nimeliongelea kwa kirefu kwamba mazingira magumu tunayaangalia kwa upand wake, zimeshakuwa *identified* Wilaya hizo 33, tunaangalia tuwape motisha ya aina gani na tufanye nini ili tuweze kutoa hayo mazingira magumu. Lakini tusikazanie kwamba lazima iwe fedha. Tunaangalia mawasiliano, huduma muhimu, barabara na nyumba za kuishi watumishi wa aina hiyo. Lakini pia, kuna baadhi ya Watumishi pamoja na Walimu, wanapolipwa *arrears* zao, huwa hawaangalii. Wakiona tu mwisho wa mwezi Benki hela ziko nyingi, yeye anaona kwamba ni sawa tu, hawaendi kuangalia kwenye *salary slip.*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Kwa hiyo, niwaase kwamba watumishi wa Umma waangalie *salary slip* zao, *arrears* wakati mwingine wanalipwa lakini bado wanakuwa wanadai. Waangalie *salary slip* zao wakati mwingine wanalipwa lakini hawasemi chochote.

Mhjeshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la kuboresha maslahi ya Walimu; tunaangalia kuboresha maslahi ya watumishi wote wa Umma bila kubagua. Lakini kwa sasa Ofisi yangu inafanya *job evaluation,* yaani uzito wa kazi wa kila Taasisi na kila kada ili kuangalia mishahara hiyo ipangwe kulingana na ugumu wa kazi na ukubwa wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru. Naishukuru Kamati kwa kutusaidia kwa ushauri na mengine tunayachukua, tunayafanyia kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Celina Kombani. Namwita Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mkangala.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Naomba nianze kwa kuwashukuru sana Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii kwa Taarifa yao nzuri ambayo ilianza kueleza ziara kwa upande wa Wizara yangu; ziara ambazo zimefanyika katika nchi tano na nchi hizi ni za Asia, Malaysia, Singapore, Indonesia na China na nia ya ziara hizi ilikuwa ni kujifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa ni ahadi kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wakiwa wa Kamati yetu waweze kutumia ziara hizi kupata uzoefu kutokana na nchi nyingine wanavyoendesha masuala hasa haya ya hifadhi ya jamii, hususan masuala yanayohusu Fao la Kujitoa na Pensheni ya Wazee. Kwa sababu tulitaka kweli tupate uzoefu wa nchi nyingine na sisi tunapokuja hapa kuleta taarifa na Miswada tuweze kutumia uzoefu huo.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA KAZI NA AJIRA]*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendeleza hapo kwenye pensheni ya wazee, kwa hatua hii tuliyofikia sasa, maana wengi wamezungumza kwamba Serikali haitaki kuleta pensheni ya wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba Serikali iko mstari wa mbele katika kuhakika kwamba pensheni ya wazee baadaye inalipika. Ambacho Serikali imesema mara zote ni kwamba hatuwezi kukurupuka na hiki kitu. Tukumbuke kwamba pensheni hii ya wazee inatakiwa ilipwe kutokana na pesa ya Hazina. Siyo pesa iliyochangiwa! Ni pesa ambayo inatokana na Bajeti, iletwe hapa Bungeni, basi itolewe kwamba hii ndiyo italipika, na ilipike kila mwezi kwa wazee wale tutaokuwa tumesema sijui ni miaka 65 au 70 ilipike kila mwezi mpaka huyo mzee atakapofariki bila kuacha mwezi mmoja.

Kwa hiyo, Serikali inachosema hapa, *sustainability* yake lazima iangaliwe kwa makini. Kwa hiyo maandalizi yafanyike. Mimi naomba tuelewane hapo, kwa kweli hakuna ambaye haoni umuhimu wa hili suala. Serikali inaliona na ndiyo maana inalifanyia maandalizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshaandaa *action plan* ya suala hili. Kwa mfano sasa tumeshamaliza ziara za mafunzo, tunachofanya sasa ni kuandaa mapendekezo yanayotokana na ziara hizi. Mapendekezo ya Fao la Kujitoa, mapendekezo ya Pensheni ya Wazee, tupeleke kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini pia mapendekezo haya yatusaidie sasa kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri ili kupata idhini ya Serikali kuhusiana na suala hili. Tunategemea *by May* mwakani 2014, hii kazi itakuwa imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuandaa Muswada wa Sheria ya Pensheni ya Wazee. Kwa kweli bila sheria, hatuwezi kujua wazee tutawalipaje pensheni. Kwa hiyo, ni lazima tuje na Sheria hii. Sheria itaandaliwa na Wizara ya Kazi au itaandaliwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, lakini itaandaliwa na Serikali. Hii tumeandaa kwamba

*by June, 2014* tutakuwa tumeshamaliza. Lakini pia kuwasilisha Muswada Bungeni sasa baada ya kuandaa hii Sheria kuhusiana na ulipaji wa pensheni ya wazee, tunafikia *by December*, 2014 tutakuwa tumeshafikia hatua hii. Kwa hiyo, tunaenda hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli hili hatulifanyii mzaha maana tumeshaliweka kwenye mipangilio na ratiba hii tunaifuata vizuri. *(Makofi)*

Suala la Fao la Kujitoa na lenyewe lina ratiba yake, naomba hilo niliseme sana kwa sababu muda wenyewe hautoshi. Lakini nashukuru kwa ushauri mwingine uliotolewa kuhusu masuala ya usalama mahali kazi, Sheria za Kazi na masuala mengine ya Hifadhi ya Jamii ambayo nasema tutayazingatia.

Naomba niongelee hili la Mheshimiwa Aliko kuhusu Polisi kwamba hawapati pensheni mpaka baada ya miaka 12. Ukweli ni kwamba tuna aina mbili za Polisi. Kuna Polisi wale ambao wanafanya kazi kwa mkataba wa miaka mitatu mitatu. Wanapeana mikataba kulingana na utendaji wao, wana-*renew* ile mikataba miaka mitatu mitatu. Ikifikia kipindi cha tatu cha ku-*renew,* yaani miaka tisa akapewa *termination,* akaambiwa basi, kutokana na vyeo vyao, huyu anapewa fedha yake ya mkupuo.

Kwa sheria ya zamani ya *GEPF*, alikuwa anapewa pesa ya mkupuo anaondoka. Lakini kwa sasa hivi baada ya kubadilisha hii Sheria anatakiwa aendeleze ule mfuko wake kusudi baadaye umsaidie mbele ya safari. Lakini aki-*renew* mara ya nne, ndiyo hiyo miaka 12 hapo amesha-*qualify* kuwa *permanent and pensionable.* Kwa hiyo, anahamishiwa *PSPF,* anaendelea sasa na pensheni kukatwa pesa yake ili afikie miaka 15. Hii miaka 15 ni kiwango ambacho kiliwekwa na *actually* kwamba angalau wachangiaji wachangie kwa miaka 15 ili mifuko hii iweze kuhimili kuwalipa pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya hapo, mpaka sasa hivi tathmini haijaonesha kwamba mifuko inaweza ikahimili pensheni hizi chini ya kiwango hicho. Hata kama akichangia chini ya kiwango hicho, hawezi kulipwa pensheni mpaka afikie umri wa kustaafu. Kwa hiyo, miaka 15 imewekwa kama vile ni rula ya kusaidia kwamba sasa mifuko hii itakuwa imeshachangiwa kiasi cha kutosha na itaweza kulipa pensheni zao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda, naomba niachane na hilo la hifadhi ya jamii, lakini kwa kweli tunalifanyia kazi hasa kupanua wigo Mheshimiwa Zitto umesema, tunachukua mawazo yako mazuri kuhusiana na wakulima. Lakini mifuko hii sasa inatoa *supplementary schemes* ambazo zinawagusa wakulima, wafugaji na wengine kama nyie hapa mnachukua *supplementary schemes,* mnaweza hata mkaziendeleza baada ya kuaachana na Ubunge kusudi mbele ya safari ziwasaidie, ingawa siyo kwa ajili ya pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni ajira, hasa ajira kwa vijana. Nakubaliana na Mheshimiwa Lusinde, kwa kweli Wizara hii wengi wanafikiria ndiyo inayotoa ajira. Lakini ajira Serikalini inatolewa na Wizara ya Utumishi, Ofisi ya Rais. Wizara yangu inafanya nini?

Kwanza tukumbuke kwamba ajira, ni tunda au matokeo ya uchumi kupitia hasa uwekezaji, na hasa uwekezaji katika viwanda. Kwa hiyo, uwekezaji ukiwepo na uchumi ukikua, basi na ajira zinakua na Serikalini wamekuwa wakiongeza ajira mwaka hadi mwaka. Sasa ajira hizo haziwezi kukidhi mahitaji ya wajiriwa waliopo.

Kwa hiyo, tumefanya nini? Wengi wamesema programu tumeshaandaa. Sasa hivi tuko katika Sekretarieti ya *Cabinet.* Lakini tunasema hasa hii program hii ambayo tunafikiri ndani ya miaka mitatu itakuwa imetuletea zaidi ya ajira 800,000, tunasema mikoani kule kuwe na programu zao ndogo ndogo kulingana na mazingira.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tulikuwa na *forum* ya ajira, huwezi kuamini, vijana wameshahamasika, wameshaelewa maana ya kujiajiri na kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Nimalizie kwa kusema, sasa hivi nina *good news* kwa vijana, kwamba tarehe 4 Desemba, 2014 tulizindua kitu kinaitwa *Labour Market Information System* au Mfumo wa Taarifa wa Soko la Ajira. Mfumo huu una-*module* tatu. *Module* ya kwanza itakuwa inaweka taarifa za watafuta kazi na wale waajiri. Kwa hiyo, Waajiri watatangaza ajira zao kwenye huu mfumo. Badala ya kutangaza kwenye magazeti wanatozwa fedha, sasa wanaweza kutangaza kwenye huu mfumo wa Serikali, hawatozwi chochote vijana wanaingia kwenye mfumo, wanaona aina ya kazi, wanajiandikisha, wanatafuta ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *module* ya pili itaonesha wahitimu wa Vyuo mbalimbali, na taaluma zao, wachumi, wanasheria na kadhalika. Digrii zao, *Bachelors', Masters, Ph.D.* Hii itasaidia pia wale waajiri kuweza kuwa-*tap.* Lakini waajiri wote *private* na *public* watapata taarifa na taaluma za ujuzi na stadi adimu zilizopo nchini sasa ili kusaidia Vyuo Vikuu na Vyuo vingine vya elimu ya juu kuandaa programu kuanza kutoa hizi taaluma ambazo ni adimu nchini.

Mfumo huu umeshaanza kufanya kazi kwa *module* hii ya kwanza na ya pili hasa kwa Vyuo vya *VETA* na Vyuo vingine vya ufundi, *(technical colleges).* Kwa hiyo, nawaalika vijana sasa muanze kuingia kwenye huu mfumo kuangalia aina za ajira zinazotakiwa. *Module* ya tatu ambayo bado, kwa sababu tunasubiri kwanza Vyuo Vikuu hasa *TCU* viweze kutuwekea taarifa hizi, hii itaonesha tabia na mwenendo wa nguvu kazi *(labour force characteristics).* Maana itaonesha hata kiwango cha ukosefu wa ajira, ajira kisekta, ni sekta zipi zinaajiri watu wengi zaidi, ikiwemo wageni wanaoajiriwa na Sekta hizo; ajira kijinsia, masaa ya kazi yanayofanywa na ajira mbalimbali na sekta mbalimbali, lakini na mahusiano kazini ambayo pia Kamati imezungumzia. Ni sekta zipi ambazo zina migogoro zaidi kazini?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Kwa hiyo, taarifa zote hizi zitapatikana sasa kwenye *Labour Market Information System* ambayo tumeizindua tarehe 4 Desemba, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Gaudentia Kabaka. Kama nilivyosema, anayefuata ni Dkt. Fenella Mukangara, na atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Simba.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika. Nianze kwa kukushukuru kwa kunipa dakika hizi chache, lakini nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuzungumzia hii taarifa ya Kamati yetu. Niwashukuru Kamati kwa maelekezo mazuri akiwemo Mwenyekiti na Makamu wa Kamati pamoja na Wajumbe wote; nawapongeza pia wachangiaji mbalimbali waliochangia na hasa kwa michango mizuri iliyogusa Wizara yangu na Serikali kwa ujumla.

Sasa napenda nitumie muda mchache kuchangia hoja chache zilizovuta hisia kutoka kwa wachangiaji mbalimbali, lakini pia kutoka kwa Kamati yangu na maagizo na changamoto walizoziona zinakabili Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze nianze na *TBC.* Maelekezo yaliyotolewa kwamba ni nini kifanyike, nakubaliana nayo na nawashukuru sana wachangiaji mbalimbali; Mheshimiwa Barwany, Mheshimiwa Marombwa, Mheshimiwa Nassib, kwanza kwa kuona umuhimu sana wa Serikali kuimarisha *TBC,* kwa maana ya kuhakikisha mitambo yao iko imara, lakini pia kuimarisha mkiundombinu yake na kuhakikisha madeni ambayo *TBC* inadai Taasisi nyingine zikiwemo za Serikali yanalipwa.

Nitoe taarifa tu kwa kifupi kwamba deni la *TBC* la *Intersat* ambalo linaweza kupelekea *TBC* kutokuwa hewani,

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



limeanza kulipwa na Serikali na mpaka sasa hivi tumekwishalipa Shilingi milioni 200. Lakini pia *TBC* yenyewe imechangamka na kuweza kulipa Shilingi milioni 100 mpaka sasa. Lakini sasa nichukue nafasi hii niseme kwamba *TBC* na yenyewe pia hailipwi. Kwa hiyo, ninachokiomba, nihimize wale ambao ni wadaiwa sugu wa *TBC* ikiwemo pia na Bunge, basi tujitahidi tuilipe *TBC* ili tuweze kukamilisha kutoa huduma zake vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kuweza kutenga hizo Shilingi bilioni sita kwa makusudi kabisa kuhakikisha *TBC* inapata nafasi ya kujiimarisha. Lakini pia tatizo ambalo linajitokeza na nadhani hili wameweza kulizungumzia hasa Kamati na kuliona hilo, ni dhamana ya Serikali ambayo bado *TBC* inaiongojea na Wizara inaingojea kwa hamu ili kusudi *TBC* iweze kupata *Concessional Loan* toka Benki ya China ili kuwezesha *TBC* kutekeleza majukumu yake kikamilifu hasa katika kumalizia masuala haya ya *digital* nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukipata *Concessional Loan* kwa *TBC* itaweza kuboresha *TBC* vizuri na katika kupitia *Concessional Loan* kuna uwezekano wa kupata Shilingi bilioni 34 mpaka 40 na hizi zitaweza kupatikana kwa kupitia *Concessional Loan*. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kwa kusema kweli niombe sana tusaidiane na Serikali iweze kuliangalia hili kwa karibu na huko tuliko tunajitahidi kuhakikisha kwamba Serikali inaona hili ni la muhimu la kuweza kutoa hiyo dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limejitokeza na hoja nyingine ni Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Kumekuwa na maswali kwamba hiyo pesa iko wapi na inapatakana vipi kama imeshaingia kwenye mfuko? Hili limeulizwa na Mheshimiwa Makilagi. Niseme tu kwamba katika bajeti ya mwaka huu kumepangiwa Shilingi bilion 6.1, nieleze tu kwamba uko mwongozo unaotumika kutumia hii pesa ya mfuko wa vijana na huo mwongozo uko katika maeneo ya uainishaji wa miradi, usimamizi na ufuatiliaji wa mikopo.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Kwa kifupi, Mwongozo huu umeshatumwa kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri na inatoa fursa ya kutoa mikopo kwa vijana ndani ya *SACCOS* za Wilaya kwa maana kwamba vijana katika kila Wilaya wanatakiwa kujiunga katika *SACCOS* na kwa kupitia huo mfuko pia kuna uimarishwaji na uanzishwahi wa *SACCOS* za Wilaya na vikundi vya vijana. Wakifikiwa wale vijana, hupewa mafunzo kwa vikundi mbalimbali. Katika hili, Wizara imeshawasiliana na Makatibu Tawala wa Mikoa yote ya Tanzania. Hili lipo, linafanyika hivi ninavyozungumza, Wilaya mbalimbali zimeshafikiwa na Makatibu Tawala mbalimbali wameishanufaika na vijana kwa kiasi kikubwa wameshajipanga katika Wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba vijana wachangamkie fursa hizi, Mfuko huu ni wa vijana wote mpaka wa Vyuo Vikuu wenye uhitaji na waliojipanga. Hili litafanyika kulingana na uwezo wa mfuko. Kama nilivyosema, changamoto bado inatokana na ile kutokupata hizi fedha mapema, lakini kiasi cha kujipanga tayari tumeshajipanga na kiserikali bado tunaendelea kufuatilia kuweza kupata hizi pesa kwa wakati.

Suala lingine ambalo limejitokeza na limezungumzwa kwa kiasi ni kuhusu Muswada wa Vyombo vya Habari. Sasa na hili tumeagizwa tuhakikishe kwamba tunalileta mara moja hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwajulisha Bunge lako Tukufu kwamba kimsingi Balaza la Mawaziri lilisharidhia kutungwa kwa Sheria hiyo ya kusimamia vyombo ya Habari. Wizara husika ikishirikiana na Mwanasheria Mkuu, imeshaandaa rasimu ya Muswada wa Sheria na Vyombo vya Habari na taratibu zinafanyika kuirejesha tena Baraza la Mawaziri kwa maamuzi ili Muswada huo uweze kuletwa Bungeni. Kimsingi, huo Muswada wa Vyombo vya Habari utahusu masuala mbalimbali, ikiwemo na uanzishwaji wa Bodi ya taaluma ya waandishi Wanahabari, utoaji wa ithibati kwa wanahabari, usajili wa vyombo vya wanahabari, uanzishwaji wa mfuko maalumu kwa mafunzo

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



ya wanahabari. Kwa hiyo, kimsingi, waandishi kiujumla watakuwa wanafaidika kwa kiasi kikubwa kuweza kuwakuza katika tasnia yetu hii ya Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa suala lingine ambalo limejitokeza ambalo nahitaji nilizungumzie, ni hoja kuhusu mporomko wa maadili katika filamu na uharamia katika kazi za wasanii. Sasa kwa kiasi kikubwa kwa upande wa mporomoko wa maadili, Bodi ya Filamu inaendelea na itaendeleza kufanya *operation* za mara kwa mara za kuondoa sokoni Filamu zinazoingia humo bila kukaguliwa zikiwemo zisizo na maadili. Lakini pia Bodi ya Filamu inaendela kukazia utekelezaji wa Sheria ya Filamu na Michezo ya kuigiza na kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Filamu pia inawaita na kufanya nao vikao wale wanahusika katika maeneo yaliyokithiri katika uvunjaji wa maadili na kutoa makaripio. Bodi pia inaziwekea madaraja Filamu zote ili kuainisha Filamu zipi zinapaswa kuonwa na umri gani. Kwa wale ambao wanaendelea kukaidi, hatua dhidi yao zinaendelea kuchukuliwa kwa mujibu wa Sheria. Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa mwitikio umekuwa mzuri, Filamu nyingi sana zimekuja katika Bodi ya Filamu ili ziweze kukaguliwa na zimeweza kuingia sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa upande wa masuala ya kiharamia, kwa maana ya kuanza kutumia miziki mbalimbali ya wasanii bila ruhusa katika mitandao ya simu, hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kuanzisha utaratibu wa kubandika Stempu za Kodi katika bidhaa za Filamu ili kubaini kazi halali na feki. Stempu zinazotumika katika kazi za Filamu na muziki zimetengenezwa na wataalamu wa hali ya juu na kuziwekea alama za siri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Stempu hizo, zinafanyika nje ya nchi, hivyo siri za utengenezaji wake haziingi katika mikono isiyo salama. Nalisema hili kwa sababu ilijitokeza wakati wa kuchangia kwamba ziko kazi zinazunguka na stempu ambazo ni za bandia. Sasa zile zinazozunguka ni

katika mitazamo tofauti, tumeweka watu maalumu ambao wanaweza kuzifatilia na kuweza kuwashika wale ambao wanahusika na kuweza kupewa adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Serikali imeweka mikakati gani kudhibiti nyimbo za wasanii na vifaa vya mawasiliano kwa mfano simu za mikononi? Nyimbo nyingi za wasanii zinazotumiwa katika vifaa vya mawasiliano zinaendelea kuwanyonya wasanii kotokana na mikataba ambayo tayari wasanii hao wameshaingia, hivyo kuna haja ya kukaa na wadau na kuona nini cha kufanya.

Hata hivyo, Serikali kupitia urasimishaji ambao tumeshazungumza, imeandaa mikataba bora inayoonesha bayana namna kazi za filamu ama muziki zitakavyotumiwa katika mifumo ya mawasiliano itakavyomwezesha mhusika kupata stahiki. Basi tunaomba wale wanaohusika wahakikishe wanatumia hizi Sheria na kuwasiliana na Bodi ya Filamu ili kusudi kazi zao ziwe katika hali nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo Mheshimiwa Kabaka ameigusia kwa kiasi ni hoja hii ya ajira kwa vijana. Niseme tu kwamba Serikali imeshachua hatua mbalimbali kukabili tatizo la ajira kwa vijana. Nampongeza pia Mheshimiwa kwa kuja na hii *Labor Marketing Information System,* ni jambo kubwa na zuri sana ambalo Serikali kwa kiasi kikubwa imekuwa ikihangaika nalo, na ni jambo kubwa ambalo Wizara ya Kazi na Ajira sasa imeanza kulishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira kwa vijana limepewa kipaumbele kuwemo katika mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Serikali imeongeza fedha katika Mfuko wa Maendeleo kama mnavyoona, tumeweza kupata sasa hivi Shilingi bilioni sita. Lakini ziko sehemu mbalimbali ambazo masuala ya ajira mbalimbali katika kila Wizara yanaendelea kutengenezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuwajengea vijana mafunzo ya ujasiriamali, uanzishaji na undeshaji wa miradi endelevu, ufuatiliaji wa masoko,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



utunzaji wa kumbukumbu za miradi, uongozi katika vikundi, uanzishaji, uendeshaji na usajili wa vikundi vya uzalishaji pamoja na Makampuni ya vijana na elimu ya stadi za maisha kwa kushirikiana na TAMISEMI. Wizara yangu inaendelea kuhimiza Idara na Taasisi mbalimbali kuhuisha masuala ya ajira kwa vijana katika sera na mikakati yao ya utekelezaji, shughuli za maendeleo katika sekta zao...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dkt Mukangara.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Ya pili imeshalia?

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Sophia Simba atakuwa mchangiaji wa mwisho kwa upande wa Waheshimiwa Mawaziri. Ajiandae Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia hoja hii muhimu, hoja ya Taarifa ya Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii.

Kwanza kabisa, napenda kuwashukuru sana kwa jinsi walivyotuelekeza na jinsi wanavyojitahidi kuhakikisha kwamba Wizara yetu inashika nafasi yake mtambuka ndani ya jamii. Aidha, nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge, kwani wametoa michango mizuri sana ya kuboresha kazi zetu, nawashukuru sana.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika sana kuona Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumzia suala la Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF).* Tumepokea ushauri wenu na tunatekeleza yale ambayo mmetushauri hasa tukikumbuka jinsi gani mlifanya kazi kubwa sana kuhakikisha mfuko huu unafufuka tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwafahamisha kwamba Mfuko huu umekuwa unaendelea kwa muda mrefu, pamoja na kwamba kwa muda mrefu tulikuwa hatupati *allocation* yoyote tokea mwaka 2005. Hatukupata *allocation* lakini umekuwa ukizunguka, pamoja na kwamba ulikuwa ukisuasua lakini kazi ilikuwa ikifanyika. Sasa kwa vile tumepata hizi Shilingi bilioni mbili tunataka tuwahakikishie kwamba tutashirikiana nao kuhakikisha kina mama wanapata hiyo mikopo ambayo wanastahili, ni haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuishukuru sana Kamati yetu pamoja na Wabunge wote kwa kuhakikisha kwamba tumepata Shilingi bilioni mbili. Niseme tu kwamba kwa kwa bahati nzuri tayari Serikali imeanza kutoa fedha kwa ajili ya Mfuko huu, tumeshapata Shilingi milioni 500. Kwa hiyo, tumeanza mchakato wa kugawa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tumeulizwa ni mpango gani tuliokuwanao wa kuboresha jinsi ya kutoa hiyo mkopo? Hii Kamati yetu tumekaa nayo, imetupa mwongozo mzuri na tumekubaliana kwamba kwa mwaka huu katika hizi Shilingi bilioni tano, tutatoa kiasi cha Shilingi milioni 12 kwa kila Wilaya, na zile Wilaya Mpya tutazipa Shilingi milioni nane nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba Shilingi milioni 12 ni *penalty* ukiangalia ukubwa wa Wilaya na ukubwa wa shida ya kupata hii mikopo. Kwa hiyo, sisi tunapoleta tunategemea Waheshimiwa Wabunge ni chachu ya nyinyi kuhakikisha kwamba ile 5% ya *own sources* inakwenda inatolewa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



inaingia kwenye mfuko huu. Kwa hiyo, mfuko utakuwa mkubwa zaidi, akina mama watapata mikopo zaidi na ile *five percent* nyingine itoke ili iende kwenye Mfuko wa Vijana. Hili liko katika uwezo wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, tusikubali kupitisha bajeti bila ya kuona zile *five percent* ya vijana na *five percent* ya wanawake. Ikumbukwe tu kwamba hizi hazitoki kwa mara moja. Kama hivi tulivyopata sisi kidogo, tumepata robo ya zile pesa. Zitakuwa zikitoka kidogo kidogo. Kama zikitoka kidogo kidogo, hata ule uchungu ambao Halmashauri inaona wa kuzitoa kuweka katika Mfuko wa akina mama utapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine limezungumzwa kuhusu urejeshaji. Ni kweli urejeshaji sio mzuri na inaeleweka. Huu mkopo ulipoanza kutolewa mwaka 1993 wengi waliuona kama ni mkopo wa kisiasa hivi, na walikuwa hawakupata elimu vizuri.

Kwa hiyo, sisi tumesema tunazaliwa upya, tunahakikisha kwamba elimu inawafikia, ndiyo wanapata mkopo.

Kwa hiyo, wale ambao hawajalipa, tunawaomba sana warudishe ile mikopo, lakini hatutawaadhibu kutokana na kutokuwa na elimu ya ujasiriamali ambayo waliikosa wakati ule. Kwahiyo, tunaomba sana mwendelee.

Mheshimiwa mmoja alisema tuwapeni mjue ni kiasi gani Wilaya mbalimbali mnatakiwa kurejesha. Hilo tutalifanya mara moja kwa sababu hizo taarifa tunazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, pamoja na kwamba hazijarudishwa, ni za siku nyingi, zikirudishwa zitasaidia ule mfuko kuzidi kuzunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limezungumzwa sana ni kuhusu Benki ya Wanawake,

nashukuru sana mmelizungumzia na siku zote mmekuwa watetezi wa Benki ya wanawake. Benki ya wanawake mpaka sasa hivi ina matawi mawili tu Dar es Salaam. Lakini tayari ina madirisha 55 nchi nzima ya kutoa mikopo. Madirisha hayo yapo maeneo mbalimbali. Madirisha hayo yako Dar es Salam, Mwanza, Dodoma, Arusha, Pwani, Moshi, Mwanga, Kibaha na Nachingwea. Sasa tunapeleka hayo madirisha Mbeya na Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba kufungua Branch ya Benki tunahitaji Shilingi milioni 500. Kwasababu unapofungua Benki, unahitaji *technology*, unahitaji *Standby Generator, furniture*, *strong room* na *bullet proof teller stations.* Kwa hiyo, haiwezekani kufungua hizi *Branches* kila mahali. Kwa hiyo, haya madirisha ambayo mengi tumeyafungua kwenye maeneo kama zilizokuwa Posta, yanafanya kazi nzuri sana, na tunatoa huduma kwa gharama ndogo sana zaidi. Kwa hiyo, naomba sana mwendelee kutumia huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge ni kwamba sasa Benki Kuu wametukubalia kuuza hisa. Naomba sote tununune hisa ili kutunisha Mfuko huu wa Benki yetu. Jinsi tutakapotunisha ndiyo jinsi tutakavyoweza kutoa mikopo. Tunahitaji kuwa na mtaji mkubwa zaidi, sisi tuwe wa kwanza kununua hisa na wadau wetu huko katika Majimbo yetu tuwaoneshe umuhimu wa kununua hisa katika Benki yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna huduma ambazo tunatoa tayari. Kwa mfano, tunatumia pia huduma ya M.pesa, tunatumia pia *ATM cards* kwakutumia *Umoja Switch.* Kwa hiyo, tuko mbali, tunaenda kidogo kidogo lakini tutafika. Zanzibar tumeshafanya mazungumzo na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kupata sehemu ya kufungua kama tulivyosema, nia tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka sana nizungumzie kuhusu matatizo ya unyanyasaji wa watoto, ukatili dhidi ya watoto na hiyo ndiyo inasababisha kuwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



na watoto wengi wa Mitaani. Watoto hawa wamekwenda Mitaani kukimbia ukatili kwenye nyumba, majumbani mwetu.

Nachanganya hapa na yale aliyosema Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, kila siku maovu makubwa yanaanzia nyumbani, tunashindwa kulea watoto wetu vizuri, watoto wanakimbia, wanakwenda Mitaani. Watoto wananyimwa chakula ndani ya nyumba, watoto wanapigwa sana, unakuta mtoto amekatwa sikio eti ameiba kipande cha nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii kazi ni ya jamii. Kuna utovu wa nidhamu ndani ya jamii. Kwa hiyo, ni kazi yetu wote, ni kweli familia inatakiwa ichukue hatamu kabla hajatoka popote ndani ya familia. Katika Wizara yetu, kuna Kitengo cha Familia ambacho kinafanya kazi hii. Tunazungumzia masuala ya *Early Childhood Development,* toka mdogo unam-*treat* namna gani? Tunasema mtoto toka yuko tumboni unaongea naye.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto jinsi tunavyowalea ndivyo wanavyokua. Toka akiwa mdogo, ukimtukana atakuwa na matusi. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Msigwa amesema hilo lakini ajue tunacho hicho Kitengo na kila mwaka tunaungana na wenzetu duniani kupitia Umoja wa Mataifa, tunaadhimisha Siku ya Familia Duniani ya tarehe 15 Mei, ya kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii nami niwakumbushe Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kutumia Halmashauri zao. Watoto wale ni watoto wa ile Halmashauri. Kila Halmashauri ihakikishe watoto wake hawako barabarani. Wale watoto waliokuwepo Dar es Salaam ni jukumu la *City Fathers* wa Dar es Salaam kuhakikisha watoto wale hawapo tena Mitaani.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Ni kengele ya pili hiyo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii - Mheshimiwa Mama Margaret Sitta. Karibu sana Mheshimiwa, muda wetu ni mdogo, jitahidi sana, usizidishe dakika 25.

**MHE. MARGARET S. SITTA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nihitimishe kwa niaba ya Kamati ya Huduma ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kabisa, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango mizuri, Kamati imepokea na kuithamini. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni vyema nikazungumzia kwanza kwa ujumla, kwa Wizara zote mbili ni mambo gani muhimu yamejitokeza, kabla sijaingia kwa undani zaidi. Kwa upande wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge waliochangia mambo makubwa mawili yamejitokeza.

La kwanza, inatakiwa kuboreshwa elimu, yaani elimu lazima iboreshwe kutokana na michango ya Waheshimiwa Wabunge. Pili lililojitokeza ni kwamba kuna umuhimu wa kuwawezesha vijana wetu kupata *study* za kuwawezesha kupata kazi za kujiajiri au kuajiriwa. Ndiyo mambo makubwa yaliyojitokeza hapa. Lazima tuboreshe elimu, lakini pia tuwawezeshe vijana wetu kupata *study* za kazi waweze kujiajiri au kuajiriwa.

Kwa upande wa afya mambo mawili, matatu yamejitokeza. La kwanza ni kwamba bado huduma za afya

zinahitajika kuboreshwa mijini na vijiji, lakini la pili ni kwamba bado tuna tatizo la uhaba wa dawa na la tatu, tuna uhaba mkubwa wa wafanyakazi maeneo ya vijijini. Hayo ndiyo yaliyojitokeza kutokana na michango ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na Wizara ya Elimu, mimi nilifikiri msemo wa Mwalimu Nyerere Marehemu, ni kwamba kupanga ni kuchagua Kwa hiyo, tuliamini kwamba Maabara iliyokaa huko ikafanya kazi, ikachagua Wizara Sita ili zitoe Matokeo Makubwa Sasa, ndiyo maana na sisi Kamati ya Huduma za Jamii, mapendekezo yaliyotoka ukiyaangalia kwa msingi ndiyo tumeanza nayo, yanajaribu kuishauri Serikali ili ipate matokeo makubwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kupata matokeo makubwa sasa usipomshughulikia Mwalimu. Hilo ndilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kuboresha elimu, tunajua, la kwanza ambalo Wizara ya Elimu imelitambua kutokana na kitabu chake cha Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, ni kuwezesha zile KKK; Kusoma, Kuandika na Kuhesabu, ndiyo utajenga msingi imara wa vijana kabla hawajafikia darasa la nne, wawe wamejua kusoma, kuhesabu na kuandika. Kwa msingi huo, kujenga msingi mkubwa wa kuelewa masomo yote kwa kadri watakavyoendelea na elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo, kama unataka kweli watoto wetu wapate misingi mitatu hiyo, lazima Walimu nao waandaliwe katika misingi hiyo hiyo mitatu, ili waitoe kwa taaluma inayostahili, kwa uwezo wa hali ya juu ili watoto kweli wapate hiyo misingi mikuu mitatu; Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Ndiyo maana ushauri wetu sisi, umemwanzia Mwalimu kwamba Mwalimu ndiye aandaliwe vizuri. Kwanza, kwa kuchagua wanafunzi wanaojiunga na Vyuo vya Ufundi; sifa ziongezwe ili wanaoingia kwenye Mafunzo ya Ualimu wawe ni vijana waliofaulu; pili Vyuo vya Ualimu navyo viangaliwe ili kweli

yule Mwanafunzi anayekwenda pale apate mafunzo ya Masomo yenyewe, yaani *Subject Competence* lakini pia apate namna ya ufundishaji, yaani *Methodologies.*

Pia tumeona kwamba kuna umuhimu wa kuangalia mtaala wenyewe wa Vyuo vya Walimu ulivyo kama unakidhi kuandaa vijana wetu wawe Walimu bora, basi inafaa. Lakini tumeona ni vizuri la kwanza kabisa tuangalie maandalizi ya Mwalimu. Lakini pia tumeona Mwalimu akishapata *study* nzuri akawa Mwalimu mzuri amefundishwa vizuri, akatoka nje sasa kwenda kufundisha, lazima na yeye aangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tulikwenda ziara ya Wajumbe wapatao kama sita hivi kutoka kwenye Kamati yangu. Tulikwenda kwenye nchi ambayo imeendelea sana kwa upande wa Elimu, namshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule tulijifunza kwamba umuhimu walioweka wakafikia hatua ya kuwa miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa elimu duniani, walimshughulikia Mwalimu kwanza. Wakasema wenyewe kwamba mtumishi anayeheshimiwa katika nchi ile ni Mwalimu.

Kwa msingi huo wakaweka na viwango kwa nchi hiyo tuliyokwenda. Hakuna Mwalimu kuingia Darasani bila ya kuwa na *Masters Degree.* Sasa sisi hatuwezi kufika huko. Lakini waliweka kiwango kwamba hakuna Mwalimu kuingia darasani chini ya kiwango hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, walivyowezesha vile, wamemfanya Mwalimu aaminiwe, athaminiwe, lakini pia mpaka wameondoa Wakaguzi kwa jinsi ambavyo wamemwandaa yule Mwalimu. Sisi tuliona ni kweli ni kitu kizuri. Ukitaka kufanikiwa kwa upande wa elimu, lazima umwandae Mwalimu. Lakini hata akiingia kazini, basi mpe haki zake, mwangalie kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, kwa kuwa Elimu ni miongoni mwa Wizara sita ambazo zinategemewa kutoa *Big Results,* yaani Matokeo Makubwa Sasa, tumeona ni lazima umwangalie Mwalimu kwa karibu. Walimu wanayo matatizo mengi, wenzangu wameongea. Walimu wana matatizo mengi. Tutapata *Big Result,* wakati watu wananug'unika, wanafuatilia mishahara yao kila siku? Wanakwenda kila siku kufuata madeni, kila siku wanatafuta kupandishwa madaraja, hawajapata fedha za likizo! Utapata *Big Result* mtu ananung'unika, sijapandishwa daraja miaka mitatu minne, kama alivyosema Mheshimiwa Zabein Mhita! Ndiyo tumeona kuna umuhimu wa kuangalia jinsi ya kuwahudumia Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu Nyerere alisema, mtu ukiona umekosea, unaweza kurudi nyuma. Serikali inaweza kuangalia, nchi hii hii ilikuwa na Tume ya Walimu, kitu gani kilifanya mpaka wakaondoa? Kulikuwa kuna matatizo gani? Kama Serikali itaona kwamba waliondoa kwa bahari mbaya, wanaweza wakarudisha Tume ya Ajira ya Walimu ikafanya kazi. Tume ya Ajira ya Walimu tunajua ikiwa chombo kimoja itasaidia. Sisi wote tumeguswa hapa. Tumekuwa tukiwaona Serikali kuhusu chombo cha Walimu kwamba kiwepo ili kupunguza matatizo ya Walimu. Kuona suala la Ukaguzi liwe Wakala, na wametupokea, wametukaribisha na kusema tunafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa tunayoipata sasa hivi inaanza kututia wasiwasi. Serikali ingesema basi, kwamba hili suala hatulitaki, ikajulikana. Au haliwezekani; au suala hili tunalishughulikia kwa utaratibu huu, tukajua. Lakini kwa jinsi ambavyo tumekuwa tukikaribishwa na kulielewa na kupewa taarifa, ilikuwa inaonekana kama Serikali imeanza kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kazi yetu ya Bunge ni kushauri. Lakini tunashauri kwa sababu ya wale tunaowawakilisha, wanayotutuma tunayaleta Bungeni. Lakini bado tunasema kama Kamati tutaendelea kufuatilia hili suala. Kwa sababu mpaka tulikwenda ngazi za juu kuona

mfumo wa kuhudumia Walimu; bado ni mbovu tukubali, haujatosheleza hata kidogo! Napenda kurudia kwa niaba ya Kamati, *Big Result* bila kumwangalia Mwalimu haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema basi, Mwalimu akishafundishwa vizuri katika Vyuo vya Ualimu, akiingia darasani apewe haki zake. Lakini isiishie hapo! Mwalimu akishaingia darasani aendelee kupata mafunzo kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii, hii, Wizara hii hii ya Elimu ilikuwa na Mpango Maalum wa Miaka 10. Mwaka 1970 – 1980, kulikuwa na Mpango wa 10 ya kuendeleza Walimu, uliokuwa unaitwa MTUU, yaani *Tanzania UNESCO* ya *UNICEF*, ambao walikuwa wanawafundisha Walimu; walikuwa wanakwenda Kasulu na Kabanga kuimarisha zile KKK, na hata kuwafanya waliokuwa wakati huo Darasa Saba, au *Grade "C",* wafanye miaka miwili kupandishwa kuwa daraja *"A".* Hasa ndiyo hayo mambo ambayo tunasema Serikali iangalie irudishe Mpango Maalum wa kuendeleza Walimu. Kwa sababu haiwezekani mtu akitoka tu Chuoni, basi biashara imekwisha. Aendelee kueleimishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, bado sisi tunasema, Serikali yenyewe imeichukua elimu kama *Big Result,* na sisi kama Kamati tulikuwa tunasema, hebu ije siku moja iseme Elimu Kwanza. Kwa sababu Elimu ndiyo nguzo ya taaluma nyingine zote; afya, uchumi na kadhalika. Ifikie hatua basi waseme Elimu Kwanza. Kwa msingi huo, kama utasema Elimu Kwanza na Walimu waangaliwe mazingira magumu wanakofanyia kazi illi waweze kukaa huko kama sehemu ya *Retention Scheme,* au utaratibu ambao utawawezesha kubaki katika maeneo hasa ya pembezoni. Kwa hiyo, Walimu waandaliwe posho ya Mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tungependa sana Serikali ituambie, zile posho za Walimu wa mwaka 2012/2013 zilizopangwa Sh. 500,000/= kwa walimu hivi zilitumikaje? Kwa

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



sababu tulifikiri Serikali ilikubali wazo la mazingira magumu. Zile fedha zilizotolewa zilitumikaje? Je, Serikali ilibadilisha msimo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ilikuwa Walimu kulipwa madeni. Sidhani kama ni kitu kizuri sana kusema tutalipa, tutalipa. Nadhani kitu kikubwa ni kuangalia chanzo chake ni nini? Tunajua, haiwezekani hata siku moja Walimu wasiwe wanadai, lakini uangaliwe utaratibu ambao unaweza kupunguza ili madeni yao yasiwe makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nalirudia ni suala la ukaguzi. Sasa hivi Shule za Msingi ni 16,412; Shule za Sekondari ni 4,731; Vyuo vya Ualimu ni 125; kati ya hivyo 91 vya watu binafsi. Sasa unaangaliaje Walimu wanavyofanya kazi katika maeneo hayo bila kuwa na ukaguzi imara? Kwa hiyo, sisi tunasema kwamba, ukaguzi lazima uwe Wakala ili usimamie hili suala la ufundishaji. Unaweza ukamfundisha Mwalimu vizuri sana, ukamlipa posho zake vizuri sana, lakini bado kuna haja ya kumfuatilia Mwalimu na kuona jinsi ambavyo anatekeleza wajibu wake. Kwa hiyo, Ukaguzi bado tunasema lazima ujitegemee uwe Wakala.

Suala lingine ambalo limezungumziwa na Waheshimwia Wabunge waliochangia, bahati mbaya kwa sababu ya muda siwezi kuwataja lakini nawaheshimu, linahusu mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafunzo ya Ufundi kama tulivyosema sisi hatutoi ajira nyingi kutokana na kutokuwa na viwanda vingi. Lakini ukiwa na stadi itasaidia. Sasa kumetolewa mapendekezo hapa kwamba *VETA* iungane na Jeshi la Kujenga Taifa, lakini na sisi tumesisitiza kama Kamati, kwamba waungane vizuri kama alivyosema Mheshimiwa Waziri alipokuwa anachangia, kwamba wahusishe pia Vyuo vya Maendeleo ili wanafunzi wengi zaidi waliokosa kazi nyingine, angalau waendelee kupata mafunzo ya ufundi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni la mfumo wa upangaji wa madaraja. Kamati ilisema hivi, kuna umuhimu kweli wa kuangalia upangaji wa madaraja na alama za ufaulu. Lakini tulisema ni vizuri Baraza la Mitihani likahusika kikamilifu kwa sababu lenyewe ndilo lenye Sera ya Mitihani kutokana na Sheria iliyounda. Huu utaratibu unaotumika sasa hivi wa haraka haraka haujapitia kwenye Baraza la Mitihani. Sisi msimamo wetu kama Kamati ya Huduma za Jamii, ni kwamba tunashauri Serikali itumie utaratibu uliotumiwa mwaka 2012, kwa mitihani itakayofanywa sasa hivi. Utaratibu ubadilike baada ya hatua zote kukamilika kwa kuhusisha kikamilifu Baraza ambalo lina jukumu hilo kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni hili linalohusu watoto wenye Ulemavu wa Ngozi wanaokaa kwenye Vituo vyao. Tulikwenda sisi Busangija. Ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Barwany kwamba mazingira siyo mazuri. Kusema kuwarudisha makwao, Kamati imesema hapana. Wasirudishwe makwao; tuiombe Serikali iwawezeshe wakae pale. Wazazi wao wamewaleta pale kutokana na usalama. Kwa hiyo, Kamati inasema, Serikali iwezeshe, waishi maisha mazuri pale, wasirudishwe, watakosa elimu.

Mhehimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna suala la Elimu Jumuishi. Kamati inasema kwamba kuwachanganya watoto wasiona, watoto ambao hawawezi kusikia vizuri, wenye uoni hafifu, kuwachanganya wote; kwa kweli hili suala Serikali iliangalie upya. Lakini badala yake kwa sababu wengi; kwa mfano, mtu anayetaka alama, achanganywe kwa kweli na wengine ambao hawaoni, inakuwa vigumu sana kumpata Mwalimu anayeweza kufanya yote hayo. Lakini tunaomba kwamba Walimu wa Elimu Maalum waandaliwe ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu nizungumzie suala la afya kabla sijapigiwa kengele. Tumeona kwamba kwa kweli mtu ni afya. Kwa kweli bila afya huwezi kufanya kazi. Bado tunaishauri Serikali, na hili nawaomba Waheshimiwa

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Wabunge, wakati wa Bajeti mtusaidie. Mtu ni Afya. Ikija Bajeti ndogo hapa, tuungane. Hali kadhalika na elimu. Sisi Wizara zetu hizi kwa kweli ni muhimu, kwa sababu pamoja na kwamba afya haikuwekwa kwenye *Big Result,* lakini mtu ni afya. Tusaidiane, Serikali iongeze pole pole mpaka ifikie asilimia 15. Mtu ni afya bwana, wanasema *a health in mind in a health body.* Huwezi kufanya kazi kama unaumwa bwana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Naibu Waziri Dkt. Seif, ameelezea, lakini Serikali ilipe. Kamati ya Huduma za Jamii imependekeza kwamba, tunapolipa madeni ya *MSD* kidogo kidogo, tunawafanya washindwe kutekeleza wajibu wao ipasavyo. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali, ifikirie kulipa Shilingi bilioni 42 kwa mkupuo. Sidhani kama ni jambo kubwa sana kama Serikali itaamua hivyo. Tunaisihi Serikali kwa kweli ilipe deni hilo kwa mkupo mmoja ili *MSD,* iweze kusambaza dawa vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Watumishi Vijijini. Mpango uliopo sasa hivi, umeshindwa kuhakikisha watu wanapatikana vijijini. Mheshimiwa Agripina Buyogera ni Mjumbe wa Kamati yetu. Ametupa mfano mzuri sana, kwamba kwao walikuwa na Wakimbizi huko Kigoma. Wakimbizi wengi sana! Wakaona tunapataje huduma hizo? Wakachukua vijana wa pale pale, huko huko Kasulu. Wakaenda wakawafundisha ili waweze kumudu mambo ya kuzalisha akinama, malaria, kuharisha, haya maradhi madogo madogo haya.

Sasa kama Wizara ya Afya walikubali wale watu wakawatibu watu, basi tunaomba Wizara ya Afya iangalie mpango ambao utawezesha kuwapata watu kutoka katika maeneo hayo hayo, kuwapa mbinu huko huko, wafanye kazi kama alivyokuwa akizungumzia Mheshimiwa Marombwa, kwamba mbona walianza kama *RMA,* wakafanya kazi vizuri, baadaye wakainuliwa! Lakini kuacha Zahanati ambazo zimekwisha, hazina watumishi, kwa kweli siyo jambo zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba suala la Watumishi, Wizara ya Afya, hebu ibuni mpango mwingine wowote ule ambao pia tumeuona sehemu nyingi. Nashukuru na pia Waziri wa Afya – Mheshimiwa Dkt. Mwinyi, tulikwenda naye tukaona, maeneo ambayo wanawatoa wafanyakazi vijijini huko huko, wanawafundisha, wanabaki huko huko na kuwapa Mkataba ili wakae vijijini, kuliko hali ilivyo kwa sasa Zahanati nyingi zimekwisha, lakini hazina watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni lile ambalo alilizungumzia Naibu Waziri wa Afya - Mheshimiwa Dkt. Seif na sisi tunaliunga mkono, tunaomba liongezewe nguvu hili suala la *E-Health* yaani kutumia teknolojia ya kisasa kufuatilia matibabu ya mgonjwa ili waone dawa zilizotumika kwa ajili ya kupunguza ubadhirifu wa dawa na vifaa vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka Mheshimiwa Lingstone alizungumzia sana juu ya mwingiliano wa majukumu. Hili nadhani tuiachie Serikali iliangalie. Tunaishukuru tena Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; tulikwenda Ghana, tukaona jinsi ambavyo afya inatolewa na chombo maalum kabisa. Walijaribu hii mitindo yetu ikashindikana. Wakaitoa afya kwenye Wizara ya Afya, wakaitoa Afya kwenye utaratibu wa TAMISEMI, wakaunda chombo kingine kabisa, *Health Authority*, kitu cha namna hiyo. Yaani *Ghana Health Authority,* ambayo yenyewe ndiyo inayoendesha masuala ya afya. Kwa hiyo, na sisi Serikali inaweza kuangalia: Je, mfumo tulionao wa mwingiliano tunaweza kuuboresha au tuanzishe mfumo mwingine ambao utawezesha watu kupata haki zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa nimepitia haraka haraka na kwa kuwa bado ninao muda kidogo ngoja nirudi kwa upande wa suala la matumizi ya lugha ya kufundishia. Turudi kwenye Elimu tena kwa sababu vyote tunavishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyojua sasa hivi lugha za kufundishia ziko mbili, Kiswahili na Kiingereza. Kwa kuwa tunasubiri Sera ya Elimu ambayo ndani yake tunaamini

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



itafafanua lugha za kufundushia, sisi kama Kamati ya Huduma za Jamii, tunashauri kwamba kwa sasa hivi wakati bado tunasuribiri ufafanuzi wa Sera, lugha zote hizi mbili vifundishwe vizuri mashuleni ili wanafunzi wazimudu vizuri. Sera ya Elimu itakapokuja itakavyofafanua tutaiona. Lakini hadi sasa sisi tunapendekeza kwamba lugha hizi mbili zifundishwe vizuri ipasavyo.

Suala lingine ambalo alikuwa amezungumzia Mheshimiwa Nyangwine, la kuhusu matumizi ya rada, hilo nadhani Serikali italitolea jibu kwa wakati wake, kwa sababu ni suala ambalo tuliona lilishughulikiwa na Kamati ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine mengi kwa kweli tumeyajibu, tunasisitiza tu kwamba jamani, Wizara ya Elimu imo katika mpango wa Matokeo Makubwa Sasa. Tunaomba yote tuliyoshauri sisi wayaone, lakini yalilenga katika kuwezesha Serikali kufikia Matokeo Makubwa Sasa, kwa kumwangalia Mwalimu na mwanafunzi. Tukizungumzia tu Shule, maana yake unazungumzia Mwalimu na mwanafunzi.

Kwa msingi huo, tuwaangalie wote wawili, kuhakikisha kweli mtoto anafundishwa vizuri, lakini kwanza kwa kumwandaa vizuri Mwalimu, aangaliwe, apate haki zake ili aweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawaomba Waheshimwia Wabunge, muipokee Taarifa yetu, kama tulivyoshauriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo katika taarifa hiyo.

Mheheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ZABEIN O. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii - Mheshimiwa Mama Margaret S. Sitta kwa hotuba yako nzuri. Wanaotusikiliza, wasiokumbuka vizuri zaidi, alikuwa ni Rais wa Chama cha Walimu na pia alikuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, muda siyo mrefu sana uliopita. *(Makofi)*

Sasa naenda katika kulihoji Bunge kwamba lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo katika taarifa hiyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii pamoja na mapendekezo namaoni yaliyomo katika taarifa hiyo ilikubaliwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wajeshimiwa Wabunge, Taarifa hii ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kwa kweli imekubaliwa na Bunge rasmi. Tunaitakia kila la heri Kamati ya Huduma za Jamii, tunawatakiwa kila la heri Wizara zote mbili zilizo chini ya Kamati hii; Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa kazi njema kwa mwaka huu unaofuata. Tunatumaini mtakapokutana mwaka 2014, wakati wa mjadala wa Taarifa za Kamati hizi, mambo mengi mazuri yaliyoshauriwa na Waheshimiwa Wabunge, yatakuwa yamefanyiwa marekebisho makubwa.

Waheshimiwa Wabunge, wakati Mama Margareth Sitta ana-*wind up* alisema jambo moja zuri akanikumbusha mbali kwamba anatamani kwamba ifike siku moja tutakaposema kama Taifa la Elimu Kwanza. Sasa

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



akanikumbusha mbali enzi hizo nikiwa kwenye Chuo kimojawapo huko, tuliwahi kupewa swali na Mwalimu wetu, tulikuwa wanafunzi wa nchi mbalimbali, swali likawa linasema, chukulia wewe ni Waziri wa Fedha wa nchi yako, na unapanga bajeti ya nchi: Je, kipaumbele chako kitakuwa ni nini? Huduma za jamii au huduma za kiuchumi, na kwa nini?

Kwa kifupi jibu ilikuwa ni kwamba utapanga fedha zaidi kwenye huduma za kiuchumi kwa sababu ukiwawezesha wananchi wako kiuchumi, wakinyanyuka kiuchumi, wanaweza wao wenyewe sasa wakahudumia zaidi familia zao katika afya na katika elimu. Lakini leo majibu yanaweza kuwa tofauti. *(Makofi)*

Naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Mheshimiwa Mtanda, karibu sana na jitahidi pia kutumia muda vizuri, una kama dakika 20. *(Makofi)*

**MHE. SAID M. MTANDA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ili niweze kutumia dakika 20 kuhitimisha hoja yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kabisa kwa kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna walivyoipokea na kuijadili taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa kina kwa uwazi.

Napenda pia kuwahakikishia kuwa maoni yao, ushauri na mapendekezo waliyoyatoa yatafanyiwa kazi na Kamati hii na kwa namna ya pekee kwa kuwa wachangiaji hawakuwa wengi, ningependa kuwatambua kwa majina yao.

**NAIBU SPIKA:** Waruke tu kwa sababu ya muda.

**MHE. SAID M. MTANDA - MAKAMU MWENYEKITI - KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ni wachangiaji kumi na mbili na kwa hiyo ningependa kuwatambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba sasa kujielekeza kwenye mambo makubwa matatu ambayo yamekuwa ni sehemu ya mjadala katika Bunge letu kutokana na hoja ambayo niliwasilisha mapema asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni kuhusu pensheni kwa wazee. Bado Kamati yetu inaendelea kuamini kwamba jambo hili muhimu na ni lazima Serikali ilichukulie kwa upeo mkubwa ili kuhakikisha mipango ambayo tumeelezwa na Wizara inayohusika na ratiba iliyotolewa inatekelezwa ili wazee wetu waweze kuishi katika mazingira bora na salama zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni ilitoka ripoti ambayo inaonesha kwamba nchi yetu Tanzania ni miongoni mwa nchi duniani ambapo siyo sehemu salama sana kwa kuishi kwa wazee. Kwa hiyo, Kamati yetu inatambua mazingira hayo hatarishi na usalama kwa wazee hasa ukosekanaji wa huduma bora za afya kwa wazee ingawa yapo maelekezo mbalimbali ya Serikali kuhusu kuwapatia matibabu bure wazee, lakini bado wazee hao wamekuwa wakipata usumbufu mkubwa katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati yetu inaendelea kubaini kwamba wazee hawa kiasi cha milioni 2.1 sio wazee wengi endapo kutakuwa na utashi mkubwa wa kisiasa na kufanya maamuzi ambayo yanaweza kusaidia kuliangalia kundi hili kwa jicho pevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili bado ni nyeti na tunaendelea kuishauri Serikali kuendelea kulipa kipaumbele na kuleta Muswada utakaopelekea kuanzishwa kwa sheria kwa sababu sasa tunayo Sera ya Wazee, lkini bado hatuna

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



sheria ambayo inaweza kutekelezwa kupitia sera hiyo. Kwa hiyo, hilo ni namba moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili au hoja namba mbili ambayo imejitokeza zaidi katika Kamati na katika mjadala ni kuhusu suala la *TBC*. Bado Kamati inaendelea kuiomba Serikali kuhakikisha kwamba chombo hiki cha Umma kinapewa fedha, lakini pia usimamizi wa karibu ili kiweze kujiendesha na ili kiweze kushindana kwa kutoa taarifa zilizo bora zaidi lakini pia kutosahau malengo ya msingi ya kuanzishwa kwake. Kwa hiyo, tunaomba Serikali bado iendelee na mipango madhubuti katika kukinusuru chombo hiki.

Tumeeleza mara nyingi kuhusu madeni sugu, tumeeleza zaidi kuhusu pia namna miradi ya kimaendeleo isivyotekelezwa kupitia *TBC*, tumeitaka pia Serikali kutoa udhamini kwa *TBC* iweze kushirikiana na *NSSF* ili waweze kukarabati lile jengo la Mikocheni. Ni jambo kubwa ambalo Kamati yetu inaendelea kutoa msisitizo kwa Serikali na kuomba Bunge hili kuliangalia kwa macho mawili kwa sababu ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha ukifika katika Ofisi za *TBC*, wakati mwingine hata matangazo ya *TBC* yanakuwa katika hali ya mgando, dakika mbili au tatu, kwa hiyo, inapoteza hata ile heshima ya chombo hiki kwa waangaliaji wake na kwa Taifa letu. Tunaomba Serikali iendelee kutoa umuhimu wa pekee kwa chombo hiki na zile fedha za maendeleo zitolewe kama ambavyo zilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ambalo Kamati imeona iendelee kutoa msisitizo kwao, ni suala la *withdraw,* yaani kujitoa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Maeneo ambayo tumekwenda na kujifunza, wenzetu hawana kabisa utaratibu wa kujitoa. Badala yake kuna *supplementary schemes* ambazo unaweza kuweka fedha yako na baadaye kuzitoa endapo una mahitaji nazo. Nchi kama China tumeona namna ambavyo

wafanyakazi wanawekeza fedha zao ili kuendelea kupata mafao ya uzeeni. Lakini kunakuwa na akaunti maalum ambayo unaweza kujitoa muda wowote; Akaunti ya Matibabu au Akaunti ya Elimu endapo una mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya kusomesha watoto.

Kwa hiyo, tungeshauri pia na tunaendelea kuiomba Serikali na kushirikiana na mifuko yetu iweze kuwa na *supplementary schemes* au madirisha maalum ambayo yanaweza kumsaidia mwanachama pindi anapokuwa na matatizo. Kwa hiyo, suala hili ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maoni ya jumla ambayo yalitolewa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali, lakini nitambue maoni ambayo yalitolewa na Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mbunge wa Kigoma Kaskazini akishauri juu ya uanzishwaji wa *National Farmers Social Security Scheme,* ambayo lengo lake ni kusaidia wakulima kuweza kupata fedha kwa ajili ya mikopo ya pembejeo, madawa na kadhalika.

Kwa hiyo, jambo hili Kamati yetu imeona ni ushauri mzuri, tumeuchukua na tutaufanyia kazi kwa kushirikiana na wadau wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii lakini pia tutakutana na tutatoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuona namna ambavyo wanaweza kutengeneza dirisha maalum ili kuweza ku-*accomodate* watu hawa ambao Mheshimiwa Mbunge ameshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo maeneo mbalimbali ambayo Mheshimiwa Salum Barwany alizungumzia kuhusu ukatili wa watoto wenye ulemavu wa ngozi au *Albino* na Kamati yetu bado inashauri kwamba vituo hivi ni muhimu, viwepo lakini ni lazima Serikali ifanye tathmini kuona ubora wa vituo hivyo na mazingira yaliyopo pale na hatimaye kuweza kuchukua hatua badala ya kuvifunga kwa sababu kwa kufanya hivyo ni kuwaondolea ulinzi ambao ulitarajiwa kwa vijana hawa wenye ulemavu wa ngozi, yaani *Albino*.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa naelekea kuhitimisha, naomba pia nitambue mchango uliotolewa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde, maarufu kama Msumari wa Moto na siyo Kibajaji tena; ambapo yeye ameshauri mifuko hii iweze kuwekwa katika Wizara moja kwa uangalizi, yaani Wizara ya Kazi na Ajira, wazo ambalo hata Mheshimiwa Mbunge Zitto Kabwe amelitoa.

Sisi kama Kamati tumeafiki na imekuwa ni kilio cha muda mrefu cha Kamati yetu kwamba haiwezekani Mifuko hii iwe inawajibika katika maeneo mawili au matatu tofauti. *PPF* wako Wizara ya Fedha na *NSSF* wako Wizara ya Kazi na Ajira. Kwa hiyo, kwa maana ya Sera tungeshauri kwamba Mifuko hii yote iangaliwe au iwe chini ya usimamizi wa Wizara ya Kazi na Ajira ili kuleta ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Lusinde kwamba Kamati hii haijadharauliwa na Kamati hii ni muhimu na nyeti, tofauti na mawazo ambayo aliyaeleza hapa kwa sababu tu Kamati ilipewa muda mfupi wa kuwasilisha hoja zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hilo nadhani Ofisi yako itaweka utaratibu mzuri zaidi wa kutoa muda wa kutosha kwa Kamati hii kutokana na unyeti na kutokana vilevile na majukumu mengi yanayohusu maendeleo ya jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimalizie kwa kumtambua Mheshimiwa Cecilia Paresso ambaye ametoa ushauri ambao tumeupokea na Wizara pia imeueleza. Pia, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa ametueleza hapa kwamba Taifa hili ni la watu ambao wako *stressed, depressed*. Lakini nataka nimhakikishie tu kwamba Taifa hili siyo la watu ambao wana *stress*, hawana *depression,* lakini yeye kama mtu binafsi, anaweza kuwa anakabiliana na matatizo ya namna hiyo, ni masuala ya kawaida na ni mambo ya kiubinadamu, lakini kama Taifa, Taifa hili ni imara na lina watu imara wenye afya safi na salama, kwa hiyo, sina hakika kwamba tuna *stress* na *depression*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho natoa shukurani zangu kwako kwa namna ulivyotupa nafasi ya kuwasilisha hoja hii na nawaomba sasa Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako kuridhia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yangu na maboresho ambayo yamefanyika ili tuweze kwenda sambamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Said Mtanda - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa kusoma vizuri na kuhitimisha hoja yako kwa niaba ya Kamati yenu.

Waheshimiwa Wabunge, ninachotaka kufanya sasa ni kuwaomba mpokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo katika taarifa iliyowasilishwa.

*(Hoja iliamuliwa na Kukubaliwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu UtekelezajiwaShughuli zake kwa Mwaka 2013 Ilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Niwatakie kila la kheri Kamati kwa kazi ya mwaka unaofuata sasa na vilevile Wizara zote ambazo zinawajibika katika Kamati hiyo muhimu ya Maendeleo ya Jamii. Tuwatakieni kila la kheri.

Matumaini yetu ni kwamba mapendekezo na maoni ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge ambayo ni mazuri sana, kwa kweli mengi hayatajirudia tena katika ripoti ya Kamati mwakani ili tuwe tumepiga hatua fulani tuondokane na kulalamika, turekebishe yale ambayo yanaweza kabisa kurekebishika. Hiyo itatusaidia kwenda mbele kwa sababu Kamati hizi ni za msingi sana na Wizara hizi ambazo ziko chini ya Kamati hii ni za msingi vilevile. Lazima tuzipe nafasi yake mahali pake.

Kwa maelezo hayo, kwa kazi zilizopangwa kwa siku ya leo zimekamilika zote na naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi Jumatatu.

*(Saa 1.30 jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 16 Desemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*